

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Nne - Tarehe 6 Aprili, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe.Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Tukae, Katibu.

NDG.YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali, Waheshimiwa karibuni kwenye Mkutano wetu, kikao chetu cha nne na swali letu la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

Na. 24

Ujenzi wa Vituo Vya Afya Ikuti na Ipinda

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi unaoendelea katika Vituo vya Afya Ikuti, Wilayani Rungwe na Ipinda Wilayani Kyela utakamilika ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kupata huduma kwa wakati?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Ikuti kimekarabatiwa katika awamu ya kwanza ya ukarabati wa vituo vya afya 44 ulioanza tarehe 10 Oktoba, 2017 na kukamilika tarehe 31 Januari, 2018 kwa gharama ya shilingi milioni 500 ili kuongeza huduma za upasuaji wa dharura kwa mama wajawazito. Aidha, shilingi milioni 220 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba vya upasuaji na samani. Kituo hicho kinaendelea kutoa huduma zote za matibabu isipokuwa huduma za upasuaji wa dharura. Ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya Ikuti umekamilika na kinachosubiriwa kwa sasa ni vifaatiba kutoka Bohari ya Dawa (*MSD*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo cha afya cha Ipinda ulianza Oktoba, 2017 katika ujenzi huu jumla ya majengo mapya nane yamejengwa pamoja na ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje, uwekaji wa miundombinu ya maji safi na majitaka, kichomea taka na ujenzi wa njia zinazounganisha majengo (*walk way*). Jumla ya shilingi 625,899,806 zimetumika mpaka sasa katika mchanganuo ufuatao; Serikali Kuu shilingi 500,000,000, Halmashauri pamoja na wadau shilingi 90,100,975.40 na wananchi 35,798,830.60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majengo hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela imepokea vifaatiba kutoka *MSD* vyenye thamani ya jumla ya shilingi 73,909,900 na vilivyosalia vinatarajiwa kupatikana mnamo mwezi huu wa nne. Vilevile Halmashauri imenunua vitanda 47, magodoro na mashuka vyenye thamani ya shilingi 27,066,500 ambavyo vimefungwa na vinatumika katika majengo hayo. Kituo cha Afya Ipinda kinaendelea na ujenzi wa miundombinu kwa gharama ya shilingi milioni 500 ambao unahusisha kupanua huduma za upasuaji wa dharura na shilingi milioni 220 zimetolewa kwa ajili ya vifaatiba vya upasuaji na samani. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri bado kuna shida katika ujenzi unaoendelea pale Ipinda, nilikuwa nataka kujua Serikali imefuatilia gharama ya pesa ilizotoa na uhalsia wa majengo yanayojengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ujenzi wa zahanati ni kitu kingine, lakini utendaji wa wafanyakazi ikiwemo madaktari ni shida hasa Zahanati ya Ikuti Rungwe na hapo Ipinda hakuna watendaji wa kazi. Ni lini Serikali itatoa wafanyakazi ikiwemo madaktari na hasa Madaktari Bingwa wa wanawake kusaidia wanawake wa Wilaya ya zahanati ya Ipinda lakini pia Zahanati ya Ikuti Wilaya ya Rungwe?

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge naombeni muwe mnaenda *straight* kuuliza maswali ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Katika swali lake la kwanza anauliza iwapo Serikali imefuatalia kujua gharama iliyotumika na majengo ambayo yamejengwa. Majengo ambayo yanajengwa ni kwa mujibu wa ramani ambayo imetolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na ni na suala ambalo matarajio yangu makubwa na Mheshimiwa Mbunge akiwa ni sehemu ya wananchi wa Halmashauri ile ni vizuri akatuambia ni sehemu ipi ambayo anadhani kwamba haridhiki, lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea hata Mbunge wa Jimbo hajaleta malalamiko yoyote kwamba labda kuna ubadhilifu katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anaongelea juu ya suala zima la upatikanaji wa wataalam, suala la kujenga majengo jambo moja na suala la wataalam

jambo la pili, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni nia ya Serikali kuhakikisha pale tunapomaliza ujenzi na wataalam wapatikane kwa mujibu wa Ikama na jinsi mahitaji yanavyopatikana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ungando.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza sina budi kushukuru vyombo vya ulinzi na usalama hasa Kibiti tunalala usingizi.

Swali langu la nyongeza Kituo cha afya kibiti hasa kinazidiwa kutoa huduma, je, Serikali ina mpango gani wa kujengea Kibiti Hospitali ya Wilaya?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli huko uhitaji mkubwa sana na kituo cha afya kilichopo kimezidiwa, naomba nimuondoe mashaka Mheshimiwa Mbunge na nimuhakikishie mionganoni mwa hospitali 67 zinazotarajija kujengwa ni pamoja na Wilaya yake, kwa hiyo, wakae mkao wa kula Serikali inatekeleza ili kuondoa shida kwa wananchi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu nilipata ahadi kutoka Wizara hii kwamba kutapelekwa hela za ujenzi kituo kile cha Mchombe katika Jimbo la Mlimba kiliwekwa katika mpango wa Serikali na kilipata zile *grade* ambazo zinafaan kupewa pesa ili kuboresha Kituo cha Afya cha Mchombe ambapo kinahutubia kata zisizopungua 10. Je, na katika mpango uliopita hakuna hela iliyopelekwa, mimi tu mfuko wa jimbo nilipeleka hela kidogo kwa ajili ya kusaidia...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Je, ni lini sasa Wizara ya afya itapeleka pesa za kuimarisha Kituo cha Afya cha Mchombe ndani ya Jimbo la Mlimba?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Kiwanga swali lake la nyongeza juu ya ahadi ambayo anasema ilitolewa, sina uhakika juu ya ahadi hiyo, lakini kama ahadi hiyo imetolewa kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba nimuhakikishie hivi karibuni ni kama nilivyojibu swali la nyongeza jana la Mheshimiwa Mipata kuhusiana na kituo chake cha afya Kasu kuna matarajio ndani ya mwezi huu kuna pesa ambazo zitapatikana kwa ajili ya vituo vya afya visivyopungua 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sina uhakika kama katika hivyo 25 na yeche ni mionganini mwa hivyo ambavyo vinaenda kupelekewa pesa.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa swali linalofuata linaelekezwa Ofisi ya Rais hapo hapo TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 25

Serikali Kusaidia Vikundi vya Wanawake Rukwa

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia vikundi vya wanawake waliopo katika Mkoa wa Rukwa katika suala la mikopo na kuwapatia elimu ya ujasiriamali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi nya wanawake vinawezeshwa kupitia mfuko wa wanawake unaotokana na asilimia tano ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Sambasamba na hilo Serikali inawahimiza Maafisa Maendeleo ya Jamii kuendelea kutoa elimu ya ujasiliamali kwa vikundi nya wanawake ili kuwajengea uwezo, kuibua miradi yenye tija itakayosaidia kupata kipato na kurejesha mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 vikundi nya wanawake 55 vyenye wanachama 698 vimepatiwa mikopo ya shilingi milioni 56.87 kati ya shilingi bilioni 6.5 zilizokusanywa kutokana na mapato ya ndani katika Mkoa wa Rukwa.

Vilevile katika mwaka wa fedha 2017/2018 vikundi 33 nya wanawake vimepatiwa mikopo yenye jumla ya shilingi milioni 118 kati ya shilingi bilioni 4.2 ya makusanyo ya mapato ya ndani hadi machi, 2017 sawa na asilimia 2.78.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kutoa maelekezo kwa Halmashauri kuimarisha makusanyo kwa kutumia mifumo ya kielektroniki iliyowekwa katika Halmashauri zote 185 na kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa kwenye mfuko kila zinapokusanywa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwakang'ata swali la nyongeza kama unalo.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa wanawake wengi wamehamasika sana kuanzisha VICOBA na wengine wameanzisha vikundi mbalimbali kwa lengo la kujkwamua kimaisha lakini wamekuwa wakiangaishwa sana kwa kupata hiyo asilimia 10; sasa ni lini Serikali itaweka mazingira mazuri ili hata kama hiyo asilimia 10 ipo lakini wawekewe mazingira mazuri ya kupata mikopo kwenye mabenki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa asilimia 10 ya wanawake, walemavu na vijana inachelewa sana kuwafikia walengwa; sasa basi kwa nini Serikali isipunguze masharti ya kukopa kwenye mabenki ili wanawake waweze kukopa?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba ukilinganisha masharti yaliyopo katika upatikanaji wa hii asilimia tano ambayo imekusudiwa kwenda kwa wanawake na vijana masharti yake ni rahisi sana ukilinganisha na masharti ambayo yanatolewa na taasisi za fedha kama mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoomba kumekuwa na dhana potofu kama vile fedha hizi zinatolewa kama vile ni pesa ambayo haitakiwi kurejeshwa, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunasimamia ili pesa hizi zinazotolewa ziweze kurejeshwa na wengine waweze kukopeshwa, vizuri tukawa na mfumo ambao ni rasmi ili kuhakikisha kila shilingi ambayo inatolewa inarudi ili wakinamama wengine waweze kukopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili angependa masharti ya benki yakapunguzwa ili wakina mama waweze kuna *access* ya kwenda kukopa kwenye taasisi hizi za fedha. Hili ambalo lipo ndani yuwezo wetu kama ofisi ya Rais TAMISEMI ni kuhusiana na asilimia tano kama ambavyo swali lake la msingi lipo ni vizuri kwanza tuhakikishe

kwamba fedha hizi ambazo zinakusanya wa asilimia tano inatengwa na zile zinazotengwa zinakopwa ikionekana kwamba kuna *gap* ya uhitaji hapo ndio twende kwenye taasisi zingine za fedha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sambasamba na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI ni kwamba katika mwezi huu wa tatu Mheshimiwa Rais alikaa na wadau mbalimbali wenye masuala ya kibashara na viwanda katika moja ya jambo ambalo alizungumza ni kuwashauri watu wa mabenki kuweza kupunguza riba na kuweka masharti ambayo yatawasaidia zaidi wafanyabiashara. (*Makofii*)

MENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa sasa nihamie hapo Mheshimiwa Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi naomba nimuulize Mheshimiwa naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mfuko huu wa kina mama na vijana unatakiwa uchangiwe na maeneo mawili kwa maana ya Serikali Kuu itoe fedha kwa ajili ya ule mfuko lakini pia Halmashauri zetu zitoe asilimia 10 kwa ajili ya ule mfuko. Kwa baadhi ya Halmashauri ikiwepo Kaliua tunajitahidi sana kutenga ile asilimia 10 lakini Serikali haitoi ile sehemu yake.

Je, Serikali haioni kwamba kutokutenga ni kuendelea kudumaza wanawake na vijana kutokupata mikopo kwa kiasi kinachotakiwa? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa

Mwenyekiti, swali la msingi lilivyo ni juu ya Halmashauri kuhakikisha kwamba wanatenga asilimia 10 na yeye katika Halmashauri yake anasema wamekuwa wakitenga hii asilimia 10 kwa uzuri zaidi.

La kwanza ambalo naomba tuhamasishe na kuagiza Halmashauri zote ni kuhakikisha kwamba wanaiga mfano mzuri kama ambavyo Halmashauri ya Kaliua inafanya ili kwanza tuwe na uhakika katika hii asilimia 10 ambayo inatengwa, je, inawafikia akina mama na baada ya hapo tukiwa na uhakika na mfumo ambao ni rasmi unatumika Serikali haitasita kwa sababu lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba inawakomboa wanawake na vijana na ndio maana sheria ilipitishwa ili kuhakikisha kwamba tunawawezesha wanawake na vijana katika suala zima la uchumi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Koshuma Kiteto.

MHE.KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana; kwa kuwa Halmashauri nyingi sana zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na mapato madogo na hivyo kushindwa kabisa kutenga fedha hizi za asilimia 10, asilimia tano wka vijana na asilimia tano kwa akina mama kwa ukamilifu.

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Halmashauri ambazo hazitengi kabisa na hata tuliona katika bajeti ya mwaka jana kuna Halmashauri mbili zilikuwa zimetajwa kwamba hazijatenga kabisa fedha hizi za akinamama na watoto, lakini hatujaona Serikali ikiwachukulia hatua. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Halmashauri ambazo hazitengi kabisa fedha hizi za akina mama?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu kwa kifupi tu, adhabu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna *excuse* yoyote ambayo itasababisha

Halmashauri isamehewe eti kwa sababu makusanyo yake ni kidogo. Kwa sababu hata kama ungekusanya shilingi moja, shilingi moja hiyo tunachotaka asilimia 10 ya shilingi moja si ya kwako. Wewe ni kama *conduit* tu unatakiwa pesa hiyo iende kwa wanawake na vijana.

Kwa hiyo, kama ambavyo tulisisitiza juzi katika jibu ambalo alijibu mwenzangu tutachukua hatua kali kwa Halmashauri yoyote na hasa Wakurugenzi wahakikishe kwamba asilimia 10 ya kutenga katika mapato ya ndani sio *option, it's a must!* Na yejote ambaye hatatekeleza hilo hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa Wizara ya Katiba na Sheria.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naona umemuacha Kigoda. Naomba nianze halafu Kigoda afuate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba swali langu Na. 27 sasa lipatiwe majibu kwa niaba ya wanawake.

Na. 27

Serikali Kuzitambua Sheria Zilizopitwa na Wakati

MHE. AMINA N. MAKILAGI aliuliza:-

Zipo sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati na sheria nyingine ni kikwazo katika kufanikisha shughuli muhimu za Taifa letu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzitambua sheria zote zilizopitwa na wakati na zile zinazochelewesha ukuaji wa uchumi?

MWENYEKITI: Ahsante, nimeruka swali nitarudi, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri Antony Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakati wote imekuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinapitiwa na kufanyiwa marekebisho kadri inavyohitajika ili kukidhi mahitaji. Mkakati huo unasimamiwa na Wizara kuititia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania illyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171. Tume hii ni chombo mahsus cha Serikali chenye kazi ya kusimamia mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1983, Tume ya Kurekebisha Sheria imefanikiwa kuandaa ripoti 37 za mapitio na marekebisho ya sheria mbalimbali na kuziwasilisha Serikalini ambapo baadhi yake zilishatungiwa sheria na nyingine zinaendelea kufanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya mapitio ya sheria ili kubaini sheria zilizopitwa na wakati na hatimaye kupendekeza marekebisho, kutunga sheria mpya au kufutwa kwa sheria ni endelevu na imekuwa ikifanyika muda wote ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Makilagi.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amethibitisha kwamba kweli ziko sheria ambazo zimeshapitwa na wakati na Tume ya Kurekebishesha ya Sheria ya Serikali inaendelea kuzifanyia marekebishesha. Ningependa kujua ni sheria gani hizo sasa ambazo ziko katika huo mchakato na pia ningependa kujua hizi sheria zinaletwa hapa lini ili Bunge lako tukufu liweze kuzipitisha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa kuwa kumekuwa na kilio cha muda mrefu na hata leo Mheshimiwa Mwenyekiti imethibitisha kwamba kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha Waheshimiwa Wabunge Wanawake na Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumekuwa na kilio kikubwa sana cha wanawake na vijana juu ya kutungwa sheria ya mfuko wa wanawake na vijana na walemau. Lakini pia kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha wakulima wadogo wadogo kwamba kilimo chao hakiwaletei tija kwa sababu hakuna sheria inayoweka mfumo mzuri wa wakulima wadogo waweze kuletewa tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua sasa. Serikali ina mkakati gani wa kuleta hizi sheria Bungeni. Hili suala la kuwa kila siku tunaambiwa Serikali itaweka msukumo kuhakikisha asilimia 10 ya wanawake na vijana inatengwa ili tuweze kufikia mahali panapohitajika. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya akina mama nchini na ni kazi kubwa amekuwa akiifanya kwa ajili ya akina mama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la kwanza anauliza ni sheria gani zipo katika mchakato. Kama nilivyo sema, kazi kubwa ya Tume ya Kurekebishesha Sheria ni

kupitia sheria na baadaye kutoa mapendekezo kupitia taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha Tume inafanya kazi ya mapitio ya sheria za mambo ya jinai (*criminal justice*) wanafanya pia mapitio ya sheria ya mambo ya *evidence law*, utoaji wa ushahidi mahakamani, lakini pia wanafanya mapitio ya sheria ya ufilisi (*insolvency law*) na vilevile wanafanya mapitio ya sheria ya huduma za ustawi wa jamii. Kwa hiyo, hizo ndiyo kazi ambazo zinafanyika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, katika swalii lake la pili ameuliza kuhusu lini Serikali italeta sheria mahsusii kwa ajili ya utungwaji wa uundwaji wa mifuko hii maalum kwa ajili ya akinamama na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Naibu Waziri kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mifuko ya akina mama na vijana ipo na inaongozwa na miongozo yake tayari na imekuwa ikifanya kazi katika utaratibu huo wa kuchangia asilimia 10 hizo za mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwongozi tayari upo. Labda ambacho kinawenza kikafanyika ambapo Serikali imekuwa ikijibu hapa ni kuboresha na kuona namna bora ya kuweza kuwafikishia kwa urahisi zaidi akina mama na vijana huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wakulima wadogo wadogo kutungiwa sheria. Kama Serikali tunaichukua na tutaona umuhimu wake hapo baadaye wa kuweza kulifanyia kazi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wangu. Tunaendelea, mniwie radhi narudi kwenye swalii namba 26 na nimuombe radhi sana Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda ambaye ndiye anauliza swalii. Linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 26

Hitaji la Gari la Wagonjwa Hospitali ya Handeni

MHE. OMARI A. KIGODA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa (*ambulance*) kwenye Hospitali ya Wilaya ya Handeni hasa ikizingatiwa hospitali hiyo inahudumia wagonjwa wengi kutoka takribani majimbo manne?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda Mbunge wa handeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji Handeni ina gari moja la wagonjwa lenye namba za usajili SM 11322 ambalo linatoa huduma kwa wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni. Gari hilo kwa sasa liko katika matengenezo Mjini Tanga baada ya kupata hitilafu. Taratibu za matengenezo zinaendelea kufanyika ili liendelee kutoa huduma kwa wagonjwa. Katika hali ya dharura, Halmashauri inatumia magari ya kawaida kutoa huduma kwa wagonjwa hadi hapo gari la wagonjwa litakapotengemaa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kigoda.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Handeni inahudumia karibia majimbo manne; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali hili ni suala la dharura haoni kwamba kuna umuhimu wa sisi kupata *ambulance* badala ya kutumia haya magari ya kawaida ambayo muda mwingi

vifo hutokea njiani kwa sababu sio magari *special* ya kusafirisha wagonjwa? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ndugu Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba uko uhitaji mkubwa sana wa gari la wagonjwa na pia ni ukweli usiopingika kwamba uwezo wa Halmashauri kuweza kununua gari jipya kwa sasa hivi ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulitambua hilo ndiyo maana Halmashauri ya Handeni imetuma ombi maalum Wizara ya Fedha ili kuomba gari la wagonjwa liweze kununulliwa. Naamini hali ya bajeti ikitengemaa ombi lao litawenza kujibowi na wagonjwa waweze kupata gari ambalo litakuwa linamudu kwa mazingira ya Wilaya ya Handeni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwanausi, Mheshimiwa Maige na mwisho Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lulindi nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kuwa Kituo cha Afya cha Nagaga kilichopo katika Jimbo la Lulindi, Wilayani Masasi liliungua moto miaka mitano iliyopita. Je, Serikali haioni umuhimu sasa katika mgao huu wa magari yaliyopatikana kupeleka katika Kituo cha Afya cha Nagaga ili huduma za afya ziendelee kuboreka? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uko uhitaji mkubwa sana wa magari ya wagonjwa. Kama ambavyo Serikali ingependa yote tukaweza kuyatatua kwa mara moja, lakini pia ni ukweli

usiopingika kwamba bajeti hiyo kwa sasa haiwezekani kwa wakati mmoja tukatekeleza yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge ajue nia njema ya Serikali ndiyo maana katiak orodha ya Wilaya zile 27 ambazo zinaenda kujengewa Hospitali za Wilaya ni pamoja na Wilaya yake. Kwa hiyo, aelewe dhamira njema ya Serikali na kadri uwezo utakavyokuwa unajitokeza hakika hatutawasahau.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Maige.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiografia ya Jimbo na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala wewe unaifahamu lakini pia hata Mheshimiwa Kandege anaifahamu kwamba vituo vya afya vimejengwa sana na wananchi na hivi sasa tuna vituo vya afya vitatu, cha Isaka, Ngaya na Bugarama. Lakini vituo vyote hivi havina gari la wagonjwa na kwa Halmashauri nzima gari ambalo linafanya kazi ni gari moja tu. Wananchi wamefanya kazi kubwa na wanaamini Serikali yao pia inaweza ikawashika mkono.

Kwa hiyo, nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri unawaahidi nini wananchi hawa angalau kuwapatia gari angalau kwenye kituo kimoja katika hivi vitatu nilivyovitaja?

MWENYEKIT: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Halmashauri za kupigiwa mfano na kama kuna Wabunge ambao wanatakiwa wapongezwe ni pamoja na Mheshimiwa Maige. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika Halmashauri ambazo wamejenga vituo vya afya vingi, hongereni sana.

Pia nimuombe Mheshimiwa Maige kwa kushirikiana na Halmashauri yake, natambua uwezo mkubwa wa Halmashauri yake hakika wakiweka kipaumbele kama ni suala la kununua gari hawashindwi na wengine wataiga mfano mzuri ambao wao wanafanya na hasa katika *own source* zao ambao wanapata mapato mazuri ni vizuri katika vipaumbele wakahakikisha wananchua na gari la wagonjwa kwa ajili ya kusaidia wananchi wa Msalala.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale yene keta 20 na kituo kimoja cha aya haina gari ya wagonjwa. Shida tullyonayo ni kubwa sana ukizingatia mtawanyiko wa kata zetu zile pale Wilaya ya Liwale mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi, umefika, umeona jinsi shida ya Wilaya ya Liwale ilivyo juu ya kupata gari la wagonjwa. Ni lini sasa Serikali itatupatia gari la wagonjwa katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Liwale? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fursa nikiwa nahudumu katika nafasi ya Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimepata nafasi ya kwenda Liwale na tukakutana na Mheshimiwa Mbunge katika kazi nzima ya kujenga kituo cha afya na muitikio wa wananchi wa Liwale ni mkubwa sana katika kujitolea katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwa *spirit* niliyoionna na hakika na mapato ambayo wanapata kutokana na zao la korosho na wakasimamia vizuri kabisa mapato ya kwao na kituo kile cha afya kikamilika hitaji la kwanza la wananchi naomba nimuagize Mkurugenzi katika

vipaumbele vyake vya kwanza ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanunua gari la wagonjwa kwa sabbau wezo upo, pesa zikisimamiwa vizuri, kulikoni kuishia kugawana kama posho hakika uhitaji mkubwa wa gari la wagonjwa wafanye kama kipaumbele.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Tunarejea tena Wizara ya Katiba na Sheria na swali linaulizwa na Mheshimiwa Issa Ali Mangungu Mbunge wa Mbagala. Kwa niaba yake Mheshimiwa Kisangi.

Na. 28

Mabaraza ya Wazee Katika Mahakama za Mwanzo

MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. ISSA A. MANGUNGU) aliuliza:-

(a) Je, Mabaraza ya Wazee katika Mahakama za Mwanzo yapo kwa mujibu wa sheria?

(b) Mahakama ya Mwanzo Kizuiani hulipa posho za Wazee wa Baraza kiasi cha shilingi 5,000 kila wanapomaliza shauri. Je, kwa nini sasa yapata miezi tisa wazee katika Mahakama ya Mwanzo Kizuiani hawajalipwa posho zao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala lenye sehemu (a)(b) na (c) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Wazee wa Mahakama nchini yamehalishwa na sheria. Kifungu cha 9(1), (2) na (3) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 ya sheria za nchi kinaeleza kuwa kutakuwa na matumizi ya Wazee wa Mahakama katika Mahakama ya Mwanzo na Mahakama za Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mahakama ya Mwanzo ya Mbagala kama ilivyo katika Mahakama nyingine, malipo ya posho za Wazee wa Baraza yamekuwa yakipewa kipaumbele kulingana na upatikanaji wa fedha. Malipo haya yamekuwa yakifanyika kwa mkupuo wa miezi mitatu au minne ili kutoa fursa ya kuweka kumbukumbu za malipo baada ya mchakato wa kukokotoa malipo stahiki kwa kila mlipwaji kulingana na idadi ya mashauri yaliyomalizika ambayo mhusika ameshiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wazee wa Mahakama zote za Mwanzo katika Mkoa wa Dar es salaam ikiwemo Mahakama ya Mwanzo Mbagala walilipwa posho zao zote. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wazee wa Baraza katika Mahakama ya Mwanzo Mbagala wameshalipwa posho zao kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2017 kiasi cha shilingi 5,760,000. Villevile kiasi cha shilingi 2,840,000 ambacho ni madai ya wazee hao kwa kipindi cha Desemba, 2017 hadi Februari, 2018, kipo katika mchakato wa malipo na hivyo hakutakuwa na deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa umuhimu wa kipekee katika malipo ya posho ya Wazee wa Baraza ili kutokwamisha mashauri yaliyopo Mahakamani hususan kwa Mahakama za Mwanzo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa posho ya shilingi 5,000 kwa kila shauri ni ndogo sana ukilinganisha na wakati uliopo kuwalipa hawa wazee. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea posho hawa wazee wa Mahakama za Mwanzo shilingi 5,000 ni ndogo sana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wazee wanakuwa kwenye Mahakama kwa muda mrefu

sana kusikiliza mashauri hayo. Je, Serikali haioni haja sasa kubadili mfumo wa malipo, badala ya kuwalipa kwa miezi mitatu au minne kwa mkupuo, wawalipe kwa mwezi hadi mwezi yaani kwa mwezi mmoja mmoja? Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa niaba.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la kwanza la ongezeko la posho kutoka shilingi 5,000 kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wazee hawa wanafanya kazi kubwa kuisaidia Mahakama katika kufikia maamuzi na sisi kama Serikali tunatambua mchango wao mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba siwezi kutoa *commitment* ya Serikali hapa kuhusiana na ongezeko la hii fedha lakini pindi bajeti itakaporuhusu basi tunaweza tukaona namna ya kuweza kusaidia katika kuboresha eneo hili la kipato kwa wazee hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili la malipo ya mwezi kwa mwezi badala ya mkupuo. Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ni kwamba inafanyika hivi pia kwa ajili ya kupata kumbukumbu sahihi. Lakini vilevile pia inatokana sana na upatikanaji wa fedha kwa wakati kulingana na bajeti, tunalipokea wazo la Mheshimiwa Mbunge na Serikali tutaona namna ya kuweza kulifanyia kazi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Aida. Naanza na Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ukonga kwa sasa lina wakazi wanaokaribia 700 na tuna Mahakama ya Mwanzo moja tu pale ya Ukonga na kulikuwa na mpango mwaka jana kujenga Mahakama nyingine mpya ya Mwanzo kule

Chanika. Kwa hiyo, ningependa kujua kupertitia Mheshimiwa Naibu Waziri kama mpango huo wa kujenga Mahakama nyingine mpya pale ili kupunguza msongamano mkubwa kule Ukonga ukoje? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa Serikali wa mwaka 2017/2018; 2018/2019; 2019/2020 ni kuendelea kuongeza Mahakama nyingi za Mwanzo na Wilaya ili wananchi wengi waweze kupata huduma kwa wakati. Katika Mahakama ambazo zimeorodheshwa, pia Mahakama ambayo ni katika jimbo la Mheshimiwa Waitara ni kati ya Mahakama ambazo zilikuwa zimeainishwa katika wakati ujao wa fedha ili kuona namna ya kuweza kulishughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hivi sasa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria utaratibu ulioanzishwa sasa hivi ni ujenzi wa Mahakama kwa kutumia teknolojia rahisi sana ya moladi ambayo imerahisisha sana kujenga Mahakama nyingi kwa wakati mfupi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anaweza pia, kuwasiliana na mimi ili kuangalia katika orodha ya ujenzi wa Mahakama zile, Mahakama zake za Ukonga zimepangiwa mwaka gani wa fedha.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika majibu ya Naibu Waziri ameonesha kwamba anatambua mchango wa Wazee wa Mahakama. Hali kadhalika anatambua mchango wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua sasa kwa kuwa uchaguzi unapofanyika mnatenga fedha kwa ajili ya uchaguzi wa Wenyeviti wa Serikali, Madiwani, Wabunge pamoja na Rais, lakini hawa wote watatu wanalipwa kasoro

Wenyejiti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Ni lini sasa Serikali itaanza kuwalipa Wenyejiti hawa?

MWENYEKITI: Haya, ingawa ni swali jipya, sijui bwana. Ni swali jipya Mheshimiwa, sijui, utakuwa unamuonea sana mjibu swali, nadhani tuendelee.

Tunaendelea swali linalofuata, swali namba 29, linaulizwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum. Na linaelekezwa kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Na. 29

**Unyanyasaji Wanaofanyiwa Vijana wa Kike
Wanaokwenda Kufanya Kazi Nchi za Uarabuni**

MHE. MGENI JADI KADIKA aliuliza:-

Imekuwa ni mazoea sasa vijana wetu wengi, hasa wa kike wanapokwenda kufanya kazi za ndani katika nchi za Uarabuni kama vile Oman, Dubai na Saudi Arabia, kunyanyaswa na kuteswa na hata wakati mwingine wanaauawa.

Je, inapotokea kadhia hiyo, kwa nini Balozi wetu anaewakilisha nchi yetu hatoi taarifa mapema na inachukua muda mrefu kujulikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI NA
USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI aliijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyejekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyejekiti, nchi za kiarabu zimekuwa zinatoa fursa nyingi za ajira katika kada mbalimbali kwa Watanzania na Serikali inapata faraja kuona vijana wake

wanapata kazi hizo zinazowawezesha kuendesha maisha yao na familia zao. Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika baadhi ya maeneo wanayofanya kazi na haya yameonekana zaidi upande wa akina dada wanaokwenda kufanya kazi za ndani nchi za kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ripoti mbalimbali kuhusu kadhia wanazopata Watanzania walioajiriwa katika nchi za kiarabu, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kutoa vibali kuititia mamlaka zinazoshughulikia masuala ya ajira, ikiwemo Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TaESA*), kwa kushirikiana na Wizara zinazoshughulikia masuala ya kazi na ajira na balozi zetu zilizopo nchi mbalimbali huko Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya mikataba inayosainiwa na waajiriwa hao pamoja na waajiri wao na kushuhudiwa na Balozi zetu, haki za Watanzania zinalindwa ipasavyo na hutakiwa kuripoti Ubalozini pale ambapo waajiri wao wanakiuka mikataba hiyo, ikiwemo kunyanyaswa au kuteswa. Mara baada ya kupokea taarifa hizo Serikali kuititia Balozi zetu zilizopo maeneo hayo huchukua hatua za mapema kuwasiliana na muajiri pamoja na mamlaka husika katika nchi hizo katika kusimamia na kutetea maslahi ya Watanzania. Hivyo, ni muhimu Watanzania wote wakaelewa kwamba mikataba hii ina dhamira ya kuwalinda dhidi ya madhara yanayoweza kuwatoka, kama ajali na majanga mengineyo. Serikali itaendelea kudhibiti mawakala kwa lengo la kulinda maslahi ya Watanzania wanaochangamka fursa za ajira katika nchi mbalimbali na hivyo kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kukuhakikishia kuwa, balozi zetu hufanya juhudhi na kuchukua hatua za haraka katika kushughulikia masuala ya vifo yanapotokea na kujulikana na kutoa taarifa mapema kadiri zinapopatikana. Inawezekana kuna nyakati baadhi ya taarifa hizi, hasa za kiuchunguzi zinachelewa kupatikana kulingana na matukio au mazingira na utaratibu wa utendaji wa nchi

husika. Na endapo hilo linajitokeza, Serikali hulazimika kusubiri, lakini wakati hilo linafanyika ndugu pamoja na vyombo vinyavyohusika wanapewa taarifa kuhusu kinachoendelea.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kadika.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninayo maswali mawili tu ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, na Serikali ina nia nzuri tu ya kuwasaidia vijana na kuwapatia ajira, lakini kuna baadhi ya waajiri bado wanateswa wafanyakazi hao na wananyang'anywa simu wanapofika, *passport*, wanafungiwa ndani, hawajui waende wapi. Je, Serikali, ina mkakati gani wa kuifuartilia na kulikomesha tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Serikali inatuambia nini? Ni ubalozi upi ambao umefanikiwa kupambana na matatizo haya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anasema kuna baadhi ya waajiriwa huwa wakifika wananyang'anywa simu, *passport*, na kadhalika na kwamba Serikali ina mkakati gani juu ya kushughulikia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Balozi inapokuwa inapata taarifa za namna hiyo inachukua hatua na ninachokiomba tu kwa waajiriwa wote walioko katika nchi hizi za kiarabu, linapotokea tatizo kama hilo wataarifu Balozi, ndio maana tunasema wanapewa mikataba na mikataba ile inalinda haki zao, lakini pia inalinda wajibu wa mwajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kuhusu Ubalozi upi umefanikiwa kufanya hayo, balozi zote zinafanya kazi hizo. Cha muhimu ni kujua tu kama kuna changamoto au kuna kadhia yoyote wale waajiriwa wanatakiwa kutoa taarifa kwa

Balozi husika. Wao wanafanya kazi na sisi tunaendelea kufuatilia kwamba, wanatekeleza kzi yao ipasavyo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Bulembo.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, tuhuma hizi zimekuwa zikijirudia mwaka hadi mwaka na kwa muda mrefu. Nchi nyingi duniani huwatumia watu wake kwenda kufanya kazi nje ya nchi ili kuingiza *remitance*, fedha za kigeni. Mfano India ni nchi ambayo inaongoza dunia kwa *remitance*, inaingiza dola za Kimarekani bilioni 69. Je, ni kwa nini sasa Serikali yangu isione umuhimu wa kuingia makubaliano na nchi hizi zinazohitaji wafanyakazi, ili kukuza sekta hii, kuwalinda na kuiboresha zaidi? Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba nchi nyingi zimeingia mikataba na nchi ambazo zinaajri watu ambao wanatoka nje ya nchi nyingine na kwamba, wanapata *remitance*. Kama nilivyowaambia kwamba, sisi tumeweka makubaliano, yani kuna mikataba katika sisi pamoja na nchi hizi za kiarabu kwa hiyo, mikataba ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu tuweke utaratibu wa kuzihusisha nchi nyingine, nadhani zaidi ya hizi nchi za kiarabu, tutafanya hivyo na tunaupokea ushauri.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Ninaomba nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kipindi kirefu

tumekuwa sasa tukipokea hayo malalamiko ya namna Watanzania na baadhi ya wafanyakazi kutoka nchi nyingine za Afrika wanavyopata shida kule wanakokwenda kufanya kazi nje ya nchi zao. Huduma hii ya kuwaunganisha Watanzania na watafuta wafanyakazi nje ya nchi ya Tanzania inasimamiwa na Sheria ya Wakala wa Huduma za Ajira Na. 9 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa katikati, mwaka huu mwezi wa pili kwenda wa tatu, niisimamisha huduma hizo kwa nchi nzima ya Tanzania ili kufanya ukaguzi wa kutosha wa kujiridhisha kama wakala hawa wanafanya kazi zao kwa kufuata sheria. Wanafahamu Watanzania wanaoenda kufanya kazi huko nje wanaishije, wana matatizo gani na nini kifanyike ili kuwaokoa kwenye kadhia wanayoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliunda timu imefanya utafiti na matokeo hayo wameshaniletea. Tumegundua kwamba ziko fursa nyingi za ajira kule nje ya nchi yetu ya Tanzania kama vile Saudi Arabia, Qatar na nchi nyingine. Lakini aina ya ujuzi unaotakiwa kule nje kama tutajipanga vizuri ndani ya Serikali na ninalihakikishia Bunge lako tutaanza kufanya hivyo, tuna uwezo wa kuwapeleka Watanzania wengi kwa mikataba rasmi na wakarudisha mapato ya kutosha kwenye nchi yetu na wakapata ajira nje ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo tu; kule Saudi Arabia wanahitaji wafanyakazi takribani 2,000 wa ujuzi wa katni na ujuzi wa juu kwenye fani kama za marubani, madaktari, walimu, madereva na za kazi za namna hizo ambazo zina ujuzi.

Ninalihakikishia Bunge lako baada ya ripoti hii sasa tutajipanga sawasawa na Watanzania watapata ajira zenye staha nje ya nchi na watarudisha mapato ndani ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, kwa majibu hayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri nadhani

yametosheleza twende mbele. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, Mbunge wa Lupembe, na linaulizwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 30

Soko la Matunda – Lupembe

MHE. JORAM I. HONGOLI aliuliza:-

Katika Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Njombe, Tarafa ya Lupembe, hususan Kijiji cha Madeke kinazalisha matunda aina ya nanasi, parachichi na matunda mengine, lakini hakuna soko la matunda hayo na hii ni kutokana na kutokuwa na kiwanda kikubwa cha matunda.

(a) Je, Serikali inasaldiaje upatikanaji wa masoko ya mazao hayo?

(b) Je, ni lini Serikali italeta kiwanda katika eneo hilo?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia taasisi yake ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TANTRADE*) wakati wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyomalizika mwezi Julai, 2017 iliwaunganisha wakulima wa nanasi, parachichi na matunda mengine ambao wana uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 6,000 kwa mwaka na kampuni ya *Tomoni Farms Limited* iliyopo Jijini Dar es Salaam. Mwakilishi wa Kampuni ya Tomoni na mwakilishi wa Kikundi cha Wakulima wa Matunda kutoka Kijiji cha Madeke walitiliana saini ya mkataba usiofungani wa kununua wastani

wa tani 3,000 za matunda kwa mwaka zenye thamani ya shilingi billioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tomoni Farms Limited* ni kampuni kubwa inayonunua matunda na mbogamboga kutoka kwa wakulima mbalimbali nchini. Aidha, wakulima hao pia wameunganishwa na wanunuvi wa matunda kutoka nchi za uarabuni kwa ajili ya soko la nje.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa ujenzi wa kiwanda kwa ajili ya kusindika matunda katika eneo hili, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeanzisha kiwanda kidogo cha kukausha *chips* za nanazi. Kiwanda hiki kinamilikiwa na wanakijiji wa Madeke kupitia mradi uliobuniwa na mpango wa maendeleo wa kilimo wa wilaya (*District Agriculture Development Plans – DADPS*), hata hivyo kiwanda hiki bado hakikidhi mahitaji ya usindikaji wa zao hili na jitihada zimeendelea kufanyika, ili kupata wawekezaji, hususan katika Kijiji cha Madeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo katika kijiji hicho ni kukosekana kwa umeme. Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ilishawaandikia barua *TANESCO* kuweka katika mipango yao kufikisha umeme katika Kijiji cha Madeke, ili uwekezaji uweze kufanyika na vilevile nimefuatilia hata *REA* watafikia kijiji hicho.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Hongoli.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki kilinunuliwa kwa shilingi milioni 100 mwaka 2013 na mwaka huo huo Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu alifungua hiki kiwanda na tangu alipofungua mpaka leo hii hakijazalisha hata tani moja. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Bisahara na Uwekezaji atakaa na Mheshimiwa

Waziri wa Nishati, ili waweze kupeleka umeme haraka kwa kuwa, tatizo ni nishati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalii la pili pia ni lini sasa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ataongozana na mimi kwenda Madeke kujiona mwenyewe jinsi wananchi wale wanavyopoteza fedha nyingi/mabilioni ya fedha, kutokana na kukosa soko la kuuza haya mananasi na matunda mengine? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Hongoli kwa jitihada kubwa anayoifanya katika kufuatilia kiwanda hiki na tija kwa wakulima wa matunda ya eneo hilo, lakini vilevile nichukue nafasi hii ya pekee kabisa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa jitihada kubwa ambayo anaifanya katika kuhakikisha kwamba, umeme unapelekwa hasa katika maeneo ambayo tunatarajia kuwa na uzalishaji mkubwa na kuongea thamani katika matunda na eneo hili tayari tumeshafanya hayo mazungumzo.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba, ni rai yangu kwa wadau wengi kuona kwamba, umeme wa *REA* unaoombwaa katika vijiji kweli uwe na tija na hivi tufanye uzalishaji kwa sababu gharama za kupeleka umeme katika maeneo hayo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, suala la kuongozana hiyo itakuwa ni bahati ya pili kwa sababu, bahati ya kwanza tayari Mheshimiwa Waziri wangu mwezi huu ulioisha wa tatu alishaenda mpaka Njombe na amejionea hali halisi na vilevile tunategemea kujenga *shades* kwa ajili ya viwanda vidogo pale Njombe.

Kwa hiyo, mimi sina taabu nitaenda, nakubali kwenda huko. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Shamsia.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipatia nafasi, ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Tatizo lililopo Lupembe linafanana kabisa na tatizo lililopo Mtwara Mjini, viwanda vingi vimekufa ikiwemo Kiwanda cha Kubangulia Korosho cha Oram ambacho kilikuwa kinatoa ajira kwa wananchi wengi wa Mkoa wa Mtwara. Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua viwanda hivyo?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kupitia Sera yetu ya Uendelezaji wa Viwanda endelevu, sisi wenyeewe kama nchi tuliona kwamba, masuala yote yanayohusiana na uzalishaji yaondoke sasa kwenye mikono ya Serikali iende katika mikono ya sekta binafsi. Jambo ambalo tunafanya sisi ni kuhakikisha kuwa tunaweka mazingira wezeshi kwa kuhakikisha kuwa ile miundombinu inayohitajika pamoja na uunganishaji wa taarifa na vikwazo vyote ambavyo vinawakibili hao wawekezaji viweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa korosho, kwanza tunashukuru kwamba kwa sasa hali ya korosho/bei ya korosho imekuwa ni nzuri, lakini sisi kama Taifa tusingependa tu kuuza korosho zikiwa ghafi. Kwa misingi hiyo, tunaendelea kufanya jitihada ya kuhakikisha kuwa viwanda mbalimbali vya korosho vinaimarishwa ili kuhakikisha kuwa tunapata tija katika zao hili.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Joseph Mkundi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ukerewe ni wazalishaji wakubwa wa matunda hasa machungwa na nanasi. Lakini wananchi wa Ukerewe wamekuwa hawafaidiki sana na matunda haya kwa sababu sehemu kubwa ya matunda imekuwa ikiharibika kwa sababu ya kukosa soko.

Je, Serikali iko tayari kusaidia upatikanaji wa kiwanda cha kusindika matunda haya ili wananchi wa Ukerewe wapate soko la uhakika wa matunda yao?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba bado tunayo changamoto katika usindikaji wa matunda. Na katika mtazamo wetu Tanzania tunajipanga zaldi katika huu ukuzaji wa viwanda hasa katika eneo la kilimo na manasi pamoja na machungwa ni mazao mojawapo ambayo yana changamoto. Jambo ambalo tunaliona sasa hivi ni kwamba iko haja ya kuunganisha taasisi zetu hasa katika kukuza teknolojia zitakazowezesha matunda yanapokuwa yamezalishwa, yasiharibike kiurahisi na kuyaongezea thamani.

Lakini vilevile nikuombe Mheshimiwa Mbunge ukiwa ni sehemu ya uhamasishaji pamoja na Serikali kuendelea kuwahamasisha wadau binafsi kwa ajili ya kuwekeza viwanda katika eneo hilo.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swalii linalofuata tunaelekea Momba.

Na. 31

Serikali Kujenga - Momba

MHE. DAVID E. SILINDE aliuliza:-

Katika kutekeleza azma ya Tanzania ya viwanda.

Je, Halmashauri ya Momba inatarajiwa lini kujengewa kiwanda na cha aina gani?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa uchumi wa viwanda umeainishwa katika Mpango wa pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021). Lengo kuu la Mpango huo ni kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, jukumu la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ikijumuisha sera na mikakati rafiki kwa wawekezaji pamoja na miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi wakati shughuli za biashara na ujenzi wa viwanda zikiwa ni jukumu la sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hili Serikali imeendelea kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mikoa na Wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda ikiwemo Halmashauri ya Momba ambao wametenga ekari 252.87 kwa ajili ya viwanda. Lengo la mpango huo ni kuwa na maeneo ya kutosha kujenga viwanda sasa na baadaye. Kuelimisha wananchi juu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, kuvutia wawekezaji na kuboresha mazingira ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Momba na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) itaongeza juhudii ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje kujenga viwanda Wilayani Momba kutegemeana na fursa za uwekezaji zilizopo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa ya jumla kwa sababu swali nililouliza nilitaka njue kama Momba kitapatikana kiwanda, kitajengwa au hakitajengwa. Kwa hiyo, jibu ni kwamba wananchi wa Momba huko mnakonisikia hamna kiwanda kitakachojengwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaainisha kwamba jukumu la ujenzi wa viwanda ni la sekta binafsi, lakini kauli za Serikali na viongozi wa Serikali mitaani huko, kila siku *statement* ambazo wamekuwa wakizitoa ni kwamba Serikali inajenga viwanda. Ni kwa nini sasa Serikali isibadilishe kauli yake ikawaambia wananchi jukumu la kujenga viwanda sio la Serikali, Serikali kazi yake ni kuwezesha mazingira wezeshi kama ambavyo mmekuwa mkitamka hapa. Ninayasema haya kwa sababu tumekuwa tukisia hapa...

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio nataka niulize kabisa kwamba kwa nini sasa wasibadilishe hiyo kaulimbiu kwa sababu *mind set* ya wananchi ni kwamba Serikali inajenga viwanda wakati ukweli ni kwamba Serikali haijengi viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali imejinasibu hapa kwamba inaweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi pamoja na wafanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka njue jitihada za Serikali juu ya hawa watu wa sekta binafsi kwa sababu moja kumekuwa na malalamiko, mazingira wezeshi kwa mfano huko Momba barabara mbovu, maji hayapatikana, umeme unayumbayumba, mitaji hakuna, riba zimekuwa zinapitiliza.

MWENYEKITI: Umeeleweka Mheshimiwa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nijue jitihada za Serikali kukabiliana na changamoto hizi ili hii sera ya viwanda iweze kuwa inatekeleza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano si la kuamka na kufanya. Tunafuata Dira ya 2025, tunafuata Mpango wa Pili wa Miaka Mitano na tunafuata maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Imeandikwa katika Mpango wa Pili wa Miaka Mitano kwamba Serikali jukumu lake ni kuweka mazingira wezeshi na kazi ya sekta binafsi ni kujenga viwanda. Sasa sisi Tanzania sisi Serikali ya Awamu ya Tano tunajenga viwanda sisi sekta binafsi sisi ni Serikali tunakwenda pamoja huwezi kutenganisha sekta binafsi na Serikali. Huyo anatengeneza mazingira wezeshi huyu anajenga. Huyu anachota maji, huyu anasonga ugali wote mnapika chakula. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Silinde rafiki yangu usisahau umeme wa Momba kama si Serikali, kama sio mimi nikiwa Naibu wa Nishati usingefika. Tumefyeka msitu, sasa ushukuru kwa kidogo ulichopata nije nikupatie kingine.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Maryam Msabaha. Basi naona muda, haya Mheshimiwa Devotha Minja.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijinasibu kuwa ina mpango wa kujenga viwanda 100 kwa kila mkoa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa kujinasibu ni kufanya nini? Tumia lugha nzuri tu twende mbele.

MHE. DEVOTH A. M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikieleza kuwa ina mpango wa kujenga viwanda 100 kila mkoa na mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa ambayo ilikuwa na viwanda vingi tangu enzi za Mwalimu. Lakini hivi sana viwanda vingi vimekufa na vimegeuka kuwa ma-*godown*, mfano wa viwanda hivyo ni Kiwanda cha Komoa, Kiwanda cha *Tanzania Leather Shoes*, Kiwanda cha *CERAMIC*, Kiwanda cha *U-nuts*, sasa Serikali haioni kama kuna umuhimu wa kufufua viwanda vilivyokuwa ndipo ije na wazo la kujenga viwanda vipyta. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda Biashara na Uwekezaji majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza tunamshukuru kwa ufuatilajili. Ni kweli Serikali kiko *serious* kuona kwamba viwanda vingi vinajengwa Tanzania hasa katika kuongeza thamani mazao ya wananchi tulio nao jirani na viwanda hivyo kama ambavyo nimekuwa nikisistiza kila wakati viko katika ngazi za aina mbalimbali. Kuna viwanda vidogo sana, viwanda vidogo, viwanda vyatia na viwanda vikubwa. Kwa hiyo, wananchi wenye mitaji midogo wanao uwezo pia wa kuanzisha viwanda kulingana na hali inayowezekana.

Sasa suala la viwanda vyatia zamani ambavyo havifanyi kazi, kwanza tufahamu kwamba kiwanda kina tabia sawa sawa na binadamu. Kiwanda kinapokosa mazingira mazuri na wezeshi kinaweza kufa sawa na binadamu anavyokufa. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sasa hivi kuhakikisha kuwa tunajenga mazingira wezeshi ikiwemo kupunguza au kuondoa kabisa vifo vyatia viwanda na hiyo ndiyo kauli mbiu na hiyo ndiyo jitihada inayofanyika ndiyo maana unakuta jitihada mbalimbali zinaendelea.

Kwa hiyo, Morogoro ni sehemu mojawapo ambayo tayari tumeshaitembelea na hivyo viwanda ambavyo unasema vimekuwa havifanyi kazi vizuri kama *Leather Industries* tayari tuko katika mchakato wa kuhakikisha

kwamba makongano mbalimbali ya *leather* yanafanyika ili kuhakikisha viwanda hivyo vinakuwa vizuri na kuleta tija kwa Taifa. Na nizidi kuwaomba watanzania wengi msitishike, nimetembelea viwanda. Zaidi ya viwanda nilivyotembelea asilimia 90 vingi vinaendeshwa na sisi Watanzania wenyewe. Kwa hiyo, tujitoe hata sisi Wabunge tuanzishe viwanda kadiri inavyowezekana kulingana na mahitaji ya maeneo yetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rehema Magilla.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora ni miongoni mwa mikoa inayoongoza katika uzalishaji wa maembe. Mpaka jina la Unyanyembe likapatikana ni kutokana na uzalishaji wa hizo embe, lakini cha ajabu mkoa huo wa Tabora mpaka leo hauna kiwanda cha usindikaji wa maembe, hali inayopelekea maembe yanazagaa kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niulize Serikali ni kwanini haitaki kujenga Kiwanda cha Usindikaji wa Maembe Tabora?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nirejee tena nazidi kuhamasisha Watanzania pamoja na Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwahamasisha wawekezaji katika maeneo hayo. Kwa mfano hapa Dodoma kuna Kiwanda kizuri cha Matobolo wanasantika maembewanakausha na maembe hayo yanaweza kutumika kwa muda mrefu. Kwa hiyo, sisi tuisubiri kiwanda kije chenyewe ni lazima tuwahamasisha wadau mbalimbali hata sisi wenyewe tuweze kuwekeza ili kuhakikisha kuwa maembeyo yanakaa muda mrefu.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini.

Na. 32

Barabara ya Singida-Haydom

MHE. JUSTIN J. MONKO aliuliza:-

Barabara ya Singida - Ilongero - Mintiko hadi Haydom inayounganisha Mikoa ya Singida na Manyara ni kiungo muhimu katika kusafirisha mazao ya wakulima na bidhaa za wafanyabiashara na inapita katika Hospitali ya Rufaa ya Haydom ambayo wananchi hufuata huduma kwa kukosa Hospitali ya Serikali katika Halmashauri.

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami ili kunusuru maisha ya wananchi wa Singida Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Singida – Ilongero – Mtinko - Nkugi na Kidarafa hadi Haydom ni barabara ya mkoa yenye urefu wa kilometra 93.4 ambapo kilometra 84.36 zipo mkoani Singida na kilometra 9.04 zipo katika mkoa wa Manyara. Barabara hii inahudumiwa na Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii kwa wananchi wa Mikoa ya Singida na Manyara kwa ajili ya usafirishaji wa abiria, mazao, bidhaa za biashara na pia wananchi wanaokwenda kupata huduma ya matibabu katika hospitali ya Haydom. Hivyo kwa

umuhimu huo Serikali imekuwa ikiifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 barabara hii ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 2.246 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali. Aidha, Serikali imejenga jumla ya kilometra 8 kwa awamu kwa kiwango cha lami kuanzia Singida Mjini kuelekea Ilongero na jumla ya kilometra tano za barabara hii zimepangwa kujengwa kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni kuunganisha kwa barabara za kiwango cha lami makao makuu ya mikoa na nchi jirani na baadae barabara za mikoa zitafuata.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi pamoja na majibu ya kukatisha tamaa ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba barabara hii ni muhimu sana katika eneo hili na ametueleza kwamba katika bajeti ya mwaka 2018/2019 wametenga kujenga kilometra tano tu katika barabara ambayo anasema ina urefu wa zaidi ya kilometra tisini na kitu.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kuendelea kutenga kilometra tano zitawafanya wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini na Mkoa wa Singida na Manyara kusubiri ujenzi huu kwa zaidi ya miaka 19 ijayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imekuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na ipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi na imetusumbua sana wakati wa uchaguzi kila mara.

Je, Serikali sasa ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kilometra 15 zilizosalia katika kufika katika mji wa Ilongero ili kusudi kuwaondolea walau kuwapunguzia wananchi adha hii wanayoipata kwa sasa? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Engineer Nditiye*.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara au ujenzi wowote ule unahitaji kupata pesa ya kutosha. Ninamwomba tu Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba nchi yetu ni kubwa na kila sehemu inahitaji ipate huduma kutokana na mfuko na kipato cha Serikali kilichopo na sio kwamba tuna-*concentrate* na barabara moja tu. Tunakiri kwamba kweli barabara ile ni muhimu lakini Tanzania ni kubwa na yote inahitaji pesa kutoka Wizara hiyo hiyo moja.

Kwa hiyo, nimuhidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kupata kilometra tano ni mwanzo, lakini pesa itakapopatikana tunaweza tukajenga hata kilometra nydingi lakini angalau hizo tano zilizopatikana ni muhimu azipokee na ashukuru kwamba tunafanya jitihada kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto za barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la pili, ni kweli barabara hii ipo kwenye ahadi na hata kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi barabara hii inasomeka, lakini siyo hiyo tu peke yake ni barabara ambayo inatoka kuanzia Karatu ambayo ipo Arusha, inapitia Mbulu inakuja mpaka hapo tunapopazungumza Haydom inakwenda mpaka Simiyu. Pesa zitakapopatikana na tukumbuke kwamba tuna ahadi mpaka mwaka 2020, pesa itakapopatikana hizi barabara zote zitajengwa kwa kiwango cha lami. Tuna nia nzuri kama Serikali kuhakikisha kwamba Wananchi wanapata huduma nzuri za barabara.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa ni nchi kubwa hii jamani. Hebu nianze kwa muda tulionao. Mheshimiwa Mwakibete, Mheshimiwa Ngonyani *Engineer Edwin*, Mheshimiwa Masala maana ndio mnafananafanana na Mheshimiwa Hawa Ghasia. Hebu tuone hali ya barabara nadhani kwa sababu ya muda haya Mheshimiwa Nsanzugwanko. Naenda kwa namna hiyo nilivyowataja ndivyo hivyo. Tunaanza. Mheshimiwa Mwakibete.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, wananchi wa Busekelo kwa kushirikiana na mimi nikiwa Mbunge wao tumeamua kulima barabara inayounganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa Mbeya kwa kutumia zana za jembe la mkono.

Je, ni lini Serikali itatupa *support* ili tuweze kukamilisha barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Busekelo na Makete na ukizingatia kwamba...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri. Lini mnawapa *support* wananchi hao.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana kwa jinsi anavyopigania wananchi wa jimbo la Busokelo katika kuhakikisha kwamba wanapata huduma nzuri za barabara. Ni kweli nakiri kwamba nilimwona juzi kwenye vyombo vya habari akihamasisha na kufanya kazi sambamba na wananchi kuhakikisha kwamba barabara inapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii imo kwenye llani, Serikali inalitambua na tumeona jitihada za Mbunge na kwenye bajeti yetu ya mwaka huu imesomeka kwenye hatua za upembuzi yakinifu na *details design*. Kwa hiyo, tutalishughulia.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Edwin Ngonyani.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa. Na mimi nilitaka niulize kuhusu barabara ya kutoka Mtwara – Pachani - Mkongo – Gulioni – Ligera - Lusewa inaenda Magazine - Likusenguse hadi Tunduru ambayo ina urefu wa kilometra 300 iliyoahidiwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Awamu ya Nne, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kipande hicho cha barabara kimekuwa kikisumbua kwa muda mrefu na kwa kweli tumekuwa tukipata mawasiliano mazuri sana na Mbunge akiwa anatetea kipande hicho cha barabara. Ninamhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo suala tunalo na tunalifanyia kazi; tunawasiliana mara kwa mara na Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa kuhakikisha kwamba inaingizwa kwenye utaratibu ambapo tutaanza kuifanyia matengenezo makubwa. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masala.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nichukue nafasi hii kumwuliza swali dogo Mheshimiwa Naibu Waziri; ni nini kauli ya Serikali juu ya kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Masasi - Nachingwea - Nanganga?

MWENYEKITI: Ahsante. Swali fupi na jibu fupi sasa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba pesa inatafutwa, kwa sababu hatua za awali za ujenzi wa kipande hicho cha barabara zilishaandaliwa na zinatekelezwa. Pesa

itakapopatikana, barabara hiyo itaingizwa kwenye mpango ianze kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Alex Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ya mwezi Desemba, 2017 kuhusu barabara ya Nyakahura - Murugarama ilieleza kwamba iko kwenye hatua ya mchakato wa manunuzi, ni lini sasa mchakato huo wa manunuzi utakamilika ili barabara hii yenye urefu wa kilometra 85 iweze kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami? (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu. Ni lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kumpata mkandarasi shughuli za ujenzi wa kipande hicho cha barabara zitaanza mara moja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSWAZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo tu; barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi, ni barabara ya muda mrefu sana; na kipande cha Kidahwe – Kasulu kina mkandarasi, lakini mkandarasi huyo amekuwa kazini kwa miaka kumi akijenga kilometra 50. Swali langu kwa Waziri ni kwamba ni kwa nini mkandarasi huyu halipwi madeni yake ili barabara hiyo ikamilike? Kwa nini barabara ya kilometra 50/0 aijenge kwa miaka 10 wakati hana fedha? Barabara hii mkandarasi yupo kwenye *site*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kipande cha kutoka Kidahwe kuja mpaka Kasulu kina mkandarasi. Nimhakikishie Mheshimiwa Nsanzugwanko kwamba mkandarasi huyo ameshalipwa malipo yake, lakini sasa hivi kuna mvua nyngi sana zinaendelea pale Mkoani Kigoma, tena mkoa mzima na hivyo kusababisha ucheleweshaji kidogo wa kumalizia. Kuna hatua za awali ambazo zimeshaendelea na ye ye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge anajua, kipande cha kilometra karibu 20 kitawekwa lami mara mvua zitakapopungua. Kwa sababu mambo mengine ni ya kitaalam, huwezi kuweka lami wakati kuna mvua inanyesha kila siku. Mvua za Mkoa wa Kigoma bahati nzuri anazifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipande cha kutoka Kibondo mpaka Nyakanazi kupitia Kakonko na kutoka Kasulu, *tender itatangazwa* hivi punde. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa, tunaendelea. Swalii letu la mwisho kwa siku ya leo lina...

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja, naona umenisahau.

MWENYEKITI: Nilikutaja wewe Haonga?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Ndiyo!

MWENYEKITI: Nakupa nafasi.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Mbozi na Wilaya ya Songwe hazijaunganishwa kwa barabara licha ya kwamba Wilaya ya Mbozi ni Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe, lakini wananchi wa kutoka Wilaya ya Songwe kwenda Makao Makuu ya Mkoa ambayo yako Mbozi wanalaazimika kupita mkoa mwингine ambao ni Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize sasa, ni lini barabara ya kutoka Kata ya Magamba ambayo inapitia Kata ya Magamba Wilaya ya Mbozi; na hili niliweke vizuri, Magamba hiyo inapatikana Songwe, lakini Magamba nyingine pia inapatikana Mbozi. Kuna uwezekano wa kutengeneza njia kwenda Makao Makuu ya Mkoa kutoka Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini barabara hii itatengenezwa licha ya kwamba Naibu Waziri wa Ujenzi alisema kwamba angeweza kuja Mbozi kuangalia uwezekano na hadi sasa amewadanganya wananchi wa Mbozi, hajafika. Naomba sasa jibu la Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa umeelewaka. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana. Barabara hii na mimi naifahamu sana na wewe unaifahamu sana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaunga mkono kabisa mambo ambayo yanaendelea hapa Bungeni, kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge katika kuuliza maswali. Nadhani wakati mwingine ni vizuri tuwe tunawasiliana kimkoia kwanza kujua *status* ya mambo ambayo tunakuja kuyafuliza huku Bungeni. Siyo kitu kibaya wananchi wakifahamu kwamba umekuja kuuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kuna taratibu za ujenzi wa barabara ambazo zinaendelea kuititia *TANROADS* Mkoa wa Songwe. Ninaamini kama Mbunge angewasiliana na Meneja wa *TANROADS* Mkoa, asingekuja kuuliza swali kama alilouliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Haonga kwamba *detailed design* tayari, sasa hivi tunafanya utaratibu baada ya kuititia hizo *details* kuanza kutafuta Mkandarasi wa kujenga hicho kipande cha barabara kutoka Mbozi kwenda Songwe. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali letu la mwisho kwa siku ya leo, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 33

Kukarabati Uwanja wa Ndege wa Songea

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano imeusaidia sana Mji wa Songea kwa kuleta ndege za Bombadier ambazo zinatoa huduma zake katika Uwanja wa Ndege wa Songea.

(a) Je, kwa nini uwanja huo hauongezwi urefu na kufanyiwa ukarabati ili kutoa huduma zaidi na kuruhusu ndege ziweze kutua kwa saa 24?

(b) Je, kwa nini Serikali haiweki mashine za ukaguzi wa abiria (*scanning machine*) ili kuondoa adha kwa abiria kukaguliwa mizigo yao kwa kupekuliwa ambapo inadhallilisha na kupoteza muda?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Songea ni mionganoni mwa viwanja 11 nchini viliviyofanyiwa upembizi yakinifu na usanifu wa kina kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Transport Sector Support Project*. Usanifu huu ulikamilika mwezi Juni, 2017 na ulihusisha usanifu wa miundombinu ya viwanja hivi kwa ajili ya upanuzi na ukarabati ili kukidhi mahitaji ya viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Wizara yangu, kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*), inaendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi pamoja na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi za awamu ya kwanza za upanuzi na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Songea, ambazo zitahusisha ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara za viungio, maegesho ya ndege, kusimika taa pamoja na mitambo ya kuongozea ndege, hivyo kuruhusu ndege kuruka na kutua kwa saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*), imenunua mashine za ukaguzi wa abiria na mizigo kwa ajili ya viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na Songea na tayari mashine hizo zimepelekwa katika viwanja husika, kikiwemo kiwanja cha ndege cha Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mafundi wanaendelea na zoezi la kufunga mashine hizo ambapo tunatarajia ifikapo katikati ya mwezi huu wa Aprili, 2018, kazi ya kufunga mashine hizo itakuwa imekamilika na hivyo mashine hizo kuanza kutumika katika viwanja hivyo, kikiwemo Kiwanja cha Songea.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa muuliza swali, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Napenda kumuuliza swali la nyongeza kwamba wakati utaratibu wa kumpata Mkandarasi wa kutengeneza uwanja huo unaendelea, kwa nini huduma ya ndege isiendelee? Maana yake hivi sasa huduma ya ndege imesitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa nini huduma za ndege katika Uwanja wa Songea ambazo zinawasaidia wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Njombe zisiendelee wakati Mkandarasi anaendelea kutafutwa? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumesimamisha kwa muda huduma za usafiri wa ndege katika kiwanja hicho ili kupisha marekebisho yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kuongeza tabaka la lami, kwa sababu sasa hivi ndege ikitua na kuondoka inapeperusha changarawe ambapo tuna wasiwasi zinaweza zikaingia kwenye *propeller* zikahatarisha usalama wa abiria, lakini na ndege vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafanya ukarabati wa uwanja kwa kuondoa mashimo ambayo yako kwenye uwanja ule ili tuepushe ajali. Hata hivyo, tunahakikisha kwamba huduma zitarudi hivi karibuni baada ya kuwasiliana na TAA kwamba wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba hizo changamoto zilizoko katika uwanja huo zinarekebishwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa leo ndiyo tumeishia hapo kwa upande wa maswali. Tumekula sana muda wetu lakini nimejaribu kuwavumilia kwa sababu ya maslahi mapana ya nchi yetu. (*Makofii*)

Wageni tulionao Bungeni asubuhi hii; wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika tunao wageni saba ambaao ni Wabunge, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambaao ni Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na ni Wajumbe wa Kamati Ndogo ya Tume ya Bunge hilo, wamekuja hapa Bungeni kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na Tume ya Utumishi wa Bunge.

Tunao hapa Mheshimiwa Susan Nakawuki Nsambu ambaye ni Mwenyekiti wa Tume, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Anne Itto Leonardo, Mjumbe wa Tume; Mheshimiwa Leontine Nzenyimana, Mjumbe wa Tume; Mheshimiwa Fred Mukasa

Mbidde, Mjumbe wa Tume na Mheshimiwa Aden Omar Abdi Kadir, Mjumbe wa Tume. Wameambatana na watumishi wawili wa Bunge hilo. Karibuni sana Waheshimiwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano. (*Makofii*)

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kutoka Jumuia ya Umoja wa Ulaya katika Divisheni inayohusika na masuala ya Udhibiti wa Dawa za Kulevyia (*The European Union Action Against Drugs and Organized Crime*) ambao ni *Mr. Charles Stuart - Deputy Head of the EU Delegation*; tunaye *Mr. Thomas Carter, Team Leader European Union Against Drugs*; tunaye *Francesco Lo Lacono, Regional Coordinator for Tanzania*; na tuna *Maria Gaston, Mjumbe wa Delegation*. You are most welcome to the National Assembly of Tanzania. (*Makofii*)

Wageni wengine ni Makamishna wawili kutoka Mamlaka ya Kuzua na Kupambana na Dawa za Kulevyia nchini, tunaye Kamishna Jenerali mwenyewe wa Mamlaka hiyo Ndugu Rogers Sianga na tunaye Dkt. Cassian Nyandindi, Kamishna Msaidizi wa Mamlaka hiyo. Karibuni sana, tunatambua kazi yenu nzuri na ngumu mnayofanya, lakini kwa kipindi hiki ninyi ndio mmeaminiwa na Taifa hili myafanye hayo magumu kwa niaba ya Watanzania. Karibuni sana, tunatambua kazi hiyo mnayoifanya. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaye ni mtoto wake, huyu ni mjukuu wangu Semindu Abdallah Ulega. (*Makofii*)

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wauguzi kutoka Mkoa wa Mbeya. Wako wapi? Nadhani wako mahali pengine tutawaona baadae.

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, ambao ni familia yake

wakiongozwa na mke wake Ndugu Florah Ndumbaro. Shemeji yetu, karibu sana. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni Ndugu Abeid Marcus Luhwago, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kitwiru, Iringa. Karibu sana Mwenyekiti. (*Makofi*)

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Grace Kiwelu, ambaao ni watoto wake kutoka Mkoani Dar es Salaam, mko wapi? Aah, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Lucy Magereli, Mbunge ambaao ni watoto wake kutoka Wilaya ya Kigamboni Mkoani Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo ambaao ni watoto, vijana na watu wenye ulemavu kutoka Taasisi ya *Hope Deliveryya* Mkoani Dodoma, wameambatana na Mheshimiwa Kemnalth Vindo, Diwani wa Kata ya Buigiri, Wilayani Chamwino. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Agness Mathew Marwa ambaao ni watoto wake wakiongozwa na Ndugu William Faraja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, ambaao ni ndugu zake. Karibuni sana. (*Makofi*)

Hayo ndiyo matangazo tuliyonayo hapa mezani kwa siku ya leo.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Tunaendelea.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mwongozo wa Spika

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mwongozo wa Mwenyekiti

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, mna haraka ya nini? Tunaanza. Nani anasema? Upande wa huku.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mlinga.

MWENYEKITI: Mlinga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Haonga.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: *Call me J. Kitwanga.*

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Sophia.

MWENYEKITI: Waheshimiwa nimemaliza huku, msiseme naonea. Nahama Mheshimiwa Kitwanga, Mheshimiwa Gekul.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Halafu Sophia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Sophia Mwakagenda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Maftaha Nachuma. Mimi mwenyewe siruhusiwi kujuliza mwongozo eeh! Tuanze na Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kwa Kanuni ya 68(7) kwa sababu ya muda naomba nisiaisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano anajibu swali langu, alisema kwamba Mbunge angewasiliana na Meneja wa *TANROADS*, Mkoa wa Songwe, asingeuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limenisikitisha sana, maana yake inaonekana kwamba Waheshimiwa Wabunge hapa sasa hatuna kazi, kwa sababu tumekuja hapa kuwakilisha wananchi wetu kwenye Majimbo yetu, tafsiri yake ni kwamba kama ningekuwa na shida ya maji Jimboni kwangu nisingemuuliza Waziri wa Maji, ningewasiliana na Mhandisi wa Maji; kama ningekuwa na shida labda ya kilimo, ningewasiliana labda na Afisa Kilimo. Sasa dhana ya uwakilishi hapa Bungeni haionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kama inaruhusiwa kwa Mheshimiwa Waziri kujibu swali hili ambalo nimejibowi kwa kebehi namna hiyo na kuniletea usumbufu kwa wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kama inaruhusiwa au hairuhusiwi, lakini binafsi nione tu kwamba amejibu kwa kebehi na anaona kazi hii kwa sababu Waziri Mkuu yupo hapa, akiwezekana mtafutieni kazi nyingine kwa sababu ameleta usumbufu mkubwa sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nachuma.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nasimama kwa kanuni hiyo hiyo ya 68(7). Nilikuwa naomba mwongozo wako, kwa sababu tunaendelea, nimeangalia kwenye ratiba hapa, majadiliano ya Ofisi ya Waziri Mkuu yanaendelea, naomba mwongozo wako, suala ambalo nimeweza kulizungumza mapema asubuhi jana, kwamba tarehe 25 Machi, Mtwara Mjini kijana anayeitwa Abdillah Abdulrahman alipigwa risasi na Jeshi la Polisi akiwa anaokota *sea shells*, wale kumbwa pale baharini ili aweze kufanya kitoweo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kauli ya Serikali kwa sababu nimezungumza hili suala zaidi ya mara mbili, bado sijapata kauli ya Serikali. Nilikuwa naomba mwongozo wako kwamba Serikali inatoa kauli gani juu ya kuunda Kamati Maalum ya kufanya uchunguzi juu ya kifo cha huyu kijana pale Mtwara Mjini? Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7), naomba kwa sababu ya muda nisilisome. Wakati Waziri, Mheshimiwa Kandege akijibu swali langu Na. 24, alisema hajapata malalamiko kutoka kwa Mbunge wa Jimbo. Ninavyofahamu, Ubunge wa Viti Maalum ni *sign* ambayo Taifa iliingia kuwa na upendeleo kwa wanawake/kuwakilisha wanawake katika vyombo vyaa maamuzi likiwemo Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kama Mbunge halali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nikiwatetea wanawake wa Mkoa wa Mbeya na Watanzania kwa ujumla wake. Swali nilioliliza Na. 24 ni kwa manufaa ya Watanzania wa Mkoa wa Mbeya hususan Ipinda na Ikuti. Kwa kuniambia mimi Sophia sikustahili kuuliza hilo swali kwa sababu Mbunge wa Jimbo hajaleta malalamiko, naomba mwongozo wako. Je ni halali? Hyo ni moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbili...

MWENYEKITI: Mwongozo mmoja tu bwana!

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni moja? Haya basi, naomba nijibewe swali langu haraka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Na mimi naomba mwongozo wako kwa kanuni ile ile ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limejitokeza wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Mavunde akijibu maswali, hususan Na. 28 la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu kuhusu posho za Wazee wa Mahakama. Alisema kwamba Serikali itafikiria pale ambapo fedha zitapatikana, wazee hawa walipwe fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanapouliza maswali, tunategemea jibu ambalo linatolewa kwa Mbunge aliyeuliza swali ni jibu ambalo linamgusa kila

mmoja wetu na aridhike na majibu hayo. Hili la wazee wa Mahakama, majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ni majibu ambayo hatujaridhika; au binafsi sijaridhika. Kwa sababu haiwezekani mzee analipwa shilingi 5,000 kwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni la Tanzania nzima, siyo tu kwa mwuliza swalii. Hata kwangu Babati Wazee wa Mahakama wamekuwa wakihangaika usiku na mchana. Kwanza hawajui wanapataje fedha zao, lakini pia hata hicho kidogo wamelimbikiziwa wana *arrears* za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, ni kwa nini Serikali isiwe inajipanga kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge hususan kwa masuala yanayogusa maisha ya wananchi wetu?

Naomba Mwongozo wako kwa nini Serikali au Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara inayohusika wasije na majibu ya kina kuhusu Wazee wa Mahakama, lini watalipwa *arrears* zao? Lini wataboreshewa hizi shilingi 5,000 angalau walipwe fedha ambazo zinalelewaka? Wamekuwa wakijitolea na wao pia wamechoka. Naomba Mwongozo wako. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwongozo wangu nilikuwa nataka kupata kauli ya Serikali kuhusu *justification* ya nembo ya Taifa ambayo tunaitumia katika Taifa la nchi yetu. Nembo hiyo siyo tu ya Taifa, ipo kwenye kiti ambacho unakalia wewe na ipo katika Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba kila Taifa lina nembo ya Taifa ambayo ina-*reflect* mazingira halisi ya nchi na watu wake. Nembo yetu ya Taifa ina Bendera ya Taifa, ina Mlima Kilimanjaro, inaonesha bahari, ina pembe za ndovu na ina shoka na jembe. *Justification* ambayo nilikuwa naiomba ni bibi na bwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nembo yetu ya Taifa ina bwana ambaye amevaa lubega, sawa; lakini pia ina bibi ambaye amevaa wigi. Kama siyo wigi, ni Mzungu ama Mwarabu ambaye hai-*justify* mazingira halisi ya Taifa letu la Tanzania. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba, aidha, Serikali ifanyie marekebisho nembo hiyo na izuie isitumike mpaka itakapofanyiwa marekebisho. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Charles Kitwanga.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kanuni hiyo hiyo 68(7) kujaribu kuuliza, ni kwa nini Bunge lisione umuhimu wa kuwa na vitambulisho vya namna hii ambavyo ndani yake kuna *embedded chip* au viwe na *attached chip* kama hii hapa ambayo ina uwezo hata *camera* zetu, mtu akiwa mbali ukiwa umeivaa hivi, *camera* inaweza ikakutambua huyu ni fulani. Maana hivi vitambulisho kwanza vina kamba ambazo nina wasiwasi watani zangu kama Mheshimiwa Lukuvi na Wahehe wengine hawa wawili, wanawenza wakajinyonga nazo. (*Makofi/ Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Waheshimiwa ambao walismama kuomba mwongozo huo. Nitawajibu kwa mtiririko huo huo nilivyowataja, nikianza na Mheshimiwa Pascal Haonga.

Mheshimiwa Haonga ye ye anaona majibu aliyopewa na Serikali kupitia Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwamba kidogo yana ukakasi kwake. Je, majibu hayo yanaruhusiwa kikanuni? Maana Kanuni ya 68(7) ya mwongozo Waheshimiwa Wabunge mnaifahamu.

Sasa unaponiomba niseme inakubalika au la, kwa mujibu wa kanuni na taratibu zetu za Bunge, mimi lazima njielekeze huko.

Umeuliza swalii la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri kakujibu. Yawezekana wewe hukuridhika na majibu hayo, labda na *tone* aliyotumia, lakini hiyo haiondoi ukweli wa maelezo au majibu yaliyotolewa na Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, mfahamu, mara nyingi maswali ya msingi, ndiyo maana Serikali inaenda, inapewa muda ikajiandae kuja kuwajibu, tena kwa ufasaha. Ndiyo maana kanuni zinasema kama mwenye swalii la msingi hakuridhika na jibu la Serikali kwa swalii lake, maana lazima yajibiiwe kikamilifu na ataaeleza kwa nini halikujibiiwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, ukiuliza swalii la nyongeza, maana mara nyingi tuna-*assume* kwamba Waziri kipindi hicho anajua nchi nzima, anaweza mara moja akakujibu uweze kuridhika. Mara nyingi ukija na *gear* ya namna hiyo, Serikali watakujibu kwa kadri wanavyoweza. Wapo baadhi ya Mawaziri wana uwezo, wanajua Wizara zao mpaka barabara zetu za mikoa nchi nzima, lakini nadhani hatuwezi kuwa tunawatendea haki kwa namna hiyo.

Mbunge kama tunavyotakiwa kufanya kazi zetu, wewe unakuwa na *data* ya kutosha. Ndiyo maana *angle* aliyokusaidia Mheshimiwa Naibu Waziri, ukiwa na *data* ile kutoka kwenye eneo lako unakotoka, kwa sababu unazo, akikujibu visivyo, pale pale unarejesha kwamba angalia taarifa nilizonazo kwa mkoa wangu kwa barabara husika ni hizi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa hilo nasema mwongozo wangu ni kwamba inaruhusiwa. Majibu hayo aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kikanuni yanaruhusiwa; na kwa sababu ya msingi wake kwamba mwenye swalii la msingi hajalalamika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Nachuma, tukio la tarehe 25 Machi, unadai kijana alipigwa risasi. Sasa katika mazingira yapi? Mimi narudi kwenye kanuni. Jambo lililotokea mapema; na mapema tumesema, mapema siku hiyo. Msiniondoe kwenye kanuni. Kwa vile ni swalii linalohusu uhai wa Mtanzania, katika

mazingira ambayo nadhani vyombo husika vinafanya, watapata nafasi ya kulitolea maelezo kwa wakati watakaoona unafaa. Huo ndiyo mwongozo wangu kwa upande wa tukio la tarehe 25 mwezi wa Tatu mwaka huu, 2018 kule Mtwara, lakini halijatokea leo.

Mheshimiwa Mwakagenda, alikuwa na swali lake la msingi ameuliza, lakini amesema majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ameeleza kwamba Mbunge wa Jimbo la Kyela, maana ninavyofahamu Ipinda na Ikuti ni Kyela! Unaanza Rungwe si ndiyo! Unakuja Ipinda. Mbunge wa Jimbo hilo hakulalamika. Nadhani ndiyo maneno ambayo yamemletea ukakasi Mheshimiwa. Wewe ndio, ni Mbunge wa Viti Maalum, hakuna Mbunge wa Mkoa.

Niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hatuna Wabunge wa Mkoa. Ndiyo maana mnaitwa Wabunge wa Viti Maalum. Mmetokea wapi? Ni utaratibu ambao umewekwa kupata idadi ya uwakilishi mzuri ya wanawake humu Bungeni, lakini hakuna Mbunge wa Mkoa. Narudia ili ikae vizuri kwenye *Hansard*, hakuna Mbunge wa Mkoa. (*Makofi*)

Mikoa na Wilaya zetu ndiyo zimegawanya katika Majimbo ya Uchaguzi. Viti Maalum ni dirisha la kuingilia kwa kundi maalum katika Taifa hili, wakitokea eneo linalohusika. Anakotokea yeye, anajua anakotokea. Hiyo haikatazi, maana *angle* ilikuwa ni hiyo kwamba Mbunge wa Jimbo hajalalamika kwa kazi inayofanyika kwenye ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo hayo mawili. Huo ndiyo ukweli. Mheshimiwa Waziri amesema, *data* ndizo hizo. Sasa yawezekana wewe ungeisaidia Serikali kwa kuelezea upungufu ambao umeuona ulipoenda kutembelea eneo husika. Maadam hujafanya hivyo, mimi siwezi kukusaidia kwa hilo.

Mheshimiwa Gekul, swali namba 28 kuhusu posho za wazee. Mheshimiwa Gekul nakurudisha kwa mwongozo wangu ambao nimeanza nao. Wewe yawezekana hukuridhika na majibu yaliyotolewa na Serikali, lakini wewe

hukuwa umeuliza swalii la msingi. Mheshimiwa Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, ndio alikuwa na swalii hilo ninavyokumbuka mimi, kajibila na Serikali, karidhika. Wewe huwezi uka-*demand*sasa maelezo kupitia swalii la nyongeza ambalo majibu hukuridhika nayo. Huo ndiyo mwongozo ambao tumeuweka siku zote tuufahamu.

Mheshimiwa Mlinga, hilo tukio limetokea leo?
(*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nembo hii ya Taifa iko hapa kwa mujibu wa sheria za nchi. Yawezekana ukawa na mawazo mazuri kama alivyosema yeye, lakini njia nzuri ya Kibunge, unaweza ukachokoza swalii uone, je, kuna umuhimu wa kuifanyia marekebisho sheria hiyo?

Kwa sasa hivi, kwa kiapo chetu cha Ubunge, kinatutaka tuheshimu Katiba na sheria za nchi. Mojawapo ni sheria inayosimamia nembo yetu ya Taifa. Huo ndiyo mwongozo wangu. Kwa hilo, tuheshimu sheria inayosimamia nembo hiyo.

La mwisho, Mheshimiwa Charles Kitwanga, unaweza ukasema limetokea leo, nami navaa kile kitambulisho, tunatakiwa wote tuvae. Yeye ametoa ushauri kwamba twende na wakati, twende na teknolojia.

Hili nalichukua, maana tulianza nalo kwenye *briefing* juzi nakumbuka, nililisikia vizuri sana. Kwa hiyo, nalichukua nilifikishe kwa Katibu wa Bunge, kama Mtendaji Mkuu wa Bunge letu. Wao walichukue walione katika upana wake ili tupate kitambulisho cha Kibunge kinachoendana na hadhi ya Mbunge. Nadhani hoja ndiyo hiyo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, huo ndiyo mwongozo wangu kwa maeneo niliyoombwa na Waheshimiwa Wabunge.

Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu
kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tuna orodha za pande zetu zote kwa siku ya leo. Tutajitahidi kwa kadri muda utakavyoturuhusu, hizo dakika kumi mnazo kila Mbunge lakini haiwazuii kuititia vyama vyenu mkaelewana mkagawana tano tano ili muwe wengi zaidi.

Lakini naanza, Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe mchangiaji katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai; pili, kwa dhati ya moyo wangu kabisa namshukuru sana Rais wetu wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kuleta maendeleo katika Taifa letu hili la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kazi kubwa anayoifanya na ambayo inaonekana dhahiri ya kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo inabidi nichangie ni eneo la afya. Kwanza kabisa naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano, kwa taarifa sahihi zilizopo ni

kwamba Halmashauri yangu ya *Nzega DC* ni mojawapo ya Halmashauri 67 ambazo zimepewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kujenga hospitali mpya. Napongeza sana hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ni matumaini yangu, kama ambavyo tumeelezwa kwamba fedha hizi zinakuja na ramani maalum kutoka Wizarani; na kwamba kwa kuzingatia matumizi ya *force account* katika ujenzi wa miradi sasa hivi, ni matumaini yangu kwamba shilingi 1,500,000,000 zitatosha kabisa kujenga hospitali hii mpya kwa kutumia *force account* na ramani maalum ambayo imekuwa *tested kwenye ngazi* ya Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo liko dhahiri ambalo ni lazima nongoose ni hali ya upatikanaji wa dawa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya. Tunafahamu kwamba Kitaifa Serikali ya Awamu ya Tano imeongeza bajeti ya dawa kutoka bajeti iliyokuwa awali, mwaka 2015 ambayo ilikuwa *around* shilingi bilioni 31 kwa mwaka, imeongezwa mpaka shilingi bilioni 269 kwa mwaka. Hili ni ongezeko kubwa sana na kwa Halmashauri yangu ya *Nzega DC* pekee ongezeko hilo limetoka shilingi milioni 300 kwa mwaka 2015 mpaka shilingi milioni 700 mwaka huu. Hili ni ongezeko la zaidi ya asilimia 100 na ushee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jambo ambalo liko dhahiri sana na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene na Halmashauri ya *Nzega DC* kwa ujumla, ninapongeza kwa dhati, kwa sababu hali ya upatikanaji wa dawa kwa kweli *ime-improve*, imeongezeka kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo sasa inabidi lifanyike na huu ni ushauri wangu, baada ya kuhakikisha sasa tunapata dawa za kutosha kwa kuwa na bajeti ya kutosha, jambo kubwa ambalo inabidi lifanyike sasa ni *ku-address* tatizo la uhaba mkubwa wa waganga na madaktari katika vituo vyetu vya afya, hili bado ni tatizo. Mimi katika kituo changu cha afya cha Itobo na Bukene ambavyo ni vituo ambavyo vimejengwa kwa hadhi ya kisasa, vina vifaa vizuri

vya kufanya upasuaji, lakini katika vituo vyote hivi viwili mganga anayeweza kufanya upasuaji ni mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Itobo kuna mganga mmoja tu anayeweza kufanya upasuaji na hata Kituo cha Afya cha Bukene pia kina mganga mmoja tu anayeweza kufanya upasuaji. Sasa kutokana na *workload*, idadi ya wagonjwa wanaokuja kupata huduma pale, huyu mganga mmoja kwa kweli ameemewa, hawezo kutoa huduma stahiki inavyotakiwa.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba tumeweza ku-*address* tatizo la *access to health services*, sasa twende hatua nyingine ya ku-*address* tatizo la *quality* (ubora wa huduma za afya) kwa maana ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na Waganga na Madaktari na vifaatiba vya kutosha ili huduma hii muhimu iweze kupatikana kwa wananchi wetu ambao wanaihitaji sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni eneo la miradi ya maji. Kwanza nitumie fursa hii, kama Mbunge wa Jimbo la Bukene, lakini Mbunge katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, kuipongeza Serikali kwa mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria. Tunafahamu kwamba Serikali imewekeza shilingi bilioni 600 ili kuhakikisha maji yanatoka Kahama na kufika Tabora Mjini. Kutokana na zoezi hilo, sisi watu wa Nzega tunanufaika; tuna vijiji vingi sana ambavyo vitapitiwa na maji na kufanya wananchi wetu wapate maji salama ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mradi huo mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria, Serikali kwa kutumia Mfuko wa Maji wa *WSDP (Water Sector Development Programme)* imetupatia shilingi bilioni tatu kwa ajili ya miradi ya bomba yanayotokana na visima virefu. Katika Jimbo langu la Bukene pekee tunakwenda kupata visima virefu katika Vijiji vya Mambali, Lugulu Lwanzungu, Luhumbo, Bukene yenyewe, Kabanga, Itunda, Kasela, Isagehe, Ilagaja, Lyamalagwa, Mwamala na Kayombo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vijiji 12 ambavyo shilingi bilioni tatu itatumika kutafuta maji chini ya ardhi na kujenga miradi mikubwa ya kusambaza maji ya bomba. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo liko wazi. Kama mwakilishi wa wananchi, naipongeza Serikali kwa juhudhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kuwe na *flexibility* katika matumizi ya fedha hizi, kwa sababu eneo letu la Nzega na Mkoa mzima wa Tabora kuna tatizo la kupata maji chini ya ardhi. Sasa hivi mkandarasi yuko *site*, lakini visima vingi anavyochimba anakwenda mpaka mita 150, 200, lakini anakosa maji. Kwa hiyo, kuwe na *flexibility* kwamba endapo tutakosa maji chini ya ardhi, fedha hizi ziruhusiwe kutumika katika vyanzo vingine ambavyo siyo lazima iwe chini ya ardhi, kuna vyanzo vya mabwawa, kuna vyanzo kwa mfano maji ya Ziwa Victoria yakifika Nzega yenye we plia yatakuwa chanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fedha hizi zitumike kwenye usambazaji kwa sababu kuna uwezekano tukakosa kupata maji chini ya ardhi kwa visima vyote ambavyo tumepanga kupata. Kwa hiyo, ushauri wangu hapa ni *flexibility* ya matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la barabara; ninafahamu kwamba sasa hivi mkandarasi yuko *site* kwa maana ya kufanya upembuzi wa kina kwa barabara ya kilometra 189 ambayo inatoka Tabora kuititia Mambali – Bukene – Itobo – Mwamala – Kagongwa na hatimaye kuunganisha na Mkoa wa Shinyanga. Hii ni barabara muhimu sana kwa sababu itaunganisha Mikoa ya Tabora na Shinyanga kwa kuititia maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa sana wa mpunga, alizeti na mazao mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba Serikali ifanye usimamizi wa karibu sana kwa huyu Mkandarasi anayefanya usanifu wa kina, kwa sababu mkataba unasema, anapaswa kukabidhi kazi hii mwisho wa mwezi wa Kumi na Mbili mwaka huu. Kwa mujibu wa

makubaliano ya awali ni kwamba barabara hii katika Miji ya Bukene na Itobo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Vedasto Ngombale, kama niliyosema, atafuatiwa na Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kusema katika hotuba ya mtani wangu Waziri Mkuu kwa niaba ya wananchi wa Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Maadhimisho ya Sherehe za Vita vya Majimaji. Historia inaeleza wazi kwamba Vita ya Majimaji ilianza Kilwa na sababu kubwa ya kwa nini Wahenga wetu wale walianzisha ile vita, ni kwa sababu walikuwa wanakataa kunyanyaswa, wanakataa kunyang'anywa ardhi yao, wanakataa uonevu, lakini walikuwa na ujasiri mkubwa wa kupambana na Mkoloni Mjerumani ambaye alikuwa anatisha sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Pwani tuna misemo yetu ambayo ina maana na hekima kubwa. Watu wa Pwani tunasema, raha ya maji ya dafu yanyewewe kwenye kifuu chake. Maji ya dafu yakinyewewe kwenye bilauri hupoteza ladha. Yakinyewewe kwenye bilauri hupoteza sifa na harufu yake. Tabia ya dafu ukilipasua ukatoa mzibulio, ukachokoa basi sharti unywe kwenye kifuu chake. Ukichukua yale maji kuyapeleka kwenye bilauri, ladha inapotea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi inayojitambua. Siamini kama inafanya mambo yake howyo

hovyo. Kila linalotokea ni historia! Katika hali ya mshangazo, watu wa Kilwa tunashangaa kwa nini Sherehe za Vita ya Majimaji zinazogharamiwa na bajeti ya Serikali zinafanya Songea na siyo Kilwa, Nandete? Hatuelewi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waandishi mbalimbali wanazungumzia Vita ya Majimaji. Mwandishi Clement Gwasa anasema, Vita ya Majimaji ilikuwa *planned* na sababu zake zilanza toka mwaka 1903 na kuja kupigana mwaka 1905. *It was very, very planned.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa ninajuliza, hivi ni vigezo gani viliviyotumika kuzipeleka zile sherehe zinazotambuliwa na Serikali Songea? Kwa sababu kama hoja ni watu kunyongwa, hata sisi viongozi wetu wa Kilwa walinyongwa. Kinjekitile alinyongwa; na Hassan Omar Makunganya alinyongwa. Uksoma kitabu cha *The Majimaji Uprising* kinasema, kiongozi wa ndugu zangu, watani zangu akina Mheshimiwa Jenista, Wangoni wa wakati huo, aliposhawishiwa ajiunge na kumwondoa Mkoloni Mjerumani, yeye alisema hana muda kwa sababu Mjerumani ni rafiki yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipofikia wakati wa Vita ya Majimaji, Chabruma aliamua tu kujunga na mapambano ya Vita ya Majimaji kwa sababu binafsi na sababu yenye we aligundua kwamba mke wake, Bi mdogo, si mwaminifu katika ndoa. Kwa sababu hiyo akaamua kwenda kwa DC kwenda kulalamika. DC akamwambia kama hivyo ndivyo, basi naomba unilettee ushahidi. Huyu kiongozi Chabruma alishindwa kupeleka ushahidi kwa DC, ndipo basi akaona kumbe hawa Wajerumani hawafai, basi na mimi nitaungana na Wamatumbi kumwondoa Mjerumani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama sisi tuliamua kupambana vita kwa sababu ya kutetea Utaifa wetu, ardhi yetu na umoja wetu, hivi nani sasa anastahili kupewa heshima kitaifa? Ni yule aliyejunga na Vita ya Majimaji kwa sababu binafsi au sisi tuliokuwa tuna lengo la kuwaunganisha Watanzania? Haya mambo yanaumiza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumefanya mambo mengi, sisi ndiyo Taifa ambalo tulithubutu kuhakikisha kwamba nchizote kusini mwa Afrika zinapata uhuru. Mwalimu Nyerere kwa sababu zake binafsi akaona hapana, lazima hawa wenzangu wapate uhuru. Sasa kama itatokea mtu akasema heshima hii ya sisi kuthubutu ipelekwe Rwanda, ni kitu ambacho hakieleweki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa najisikia kutetemeka ninapomwona Mkuu wa Majeshi anaenda pale Songea eti kwamba wale ndio majemedari wa Vita ya Maji Maji. Haieleweki! Naomba mtani wangu, Mheshimiwa Jenista, kalifanyie kazi hili, watu wa Kilwa tupate haki yetu kwa sababu ya ujasiri wa kuthubutu kumwondoa mtawala mkali sana, Mjerumani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hilo litaeleweka. Nilishauliza maswali hapa, ndugu yangu Mheshimiwa Mwinyi akanijibu vizuri sana, nikataka ufanyike upembuzi wa kihistoria, lakini kuna hoja pia ya sisi waathirika wa Vita ya Majimaji tulipwe fidia kama ambavyo wenzetu wa Kenya wamelipwa, wenzetu wa Namibia wamelipwa. Hakuna chochote kimefanyika, naomba hili lizingatiwe kwa sababu historia ni jambo muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye suala la watu wenye ulemavu; ukurasa wa 24 na 25 katika hotuba ya Waziri Mkuu anazungumzia suala la watu wenye ulemavu. Anaeleza kwamba Serikali pamoja na wadau wamechangia vifaa kwa watu wenye ulemavu. Amesema wametoa viti mwendo 240, wamechangia magongo ya kutembelea 350, bajaji sita, kofia pana 128, fimbo nyeupe 175, miwani maalum 70, shime sikio 20, vyerehani vinane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye ulemavu Tanzania na idadi hii ya vifaa vilivytotolewa na Serikali, nafikiri ni utani kwa watu wenye ulemavu. Walemovu wana mahitaji maalum kutokana na aina ya ulemavu walionao. Kuwa mlemavu siyo *planned*, ni suala linalotokea kwa bahati

mbaya. Serikali bado haijaangalia mahitaji muhimu ya walemavu kutokana na aina yao ya ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mlemavu wa ngozi hakuchagua kuwa mlemavu wa ngozi; na hitaji lake maalum kulingana na aina yake ya ulemavu, ni kupata mafuta maalum ambayo yatamsaidia kupambana na athari za miale ya juu. Sasa kama haya mahitaji hayatolewi bure na Serikali, mimi bado sielewi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlemavu asiyeona apate fimbo maalum; mlemavu kiziwi apate shime sikio; mlemavu wa viungo apate viungo bandia. Katika hali ya kushangaza, kati ya vitu vinavyouzwa kwa bei ya juu ni pamoja na viungo bandia. Vifaa hivi ni hitaji maalum kwa walemavu kulingana na aina yao ya ulemavu, vitolewe bure na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye ajira ya Watendaji wa Vijiji wa darasa la saba. Kadri siku zinavyozidi kwenda mbele kasi ya watumishi wa Serikali hasa wa kada ya chini kuichukia Serikali inaongezeka. Ni kwa sababu Serikali haijajipanga katika kuhakikisha haki za watendaji wa chini zinazingatiwa. Watendaji wa vijiji wameondolewa kienyeji eti kwa sababu wao ni darasa la saba... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Constantine Kanyasu ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba nitoe ombi kwa Serikali ya CCM ya Awamu ya Tano na ombi hili naomba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Lindi na Mtwara waniunge mkono kwa sababu hii ni hoja yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ya Awamu ya Tano, naomba sana haka kasungura kadogo tulikonako basi tukagawanye sawa sawa, kwa sababu sisi sote tunachangia kwenye haka kasungura. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naleta hili ombi? Kwa sababu ukipitia bajeti, hii ni bajeti ya tatu, bado Mkoa wa Lindi na Mtwara kwenye bajeti hii tunapata hasa kwenye pesa za miradi wa maendeleo kidogo sana. Kwa ushahidi jana dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia kalisema hili, kwamba bajeti iliyokwenda kwenye Bandari ya Mtwara ni ndogo. Siyo bandari tu, ye ye ameongea hivi kwa busara tu kwa sababu ya mazingira aliyonayo, lakini ukweli ni kwamba bajeti tunayopewa Mikoa hii miwili ni ya shida sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ukiangalla, juzi tu hapa kuna mradi umetokea wa ukuzaji wa maliasili Ukanda wa Kusini, lakini ukanda wenyewe wa Kusini uliotajwa na kupelekwa zile pesa ni Morogoro, Mbeya, Iringa, Liwale, Lindi haipo, Mtwara haipo na pesa zimetoka. Ni jambo la kushangaza sana! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu Mheshimiwa Masala amesema asubuhi hii, kuna barabara ya Masasi – Nachingwea – Nanganga, ile barabara upembuzi yakinifu umeisha mwaka 2015 lakini mpaka leo pesa zinatafutwa. Ipo miradi kwenye nchi hii imefanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2017/2018 na sasa wakandarasi wako kazini. Suala hili nimewahi kuliuliza, hivi kuna tatizo gani? Kuna barabara nyingine utasikia zimejengwa na fedha za nje, kwa nini hizi bararaba zetu za Liwale, Lindi, Mtwara hazijawahi kupata wakandarasi wa nje? Suala hili ni zito sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea hilo hilo sisi Mwenyezi Mungu alitujalia tukapata gesi asili Mtwara, nafikiri uletaji wa gesi ile Dar es Salaam palitokea vita sana ya maneno na migomo mbalimbali. Leo hii mkoa ambao una tatizo la umeme; kwa siku unakatika zaidi ya mara kumi au mara tano au mara sita ni Mkoa wa Lindi na Mtwara. Kulikoni Mkoa wa Lindi na Mtwara? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi zaidi, hata Kamati zako za Bunge zinazotembelea kukagua miradi iliyopewa fedha za Serikali, uendaji wa Mkoa wa Lindi na Mtwara ni mdogo sana na wakienda, basi walikuwa wamekusudia kwenda Songea, wakapitia Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati ya Ulinzi na Usalama imeweza kwenda Mtwara na Lindi, ni kwa sababu tu ya matokeo yale ya Rufiji, inasemekana wale watu wamejificha Lindi na Mtwara, walikwenda kufanya tathimini hiyo kuona kuna nini, lakini siyo kufuata miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai kwamba hakuna miradi ya maendeleo inayokwenda, inakwenda lakini ni miradi midogo sana. Hakuna miradi mikubwa inayovutia Kamati yako ya Bunge kwenda kukagua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ya Awamu ya Tano tusifanye hivyo. Sisi sote tunachangia kwenye pato la Taifa hili na tuna haki ya kufaidi matunda ya Taifa hili.

Vilevile nakuja kwenye upande wa elimu; upande wa elimu kwa kweli tunacheza, hatujaamua kuwekeza kwenye elimu. Kwa sababu kwa mujibu wa takwimu iliyotoka Hakielimu, wanasema walimu wanaokwenda madarasani kufundisha kwa ari ni asilimia 37. Ina maana wengine wote wanaokwenda ni kwa sababu wameajiriwa, ilimradi tu wanakwenda. Tatizo ni nini? Maslahi yao hayajatekelezwa. Walimu wanafanya migomo ya kimoyomoyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika kuboresha, tumeamua kuongeza tatizo lingine. Tumechukua walimu wa sekondari wakafundishe shule za msingi. Matatizo ya huko ni makubwa mno kuliko tunavyofikiria. Zoezi lile zimeendeshwa tofauti na Serikali mlivyopanga. Zoezi lile limeendeshwa kwa ubaguzi mkubwa na kwa uonevu mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa naongea na Afisa Utumishi wa Wilaya yangu, namuuiliza mbona kuna malalamiko makubwa sana kwenye hili zoezi? Akanambia

hata mimi taarifa hiyo nilikuwa sina, Afisa Elimu amefanya jukumu hili bila kunijulisha. Kweli haya malalamiko ya Watumishi wa Idara ya Elimu hata kwangu yapo. Wameachwa walimu wenye *Diploma* wanaendelea kwenye shule ya sekondari, wamechukuliwa watu wa *Degree* wamepelekwa shule za msingi. Kilichofanyika ni watu kukomoana. Wametumia hii *loophole* kama Mwalimu Mkuu (*Head Master*) akiona kwamba ana matatizo na mwalimu fulani, anamhamisha anampeleka shule ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kule badala ya kuwa shule ya msingi ama kuinua elimu, tumekwenda kufanya kama kule ni jela. Jambo hili haliwezi kukubalika. Ombi langu, Serikali hebu mrudie hili zoezi mwone ni namna gani limetekelezwa kama nia yenu ilikuwa ni nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vilevile nataka nizungumzie taasisi hii inayoitwa *TARURA*. Taasisi hii ya *TARURA* imeundwa kwa nia nzuri kama mnavyodai, lakini taasisi hii mpaka leo hii haieleweki mhimili wake ni upi? Sisi Wabunge hatuna nafasi ya kuihoji *TARURA*. Halmashauri, Madiwani wetu hawana nafasi ya kuihoji *TARURA*. Juzi nimeuliza swali hapa Mheshimiwa Waziri anasema, *TARURA* watapeleka ripoti yao kwenye *DCC*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hebu tujiulize, ni wangapi tunahudhuria hizo *DCC*? *DCC* kwa mwaka zinakaa mara ngapi? Pamoja na kwamba kwa mujibu wa sheria wanatakiwa wakae mara tatu, lakini sina hakika kama kuna Wilaya yoyote ile inayoweza kutimiza hiyo azima ya mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba hawa watu wako huru, wanajifanya mambo wavoyotaka. Kuna u-specialist gani wa Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ambaye anamzidi Mhandisi wa Maji, Afisa Elimu na Afisa Maliasili au Afisa Ustawi wa Jamii? Maana hawa wote tunakuwa nao kwenye Baraza la Madiwani. Kwa nini huyu Meneja wa *TARURA* asiingie kwenye Baraza la Madiwani, ukizingatia hizo barabara anazozihudumia ziko chini ya

Halmashauri. Vipaumbele vya barabara gani ijengwe kabla ya ipi, sisi Halmashauri ndio tunajua. Sasa nataka kufahamu, Serikali jie na majibu, kwa nini kuna u-specialist wa *TARURA* isiende kwenye Halmashauri zetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nije kwenye uwekezaji; mnaongelea mambo ya uwekezaji, lakini uwekezaji huo una matatizo makubwa sana hata kwa wawekezaji wadogo. Hizi mamlaka za usimamizi zimekuwa ni nyingi sana na tumekuwa tukilia hapa mara kwa mara kwamba kama inawezekana, hizi taasisi nyingine ziunganishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujuu tatizo la uwekezaji nchi hii hasa kwa wawekezaji wadogo, hebu fungua kiwanda kidogo tu cha kusindika tu sembe, atakuja *NEMC*, atakuja *TFDA*, atakuja *TBS* watakuja sijui *TRA*, watakuja sijui watu wa *OSHA*, ni vurugu mtindo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sasa ili uweze kuwa mwaminifu ukatekeleza hayo yote, basi kama siyo miezi miwili au mitatu itakuchukua kupitia kwenye hizi taasisi. Kwa sababu ingewezeekana hizi taasisi zote zingekaa pamoja au kwenye ile fomu moja ambayo utajaza hawa watu ukawakuta kwenye sehemu moja wakujazia hizo fomu wakaku-*verify* ukafanya hiyo kazi, lakini hapana. Leo utakwenda taasisi ya...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Na *OSHA*, umeshaosha, ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa kama nilivyosema.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Kwanza kabisa naipongeza sana hotuba ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri iliyofanyika. Pia nampongeza sana

Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuwafanya Watanzania. Hata ukiangalia michango ya Wapinzani, imebaki mambo machache ambayo naamini baada ya bajeti hii, watacaa sawa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema humu ndani kwamba mimi ni darasa la saba; na humu ndani tuna matabaka tofauti, inawezekana ni vizuri zaidi kila mtu akatetea wenzie. Nampongeza Mheshimiwa Rais alipoenda pale bandarini akiwa anazungumza na watumishi wa Bandari kuhusiana na suala la vyeti *fake* na wale walio-forge kutoka darasa la Saba kuwa na vyeti vya *form four*, alitamka waziwazi mchana kwamba wale wote walio-forge vyeti kutoka darasa la saba kwenda *form four*wafukuzwe kazi, lakini wale walio na vyeti vyao vya darasa la saba na kazi wanazozifanya wanafanya vizuri, waendelee na kazi, kila mtu alisikia na suala hilli lilisemekana lilizungumzwa mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa humu ndani kuna wasomi wengi, lakini pia kuna wa darasa la saba wengi na huko nje hata ninyi wenye *degree* humu ndani, kuna ndugu zenu wa darasa la saba ambao walikuwa wameajiriwa hizo ajira ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri sana Serikali yangu, ninashangaa ni kwa nini wamewafukuza Watendaji wa Vijiiji wa darasa la saba. Wanataka hizi nafasi za darasa la saba, hizi za utendaji wapewe watu waliotoka Vyuo Vikuu. Ni wapi? Ni Wilaya gani? Ni Kijiji gani ambako mmepeleka Mtendaji *graduate* akawezekufanya kazi akawazidi darasa la saba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefukuza madereva, hivi niwaulize ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri, wewe unasomesha mtoto wako *English Medium* kwa hela nyingi anaenda sekondari, *form six*, Chuo Kikuu, akitoka Chuo Kikuu tena akawehereva? Hivi tunafanya mambo gani ya ajabu? Ninaomba sana Serikali yangu tena na Wabunge wenzangu wa CCM tuitake Serikali itoe tamko la kuwarudisha watendaji

hawa kwenye kazi, siyo kuwalipa. Haiwezekani mtu amefanya kazi toka mwaka 2004, unakuja kumfukuza leo. Hatuzungumzi suala la kulipwa mafao, warudishwe kazini watoke kwa muda wao wa kustaafu na hili limefanyika hata kwenye Majeshi. Kwenye majeshi enzi hizo, watu walikuwa wanachukuliwa darasa la saba, leo wengine ni Mameja, wengine ni ma-*OCD*, wameachwa mpaka wastaafu. Iweje Watendaji tunawafukuza? Mtu amebakiza miaka miwili, unamfukuza! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe Serikali iwarudishe. Kama Serikali itakaidi, mimi nataka niwape ushauri, kwa sababu humu ndani kuna Wabunge kama sikosei 100 na zaidi wa darasa la saba, siyo la saba tu, hata *form four failure* wamo, vyuo vikuu wenye vyeti havieleweki wamo humu ndani. Ninaomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi mnisikillize vizuri, ni kwamba kama hamwezi kuwarudisha hawa Watendaji na sisi Wabunge wa darasa la saba humu ndani mtufukuze. Halafu siyo kwamba mtufukuze, kwa sababu ukiangalia...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma, kaa kidogo tu. Taarifa, tunakutunzia muda wako.

T A R I F A

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa shemeji yangu anayechangia kwamba kama kuna wasomi wa vyuo vikuu wenye vyeti feki, ni muhimu akawataja hapa ili wajulikane ili asituhumu watu kwa ujumla wake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma, unasemaje?

MHE. JOSEPH K MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kama ni taarifa, lakini *record* yako inajulikana Chuo

Kikuu ulikuwa na kazi gani. Sasa unaweza ukawa ni wewe mmoja wao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni hata sababu ya Wabunge wa darasa la saba kuwa humu ndani na wale wenye vyeti ambavyo nimevitaja, ni bora katiba ikatuondoa humu ndani. Mkituondoa, mturudishe kwa Viti Maalum kama makundi mengine yaliyoko humu ndani, kwa sababu na sisi tuko wengi wa darasa la saba. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuangalia, hebu naomba uangalie tu ukurasa wa 49, kipengele cha elimu ukisoma namba 80 pale waliodahiliwa kuingia darasa la kwanza walikuwa milioni mbili, waliodahiliwa kutoka darasa la saba kwenda *form one* mpaka *form four* ni 500,000. Kwa hiyo, darasa la saba tena wamekuwa wengi kuliko walioenda sekondari. Ukiisoma hili taarifa, haikufafanua kutoka kwenye 500,000 kwenda chuo kikuu utakuta kuna 100,000. Kwa hiyo, ukipiga hesabu ya kawaida, sisi tuko asilimia 85. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ukiangalia walipakodi wakubwa Tanzania na Mheshimiwa Mipango na Waziri wa Viwanda yuko hapa, wajasiliamali wanaolipa kodi kubwa na wenye viwanda vingi ni darasa la saba. Hebu asimame hapa anitajie mtu mwenye kiwanda anayelipa kodi Serikali mwenye chuo kikuu hapa. Wote tumewaa jiri, halafu sisi tunakuja tunatozwa kodi, tunaonekana hatufai hata kwenye kazi zinazolingana na elimu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, kama tunaondolewa kwenye Katiba, nasi tuwekwe kwenye kundi la Viti Maalum kama wanawake na wale mavu, nasi tuwakilishe, twende hivyo hivyo na kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa sababu tunakosa wawakilishi kwenye Baraza lenu ndiyo maana mnataka kuwatoa hawa watu.

Naiomba sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa hili Waheshimiwa Wabunge tuungane kwa pamoja, ondoeni hata uvyama kwa sababu hawa darasa la saba mna

shangazi na wajomba zenu waliofukuzwa, mkijipigia makofi wenye Chuo Kikuu wachache tutakutana 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nizungumze suala la uvuvi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala hili hiyo *operation* nilizungumza kipindi kilichopita, *operation* ina maana nzuri na hakuna mtu anayekaa kwenye Kanda ya Ziwa aneyeshabikia uvuvi haramu. Ila uendeshwaji wa zoezi haukuufata haki. Tunazo mpaka risiti za watu wa Wizara, mtu ametozwa shilingi milioni 20 halafu risiti ikaandika 2,015, tunazo. Kwa nini mnakuwa wagumu kuunda Tume ya kuwachunguza hawa watu. Kuna Bray sijui kuna Sokomba huko Wakurugenzi, ni miradi wametoa watu wao Dar es Salaam kuwapeleka kule, wanachukua hela za watu wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri iundwe Tume ikachunguze zoezi hili. Nataka nikwambie kwamba ujasiriamali anaohamasisha Mheshimiwa Rais, sisi darasa la saba tunaupokea kwa hali na mali. Kuna watu leo wako Sirari pale, wamepewa vibali nya Serikali na Wizara ya kuleta mitego; mtu amepewa kibali mwezi wa Tano, mwezi wa nane, akaanza *process* za mkopo, akapata hela mwezi wa kumi na moja, akapeleka *order*. Amerudi hapa mwezi wa kwanza. Serikali imekagua ikasema iko sawa, Wizara ya Uvuvi, *TBS* sawa; kodi ikalipwa, kesho yake Mheshimiwa Waziri Mpina amesema mitego isitoke. Nimefuta vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu mpaka leo anaendelea kutozwa *storage* ya pale Sirari. Hakuna huruma, halafu mnahamasisha watu wafanye kazi. Ndugu zangu naomba sana, Mheshimiwa Waziri hebu unda Tume ichunguze suala hili la uvuvi. Kiukweli sisi watu tunaotoka maeneo ya uvuvi, mnatupa wakati mgumu sana kuzungumza na watu wetu. Hamfanyi haki. Naombeni sana iundwe Tume. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nilikuwa naomba kuishauri Serikali, katika uchumi wa Mheshimiwa Dkt. Magufuli anataka tujitegemee sisi wenyewe kwa kulipa kodi, tuachane na wahisani, lakini hizi sheria ambazo tunazitumia, ni za Kiingereza ambazo zinataka sisi tuendelee kuwa Watumwa wa Wazungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano, kuna sababu gani kijiji ambacho kama Mjumbe mmoja aliyechangia kwamba watoto wa shule wanatembea kilometra 11, wananchi wamehamashana, wamejenga madarasa mawili, matatu wakajenga Ofisi ya Mwalimu, wakajenga choo kizuri na mazingira mazuri. Wizara inakataa kufungua, inasema mpaka tufikishe madarasa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule inaanaza na darasa la kwanza, siyo darasa la saba. Ziliwekwa zile sheria ili tuendelee kukopa, tukamilishe kila kitu, tutaanza vipi? Umejenga madarasa mawili, unaanza na darasa la kwanza, mengine yatajikuta shule imefunguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, kuna sheria ambayo imewekwa inasema Kituo cha Afya hakiwezi kuwa Hospitali ya Wilaya. Ni hizo hizo sheria za kuendelea kufanya sisi watumwa tukakope hela kwa Wazungu. Kama tunatumia hizi hizi hela zetu za kupeana shilingi 200/shilingi 300/=, mimi Kituo changu cha Afya kinapungukiwa majengo mawili, kwanini ile shilingi 200 isiki-*top*kile Kituo halafu kikawa Hospitali ya Wilaya? Tunadanganyana hiki kitakuwa Kituo cha Afya halafu hapo hapo tutajenga Hospitali ya Wilaya, ambapo unanilettea shilingi milioni 500. Miaka 20 mimi nimeshakufa, Ubunge simo, nani anapata hiyo faida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali na Wawaziri mfikirie upya kuangalia hizi sheria za kuendelea kutufanya sisi tuwe tegemezi. Kama tunajitegemea wenyewe, turudi kwenye kile ambacho tunaweza kukifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Wizara ya Viwanda, Mheshimiwa Waziri Mwijage naomba sana kwa ushauri wangu hata nchi za China tunaenda kule, hawakuzingatia sana mambo ya viwango ndiyo maana wamefika hapa, ndiyo maana ukienda leo utapata shati la Tanzania, utapata shati la Marekani bei inakuwa tofauti. Sasa kuna kitu mnasema *gauge 32*, *gauge 34*, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri tuachie hata *gauge 38* hata 40 kulingana na umaskini wa Watanzania watu wetu Wasukuma wanataka wauze mahindi anunue bati aezeke nyumba, wewe uking'ang'ana na hiyo *size* yako ya *gauge 30* mbona kwenye Matembe na majani huendi kuzuia? (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma kwa mchango wako.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Constantine Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomari na Mheshimiwa Munira Khatib ajiandae.

MHE. COSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na nimepata nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba nitoe pongezi kwa hotuba nzuri na kwa kweli ninaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kushiriki katika tukio la uwashaji wa Mwenge pale Geita Mjini, nimpongeze sana kwa hotuba yake nzuri, lakini niwapongeze sana Wizara pamoja na watendaji wote ambao tulishirikiana nao kwa kiwango kikubwa na kwa kweli niwapongeze pia wananchi wa Jimbo la Geita Mjini ambao walijitokeza kwa wingi sana na kuvunja *record* katika siku ile ambapo Mwenge ulikuwa unawashwa na watu wa Geita hatuna cha kuwalipa tunawashukuru sana kwa sababu ni tukio la kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mliona tulipeleka sherehe zile za kuwasha Mwenge sehemu ambapo ni katikati kidogo ya msitu, ille ni eneo maalum la hekta 12 ambalo tumetenga kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha michezo na wananchi wa Mkoa wa Geita kama wangepewaa nafasi ya kusema neno moja kupitia mwakilishi wao, basi ombi lao kubwa lilikuwa ni msaada wa kupata namna ya kujenga uwanja wa michezo wa Mkoa wa Geita. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba sana hilo lisikike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niende kwenye suala la uvuvi, ninaunga mkono zoezi la kupiga vita uvuvi haramu na tangu nimeanza kuzungumza Bungeni hakuna sehemu niliwahi kukosoa au kuunga mkono uvuvi haramu. Tatizo langu kubwa limekuwa ni *approach* iliyotumika kupambana na *operation* yenyewe lakini pia na namna ambavyo huko chini linavyotekewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unakumbuka katika matukio tulipokuwa hapa Bungeni niliomba mwongozo baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri alipokiri kwamba nyavu ya dagaa ya milimita nane inaweza ikakamata samaki aina ya Sangara ambaao wako chini ya sentimita 55 na akakiri kwamba nyavu ya dagaa inaweza ikaja na samaki wadogo wadogo. Naibu Spika baada ya Naibu Waziri kukiri alliagiza Serikali tangu siku hiyo iache kusumbua wananchi wanaokamatwa hovyo, wanaopigwa faini hovyo kwa sababu ya kukutwa na samaki wadogo wadogo, kumbe nyavu zina uwezo wa kukamata samaki wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maagizo hayo ya Bunge hili, wananchi waliendelea kukamatwa, wameendelea kutesema na hali ya maisha ya wananchi wanaozunguka ziwa ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa ni moja tu tumefikiria sana *size* ya samaki wa kuuza nje wanaoanzia sentimita 50 kwenda juu wa sangara tukaacha kufikiri kwamba samaki ni maisha ya wananchi wanaozunguka ziwa. Samaki sangara ambae anauzwa nje anaanzia sentimeta 50 lakini

sato ambae hauzwi nje anaanzia sentimeta 25; sasa samaki sangara ambae analiwa Tanzania lazima aanzie sentimeta 50 sawa na anayeuzwa nje kitu ambacho hakiwezekani kwa sababu nyavu zilizoruhusiwa na Serikali zinaweza kukamata samaki size ndogo kuliko ambao wameruhusiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mateso wanayoyapata wananchi ni makubwa sana hivi sasa tunavyozungumza Mtendaji wa Kijiji anakamata samaki, Mgambo anakamata samaki, Polisi anakamata samaki na matukio mabaya kabisa ambayo yanaendelea. Siku moja nilikuwa Geita mama mmoja anawenda kumsalimia mwanae hospitali ana samaki wanenye wamebanikwa amebeba kwenye *box* ndani ya *hiace*, ikakamatwa *hiace*, akakamatwa na mwenye samaki, kosa la mwenye *hiace* ni kwa nini amesafirisha samaki wanenye *box* na kosa la mwenye samaki kwa nini amesafirisha samaki wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria haisemi hivyo, sheria inataja kama unataka kusafirisha samaki uwe na usafiri maalum wa samaki, lakini samaki wale ni wa biashara siyo samaki wa kula. Kuna matumizi mabaya sana ya sheria. Tulipotunga kanuni za uvuvi tuliweka Sheria ya Adhabu inasema kuanzia shilingi 50,000 mpaka shilingi 2,000,000, Waziri amekwenda amechukua Sheria za Mazingira akaziingiza kwenye Sheria za Uvuvi, akasahau mukhtadha wa uvuvi ni wa watu maskini anapiga faini kuanzia shilingi 50,000 mpaka shilingi 50,000,000, matokeo yake mtu mwenye mitumbwi miwili; mwenye mtaji wa milioni sita anaambiwa faini ya milioni tano, matokeo yake wavuvi wote wamefilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi tulikamata nyavu mpya tukazichoma moto. Katibu Mkuu wa Wizara wakati anachoma moto alikuwa anasikitika anasema ninachoma moto huku roho inaniuma nyavu za bilioni mbili. Mimi nikajiuiza, mimi nimesoma *Mbegani Fisheries*, kwa nini hakuchukua nyavu zile akapeleka chuoni wale wanafunzi wakajifunza kukata, kutengeneza *single* au akawapelekea *Nyegezi Fisheries* wakajifunza kutengeneza *single* ili wawape vijana wafanyakazi za uvuvi. Unachukuaje mtaji wa bilioni

tatu unachoma moto nyavu mpya halafu unasikitika huku unafanya unachotekeleza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho angefanya angechukua zile nyavu akasema kumbe nyavu iliyoungwa mara tatu inaweza kukatwa ikapatikana *single* akawapelekea chuongi, akawaambia ninyi chuongi jifunzeni kushona, jifunzeni kukata, wapeni watu wanaohitaji mitaji ingewasaidia. Sasa mtu huyu aliyechomewa nyavu amekubali masharti, amepata hasara. Amendika kibali cha kuomba kuagiza nyavu nje mwezi wa kwanza, leo mwezi wa nne barua zake ninazo hapa hajaruhusiwa, kule wavuvi hawana nyavu, wamekaa, Serikali imekaa, wanaangaliwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kambi ilikuwa na wavuvi 50 hakuna mvuvi hata mmoja, viwanda vile vya samaki vya Mwanza *vime-paralyze*, wananchi wame-*paralyze*, Waziri hafanyi maamuzi nini tatizo hapa? Maagizo tukilalamika hayachukuliwi hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana inawezekana Waziri hafahamu yanayoendelea kule chini. Alichokisema Mheshimiwa Musukuma hebu tuunde tume tukasikilize watu. Kuna watu wamekufa kwa sababu ya kukimbia, wanawakimbia mgambo wanakuufa kwenye maji na huu ni uonevu wa hali ya juu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Kanda ya Ziwa maisha yetu ni uvuvi na ufugaji. Kwenye ufugaji kilichotokea mnajua, kwenye uvuvi kilichotokea mnafahamu, tunakwenda wapi sasa? Kwa sababu bahati mbaya sana Waziri wa Kilimo naomba nikuambie hata pamba tuliyokuwa tunaitegemea juzi imeanza kuliwa na wadudu na bahati mbaya sana matunda nayo yanaliwa na wadudu inawezekana isipatikane. Tunawasababishia umaskini Watazania.

Mheshimiwa iti, tunalolisema hili mimi ninazo karatasi hapa za watu walioomba vibali mwezi wa kwanza mpaka

leo hakuna kinachoendelea. Inatuumma sana kwa sababu hatukuingia humu kwa bahati mbaya, tuliingia humu kuja kutetea wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni suala la Watendaji, nilifunga safari nikaenda kwa Katibu Mkuu wa Utumishi kwenda kumuuliza hivi ni kwa nini tangu mwaka 2004 mpaka leo 2018 walikuwa hawajachukua hatua akaniambia mwaka 2004 ilipotolewa maelekezo na Katibu Mkuu Utumishi tuliwapa miaka mitatu, ilipoisha tukawapa miaka mitatu, ilipoisha waliokuwepo wakaka kimya. Busara ya kawaida ya waliokuwepo kukaa kimya waliona zoezi hili halitekelezeki, ndiyo maana walikaa kimya kwa sababu kama ingekuwa yule aliyekuwepo wakati ule anajua hili suala ni gumu, tangu mwaka 2010 angeagiza watu wafukuzwe kazi, sasa baada ya hapo watu walipata barua za ajira, watu wengine ni *pensionable* leo unawafukuza kazi unasema hawa wameiingizia Serikali hasara, hili siyo la kweli na halikubaliki na hatuvezi kulikubali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo naomba niliongee ni la wananchi wangu wa Geita. Geita tuna mgogoro na watu wa *GGM*. Tangu miaka mitatu, minne iliyopita Mawaziri walikuja karibu sita, nyumba za wananchi karibu 800 zimepasuka kwa sababu ya milipuko ya *GGM*, leo ni miaka mitatu Serikali ikitoa maagizo *GGM* hawatekelezi. Kuna wananchi pale wanakaa ndani ya vizingi vya *GGM* miaka 18 hawalipwi fidia, Serikali inatoa maagizo hayatekelezwi. Kuna wananchi Nyakabale, kuna wananchi Mgusu, kuna wananchi Manga wako ndani ya vizingi vya *GGM* hawaruhusiwi kufuga, hawaruhusiwi kulima, wanakamatwa na maliasili, wanakamatwa na mgodi lakini Serikali ilitoa maagizo mgodi hautekelezi. Nilitaka kufahamu ni nani... (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia

Shomar atafuatiwa na Munira Khatib na Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande ajiandae.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyotoa matumaini na iliyomfanya kila Mtanzania aende kifua mbele kutokana na hotuba ilivyopangika. Hata wasomi kwenye redio, kwenye mitandao, kwenye *television* wanazungumza *speech* yake jinsi ilivyokuwa zaidi ya kusomeka imetekelzeza na bado inaendelea kupendwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitazungumzia zaidi tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ujio wake Zanzibar wakati ule wa Sherehe za Mapinduzi na alipang’iwa kwenye ratiba kwenye mabanda ya maonyesho pale Maisara, watu walifurahi jinsi alivyohudhuria na jinsi alivyotekeliza wajibu wale aliopang’iwa. Zaidi ningependa kumuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Waziri wa Muungano na Zanzibar ni sehemu ya Muungano ningependa apange ziara yake kama Waziri Mkuu aje Zanzibar kuimarisha Muungano. Taasisi za Muungano Zanzibar zipo, wafanyakazi wa Muungano Zanzibar wapo kama anavyofanya huku Bara akazitembelea taasisi, akanong’ona na Watanzania waliokuwepo huku, basi tunaomba na Zanzibar afanye ziara kama hiyo. Tunampenda na tunamuomba aje Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza katika ukurasa wa 12 ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezengumza kuhusu mafanikio ya Watanzania na takwimu siyo mbaya katika ajira, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ningesema ajira kweli zinafanywa na zinatekelezwa vizuri, lakini kuna ajira nyingine tunaziacha. Kwa mfano, Mabalozi wetu wako nje tumewapa kazi wanashughulikia diplomasia ya uchumi lakini Watanzania wako wenyе *Masters*, wako waliokuwa na *degree*, wana *Ph.D* wamebobea kiswahili, kiswahili sasa hivi kina mantiki kubwa nje ya Tanzania. Watu wengi wanazungumza kiswahili na kinataka walimu wa kiswahili na Tanzania tunao walimu, sasa ajira ni hizi tunaziacha.

Baadhi ya walimu wetu tuwapeleke, tuwaambie Mabalozi watafute hizi ajira kwa upande wa nchi walizokuwepo baadae walimu waende wakasomeshe, ajira itapatikana na Kiswahili kitazidi kuendelea katika kila nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu kazungumzia kwamba tayari tumeshahamia Dodoma, baadhi ya wafanyakazi, baadhi ya taasisi na alifika hadi akasema wafanyakazi 3,829 wamehamia kwa awamu na bado wataendelea na ataimarisha miundombinu. Miundombinu aliyokusudia ni miundombinu mikubwa lakini ya ndani hapa Dodoma tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda barabara ya Sengia, *Site Two* kule, nenda maeneo ya *Area D* karibu mtasikia kumetokea ajali maana mashimo yaliyopo ni makubwa, kila mmoja anabidi ayakwepe, huku bajaji, huku pilipiki, huku gari sasa kila mmoja anakimbia shimo anamfuata mwenzie. Sasa kama kweli amekusudia tuiimarishe Dodoma iwe nzuri basi na barabara za ndani pia zitengenezwe ili tuweze kujisikia walipa kodi kwamba tayari Dodoma iko ya kileo na ya kisasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu sekta ya uzalishaji ambayo iko ukurasa wa 27. Nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini unapotaka kuzalisha kufungua viwanda ujitalidi kuwa na malighafi na malighafi zetu nyangi ni kilimo.

Sasa tuwahamasishe watu wetu kulima ili waweze kupata malighafi kama ni pamba, kama ni nyanya ama kitu chochote ili wakati tukiwa tunafanyakazi zetu za viwanda tutakapotoa mazao yetu yawe bei rahisi. Ikiwa malighafi tutanunua, tunaimarisha viwanda, itabidi mazao yatakayotoka yawe ghali, sasa lazima tutoe elimu kwa wakulima wetu, tutoe elimu kwa watu wetu wenye viwanda tuwaambie kwamba lazima tutekeleze wajibu wetu ili malighafi iweze kupatikana na tuweze kujitosheleza na kazi zetu ziwe kuimariika kwa mujibu wa shughuli zetu za viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi pia nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama alipofanya ziara yake Zanzibar, akatembelea Mikoa ya Zanzibar kuangalia mambo ya *TASAF*, kwa kweli ameimarisha Muungano, watu waliridhika na akaona kuanzia awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu vipi inavyokwenda na vipi Zanzibar imejikita katika kupokea mradi huu wa *TASAF*.

Sasa na yeje pia namwomba kuja kule Zanzibar isiwe ni mara yake ya kwanza tu, aendelee kuja kwa sababu miradi ya Muungano ipo ambayo inamhusu aje kuingalia na Wabunge wenzie tutakuwa pamoja bega kwa bega kuwa nae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Munira Khatibu atafuatiwa na Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande.

MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo inayoweza kumkomboa mwananchi hasa maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia sehemu ya madawa ya kulevyta. Tunashuhudia Waziri Mkuu na Wizar aya Vijana jinsi inavyopambana na masuala ya madawa ya kulevyta, lakini suala hili kwa kweli bado ni tatizo moja kubwa sana ndani ya Tanzania. Tunaona Mheshimiwa Waziri, askari wanakamata vijana wadogo wadogo kwa *issue* ya madawa ya kulevyta, tunajisahau kuwa vijana wadogo siyo waingizaji wa madawa ya kulevyta. Kuna wafanyabiashara wakubwa, kuna viongozi wakubwa, kuna watu maarufu. Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na mapapa hawa na kuachana na ngedere wadogo hawa

ambao wao ni watumiaji lakini tunajisahau kama kuna watu ndiyo waingizaji wa madawa ya kulevyta; kwa sababu unamkamata kijana mdogo ambae anatumia tu madawa ya kulevyta, ukimkamata bado madawa ya kulevyta ndani ya nchi yetu yanaendelea kuingia na watumiaji bado wanaendelea kutumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *sober house* nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kuna *sober houses* 22 ambazo tayari zimeanzishwa, lakini *sober houses* siyo *solution* ya kusema tunaondoa suala la madawa ya kulevyta. Hizi *sober house* kwanza tukumbuka ni nyumba za watu binafsi, kwa hiyo, *business* bado inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana waliopo ndani ya *sober house* wanasema kwamba wakianza kupona baadhi ya *sober house* wanapewa tena yale madawa ya kulevyta ili waendelee kuwepo ndani ya *sober house*, kwa sababu kijana mmoja aliyopo ndani ya *sober house* analipia shilingi 400,000, kijana yule akiondoka ile *businessimeondoka*, kwa hiyo, naiomba Serikali ifumbue macho na kuangalia hizi nyumba za *sober house* ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kama tunataka tuendelee na *sober houses* ziwekwe ndani ya mwamvuli wa Serikali, hilo ni jambo la kwanza.

Pili, tunataka vijana hawa ambao tayari wameshaathirika na madawa ya kulevyta wachukuliwe wapelekwe hospitali, watibiwe, wapatiwe tiba na watakopona wapewe mtaji badala ya kuwapeleka *sober house* zile pesa wapewe mtaji kwa ajili ya kuwaanzishia biashara yao, kwa sababu vijana hawa wanakuwa na changamoto za maisha hawana mtaji wa kuanzishia biashara. Zile pesa vijana hawa wapewe kwa ajili ya kuanzisha biashara na wataweza kuachana na madawa ya kulevyta na kufanya biashara zao binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ajira. Naomba niongee ukweli kwa sababu nitakapoongea ukweli

nitakuwa nimemsaidia Mheshimiwa Rais, tusimdanganye Mheshimiwa Rais tukimdanganya bado tutakuwa hatujamsaidia, ili tumsaidie tumwambie ukweli, vijana wamekosa imani na Serikali yao kwa suala la ajira, suala la ajira limekuwa changamoto tuwatafutie vijana ajira ili waweze kutatua mambo yao wawe na imani na Serikali yao. Tusipoangalia vijana hawa wote watakimbilia kwenye madawa ya kulevyaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Serikali kwamba haiwezi kuajiri vijana wote ambaa wanamaliza shule, lakini tuangalie njia gani tutafanya ili kuweza kuwasaidia vijana kuweza kujikwamua na maisha. Kwanza tukae na mabenki, tuzungumze nayo, yapunguze urasimu, yaweze kuwapa vijana mkopo wenye riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki zina urasimu mkubwa kijana kama mimi nisingekuwa Mbunge leo hii nahitaji mkopo naambiwa niende na hati ya nyumba natoa wapi? Naambiwa niende na hati ya shamba natoa wapi? Ni lazima tukae tufikirie ni njia gani ya kumkwamua kijana aweze kuijendeleza katika maisha yake. Kuna miradi ambayo kuwa Mheshimiwa Rais ameianzisha, lakini unashangaa wanatoka vijana kutoka Kenya, Malawi, sijui kutoka wapi ndio anakuja kusimamia ajira hizo, tunaiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ajira hizi zote zisimamiwe na vijana wa Kitanzania, kama miradi ya umeme ilioanzishwa Rufiji, *standard gauge* na ujenzi wa viwanja vyta ndege ajira hizi zote tunaomba zipate vijana wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu afya ya akina mama; kama mwanamke na kama mzazi nitakuwa sijajitendea haki nisipochangia suala la afya ya akina mama. Tulimuona Naibu Waziri akifungua warsha yake kwa vifungashio vyta akina mama na akisema kina mama wachangie shilingi 20,000. Bado kwa mwanamke shilingi 20,000 ambaye ana kipato cha chini ni kubwa sana, kwa nini asiseme vifungaishio hivi viwe bure au aweke shilingi 5000 ambayo anajua mwanamke huyo au mama huyu anaweza kuimiliki kila mwanamke wa kijijini, kila mwanamke maskini

anaweza kununua vifunganishio hivi, shilingi 20,000 bado kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu mazingira. Kila siku tunamshuhudia mama yetu Mheshimiwa Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan akienda katika warsha za kuendeleza misitu, tusikate miti hovyo, lakini nikwambie ukweli, miti bado itaendelea kukatwa kwa sababu bei ya gesi bado kubwa sana. Mwananchi wa kawaida huwezi kwenda kumwambia anunue gesi shilingi 50,000 akaacha mkaa shilingi 20,000, miti bado tunayo lakini hatujaua ni jinsi gani ya kuweza kulinda miti yetu. Kwa hiyo, hiyo miti tunayopanda tutashindwa kuilinda kwa sababu sasa hivi hatujui ni jinsi gani ya kuilinda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu isaidie akina mama maskini kwa kuweza kupunguza bei ya gesi.

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Munira kaa kidogo tu.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mdogo wangu anaongea mchango mzuri sana, wenye tija kwa Watanzania, lakini analenga Serikali ambayo kwa bahati mbaya Serikali haipo pale, hebu tuliangalie hili, Serikali haipo pale! Dada yangu unachangia maneno mazuri lakini Serikali unayo i-*addresshaipo*. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Munira taarifa ya uchokozi kwanza hiyo, Serikali ipo Bungeni Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge watambue utaratibu na wakati mwingine wawe pia na heshima kwa Kiti cha Waziri Mkuu. Wanaelewa wazi Serikali

kuwepo Bungeni, Mawaziri waliopo na Waziri wa Nchi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu akiwepo Bungeni Serikali ipo Bungeni. (*Makof*)

Ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuwa hayupo katika Kiti chake na yupo hapa Dodoma shughuli za Serikali zinaendelea ndani ya Bunge na nje ya Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge heshimuni Kiti cha Waziri Mkuu ndani ya Bunge na hata anapokuwa nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuendelee.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi nakushukuru sana kwa ufanuzi. Mheshimiwa Munira endelea.

MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu asilimia 10 inayotokana na vijana, akina mama na asilimia mbili kwa walemau. Tukiongea ukweli ndani ya Halmashauri yetu hii pesa haipatikani, naiomba Serikali itafute njia ya kuweza kusimamia Halmashauri hizi ili vijana waweze kupata hizi asilimia nne, wanawake wapate asilimia hizi nne, walemau wapate hizi asilimia mbili jumla itakuwa ni asilimia 10. Halmashauri itakapotenga hii pesa tutakuwa tumepunguza lile tatizo la kusema ajira kwa vijana, watajua jinsi gani kwa sababu ajira zipo nyingi, kijana anaweza kujajiri kwenye kilimo, uvuvi, lakini kijana huwezi kumwambia leo hii aende akalime kilimo cha *locally* au aende akavue uvuvi *locally* lazima atataka kulima kilimo cha kisasa cha kumwagilia maji, kilimo hicho ili uweze kulima uwe na milioni tano isipungue, sasa hizi asilimia 10 zitakazotolewa na Halmashauri zetu vijana hawa wataweza kujisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la bandari kidogo tu, bandarini pamekuwa na urasimu mkubwa sana,

sisi tunaosafiri kupitia baharini pale ndiyo tunaona. Kijana anasafiri na vitenge doti 10 tu anaambiwa sijui *TRA* achangie, ushuru wa bandari, hebu tufikirie kijana huyu vitenge 10 atapata faida shilingi ngapi, pesa yote ambayo anachajiwa pale bandarini ndiyo pesa yake yote anayopata faida. Kwa hiyo anakuwa anafanya *business as usual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie tena amechangia Bara anaenda Zanzibar anachangia tena, naomba haya mambo tuyaaangalie huu urasimu mdogo wa kuondoka na doti 10 hapa za vitenge, halafu kijana yule akienda Zanzibar anakuwa-*charged*.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa.

TAARIFA

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwa kumuongezea. Kitu ambacho unakilipia Tanzania Bara tulipitisha kipindi tulichopita na kitu kile ambacho kinazalishwa Bara kitolewe ushuru kwa matumizi ya Zanzibar, maana yake unaweza ukalipia Bara na ukienda Zanzibar vilevile ukalipia maana yake unaendelea kulipia ushuru mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimpe taarifa mdogo wangu aweze kuendelea vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante. Unasemaje taarifa hiyo Mheshimiwa?

MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo tena kwa mikono miwili asilimia mia moja. Hivyo ndivyo ilivyo, tunaomba basi Serikali ikae ifikirie hili suala limekuwa tatizo sana kwa vijana wetu, hawatafika wakati wakaweza kujitegemea wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Munira. Tunaendelea na Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwanza kuchangia kuhusiana na suala zima la Tume ya Uchaguzi. Katika hotuba ya Waziri Mkuu alisema kwamba Tume ya Uchaguzi imekuwa ikifanya kazi kwa ufanisi, sasa ni ufanisi gani anaouongolea kama Tume hii mpaka sasa tumeiona ikiwa inatenda kazi kinyume na taratibu na kanuni zilizowekwa na sheria ambazo ziko wazi. Jambo la kushangaza zaidi Tume hii ipo chini ya Mwenyekiti ambaye ni Jaji, tulitegemea kwamba mtu kama Jaji angeweza kuisimamia hii Tume iweze kuwajibika na kufanya kazi zake wka kufuata taratibu na sheria na kanuni zilizopo. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tumeona katika chaguzi zilizopita Tume imekuwa ikibagulia Vyama vya Upinzani wote mnafahamu kwamba baadhi ya viongozi wetu wa CHADEMA sasa hivi wanakabiliwa na kesi, lakini kesi wanayokabiliwa nayo wanaambiwa kwamba walisababisha kifo cha mwanafunzi Akwilina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi hawa walisababisha vipi hiki kifo cha Akwilina ambacho kama ni kuna mtu wa kupewa hii kesi ni Jeshi la Polisi pamoja na Tume yenyewe, kwa sababu Tume hawakutenda haki hawakutoa barua za utambulisho wa mawakala kwa Vyama vya Upinzani. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi ya Bunge]

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 68(1) na utaratibu unaovunjwa uko katika Kanuni ya 64(1) lakini nitazungumzia Kanuni zinazofuata chini ya kifungu hicho.

Kwanza Kanuni hiyo ya 64(e) kinazungumzia wazi kwamba katika mijadala yetu ndani ya Bunge haturuhusiwi kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yejote anayeshughulikia utoaji wa haki isipokuwa tu kama kuna jambo ambalo ni mahsusii katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema tunapozungumzia Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ambaye pia ni Jaji na kama alivyosema mzungumzaji tunakiuka matakwa ya Kanuni hiyo. Kanuni pia inatukataza kama jambo lipo Mahakama halitazungumzwa na kujadiliwa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili analotaka kuendelea nalo Mheshimiwa Mbunge kulijadili, wote tunafahamu kwamba lina kesi ambayo inaendelea sasa hivi katika Mahakama. Kwa hiyo, ninaomba tu utuongoze vizuri katika utaratibu huu ambao nimeusema ili tunapochangia ndani ya Bunge tuende sambasamba na Kanuni ambazo tumejiwekea wenyewe. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Uamuzi wangu kwa hilo ni kwamba tusifike huko ulikotaka kwenda, kwa sababu suala hilo linasubiri uamuzi wa Mahakama, wewe jielekeze kuchangia hoja hii bila kwenda huko na huo ndio uamuzi wangu. Endelea Mheshimiwa Lathifah.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: *Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante lakini nafurahi kwamba ujumbe umeweza kufika. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lathifah unafahamu tusifanye hii michezo hii, ningeweza kukuambia uyafute yote uliyozungumza sikufika huko ni heshima ya Kibunge, sasa nataka uyafute, ninakutaka uyafute maneno yako.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nafuta.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuendelea na mchango wangu hapa kwenye suala la Tume ya Uchaguzi kuhusu taratibu ambazo zinatakiwa kufuatwa kila baada ya uchaguzi ni Daftari la Mpiga Kura linatakiwa kuboreshwa mara mbili baada ya uchaguzi kumalizika, mpaka sasa hivi tumeshuhudia kwamba Daftari la Mpiga Kura halijaboreshwa hata mara moja na sasa hivi ni mwaka wa tatu tangia tumalize uchaguzi uliopita. Sasa hii inatuwekea sintofahamu na tunaanza kuingia mashaka kwamba Tume wana mpango gani tunapoelekeea kwenye uchaguzi wa mwaka 2020 kama mpaka dakika hii hakujafanyika taratibu za kuhuisha Daftari la Mpiga Kura .

Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho kimetuletea mashaka na tunaomba Serikali iliangalie hili waweze kulichukulia hatua haraka iwezekanavyo ili tunapoelekeea kwenye uchaguzi hili zoezi liwe tayari limeshamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo liko katika uvezeshaji wa uchaguzi (*Electoral Support Program*) ambao ni mradi kwa ajili ya kuwezesha uchaguzi. Lakini kitu cha kusikitisha kabisa ni kwamba huu mradi haujapatiwa pesa hata kidogo. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 bajeti ambayo ilipitishwa ilikuwa ni shilingi bilioni 10 lakini hawakupewa hata senti tano na mwaka huu pia bajeti cha kushangaza bajeti imeenda kupunguzwa *by 50%* badala ya shilingi bilioni 10 wakati ule sasa hivi wanapewa shilingi bilioni

tano, sasa inakuwaje tunakuwa na mradi kama huu halafu hamna pesa yoyote ambayo inaenda kupidishwa, ningeomba hili pia liangaliwe kwa sababu mradi wa uwezeshaji wa uchaguzi ni suala muhimu sana na utahitaji kuwa na *funds* za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuongelea suala la *Commission of Mediation and Arbitration* (Tume ya Usuluhishi na Uamuzi). Nimeona katika hii hotuba ya Waziri Mkuu amesema kwamba kumekuwa na ujenzi wa Mahakama na ukarabati wa Mahakama mbalimbali lakini hamna sehemu aliyoongelea kuhusiana na suala hili muhimu la *Commission of Mediation and Arbitration*, tungeomba hili suala Serikali illichukulie umaanani na umuhimu kwa sababu mpaka sasa hivi imejitokeza changamoto nyinig sana kuhusiana na suala la Tume hii ya *Mediation and Arbitration*, kwanza hamna majengo ya kutosha, mpaka sasa hivi tunachokiona ni kwamba unakuta wanakuwa na chumba kimoja ambako ndio wanafanya hiyo *mediation* na zinavyokaa kesi mbili hadi tatu; kwa hiyo, kuna kuwa na muingiliano kunakuwa hamna *privacy*, huku wanafanya *mediation* na huku pia yaani kusema kweli tunahitaji sana kuwe kuna majengo ya kutosha. Pia kuwe kuna *staffing* maana iko *understaffed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoshangaa ni kwa nini Serikali inashindwa kuleta watumishi au kuajiri watumishi kwa ajili ya hii Tume ukizingatia tuna wanafunzi wengi ambao wana *graduate*, ishindikane vipi hawa watu washindwe kuajiriwa. Ningeshauri hili suala lingechukuliwa kama suala ambalo ni muhimu sana ikiwa kama kitengo cha kutaka kuhakikisha kwamba tunaimarisha eneo letu la utoaji haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuongelea suala la *strong institution for sustainable development*, tunahitaji kuwa na taasisi imara kwa ajili ya maendeleo endelevu. Nasema hivi ni kwa sababu taasisi zetu zinahitaji kuwa na uwezo wa kujijendesha, uwezo wa kujisimamia katika maamuzi yake, lakini kitu ambacho

kinaendelea sasa hivi unakuta kwamba mfano mdogo tu naweza kuutoa ni Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi sasa hivi kinachoendelea ni kwamba mtu anaweza akachukuliwa akawekwa mahabusu kwa muda wa siku 14 pasipo kupewa haki yake ya kufikishwa Mahakamani. Kinachobaki wanakuambia kwamba wanasubiri maelekezo kutoka juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokuwa na taasisi kama hizi, zinakosa kujisimamia na kuweza kujiendesha bila kutegemea maamuzi ya mtu huyu mmoja, naomba niwakumbushe kwamba Ujerumanu kulikuwa kuna Adolf Hitler, alikuwa anaingilia mifumo ya utoaji haki. Aliingilia hadi Jeshi la Polisi na ilipelekea hadi kukawa na machafuko. Hatutaki kufikia huko, sasa tunaomba ifike wakati taasisi zetu zijengewe uimara, ziweze kujitegemea zenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi ndiyo hapo ambapo tunakuta kunaweza kukajitokeza majanga kama mafuriko, lakini sasa kitu cha kushangaza ni kwamba hamna pesa za ndani zinazotengwa kwa ajili ya kitu muhimu kama hiki...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, muda wako ndiyo huo umeisha! Mheshimiwa Oscar Mukasa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe na tuangalie muda na Mheshimiwa Balozi Adadi.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru Mungu kwa uhai na afya na ninaendelea kuwashukuru wananchi wa Biharamulo kwa kuendelea kunipa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ujumla wake, lakini kuna maeneo ambayo inabidi tuseme. Biharamulo hivi tunavyoongea sasa hivi, kuna kilio kikubwa sana cha

wakulima wa pamba. Wakulima wa pamba wameingia kwenye dimbwi ambalo hawajui na hatujui tunatoka vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dawa kwa ajili ya kupambana na wadudu, tunaambiwa wanaletewa dawa aina ya Duduall, Duduba na Bamethrin. Dawa hizi hazifanyi kazi, kabisa na kuna maoni mara tatu. Wataalam wetu wa kilimo wa Halmashauri ya Wilaya pale wanasema tatizo la kwanza ambalo wanadhani ndiyo linasababisha hili inawezekana ni kukosekana kwa mwendelezo wa upatikanaji wa dawa kwa sababu mkulima anapotakiwa kuweka dawa kwenye pamba wiki ya mbili, lakini labda anatakiwa wiki ya nne apate dawa nytingine isipokuja kwa wakati hao wadudu wanajenga usugu.

Lakini kuna malalamiko kutoka kwa wakulima hao, wakulima wanasema wanapokwenda kwenye maduka binafsi wakachukua dawa kwenye maduka binafsi mbali na hii dawa inayoletwa na Bodi ya Pamba dawa hii inafanya kazi. Hiyo ni *hypothesis* inayoonesha kwamba inawezekana kwenye dawa inayopita kwenye Bodi ya Pamba kuna uchakachuaji na wamefikia hatua ya mbali wakulima wakafanya utafiti wao wenyewe (wakulima wa Biharamulo wana akili sana) kuna tuhuma kwamba wakulima hawa hawatumii vizuri dawa ndiyo maana haifanyi kazi. Wakamtafuta Afisa Ugani wakampeleka kijiji, pale Kijiji cha Kagondo, Kata ya Kabindi wakamwambia chupa ya dawa hii hapa changanya mwenyewe weka kwenye shamba mwenyewe. Akafanya hivyo mtaalam wakaenda siku inayofuata wakakuta wadudu sio tu wapo, inawezekana wameanza kuota na macho wanatazama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakasubiri wiki moja wakaenda wakatazama. Wadudu wapo! Wakasubiri wiki tatu, wakamuita na Afisa Ushirika akaja kutazama, wadudu wapo! Kwa hiyo, kuna tatizo. Inawezekana kuna uchakachuaji wa dawa kwenye Bodi ya Pamba kwa sababu wakulima hawa wakienda kuchukua dawa kwenye maduka binafsi inaonekana dawa ile inafanya kazi. Sasa tuna maswali mawili.

Swali la kwanza, tunatatuaje tatizo kwa msimu unaofuata? Lakini swali la pili, tunawafidia vipi wananchi hawa kwa sababu Bodi ya Pamba ambayo ni taasisi ya umma ndiyo imewaletea dawa na tuna sababu kwanini tunataka kudai fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa pamba kwenye msimu juzi ulikuwa hekta 500 kwa Wilaya nzima, msimu jana heka 900 na msimu huu heka 2,800 na mwaka jana msimu uliopita wameuza wamepata jumla ya kilo milioni sita. Kwa hiyo, uzalishaji umepanda sana kwa sababu ya uhamasishaji na wananchi walikuwa na matumaini sasa ya kuondoka kwenye umaskini. Msisahau Biharamulo ndiyo Wilaya ya pili kwa umaskini nchi hii kwa kipato cha ngazi ya kaya, mnafahamu. Sasa kama kupitia kilimo ndilo eneo ambalo wananchi wanaweza kujiinua lakini Serikali na vyombo vyake havitimizi wajibu wao ina maana tunakaa kwenye mzunguko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama ukurasa wa 29 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna ushahidi kabisa wa kitu kinaitwa *The know-do gap*. Tunachojuu ni moja lakini tunapokwenda kwenye *field* hatufanyi hiyo moja, tunafanya mbili. Anasema kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba moja ya matatizo yanayosababisha kilimo kisiwe moja ya nyanja zetu ambazo zinatuinua kiuchumi ni, kuna habari ya ukosefu wa utafiti, ukosefu wa pembejeo, ametamka Waziri Mkuu, tunafahamu lakini hatufanyi! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza wananchi wangu wakulima wamenipigia simu wameniambia chupa mbili za hii dawa ya Duduall ambayo imekuwa inatumika kama ushahidi. Tunaiomba Serikali iende ikafanya tathmini ya hiyo dawa tuone kama je ni kweli kuna uchakachujai ama ni tatizo lile lile la ucheleweshaji wa dawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri Mkuu tufanye tunachoamini ambacho tumeandika kwamba tunavyoshindwa kufanya huduma ya ugani kwa wakulima

ni moja ya sababu kubwa ya kilimo kinakuwa hakina tija kwenye nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 27, Mheshimiwa Waziri Mkuu anataja kabisa kwamba tutaweka mkazo kwenye mazao matano yakiwemo pamba lakini ukurasa wa 32 anasema; "tumeamua kwa dhati kusimamia sekta ya kilimo."

Sisi huko kwetu Kagera kuna msemo unasema wakati mnakula chakula cha mchana au usiku pale, mtoto ambaye ni mroho ama mlafi unamuona wakati wa kunawa. Kwa hiyo, kama Waziri Mkuu anatuhakikishia sasa anaweka kwa dhati tunaomba aanze na Biharamulo, twende tukatazame hizo dawa ambazo tumetunza *sample*, twende tutazame tuone tatizo liko wapi, tatizo liko kwenye uchakachuaji, kukosa *consistency* ya kuleta dawa ama tatizo liko wapi? Hiyo ndiyo itakuwa alama sahihi kwamba huyu mtoto anayenawa sasa hivi vizuri hatakula kwa ulafi. Nakushukuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee habari ya Waziri Mkuu amesema ukurasa wa 38 na 39 habari ya madini. Tunatambua Mheshimiwa Rais anaendelea na utaratibu wa kuunda ile Kamisheni. Tunaomba twende kwa kasi kwa sababu wananchi wa Biharamulo tumeypata maeneo ya uchimbaji wa madini pale, tunahitaji kupata leseni, tumeshajipanga. Huu muda unavyokwenda tunaendelea kupoteza ile *momentum* na tutakosa fursa ya kufanya kazi yetu vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo viwanda. Mheshimiwa Mwijage yuko hapa. Nimeona kwenye ukurasa wa 35 wa hotuba ya Waziri Mkuu tunasema viwanda 3,000. Naomba tusiiweke *too general* tuzungumze kwenye hivyo 3,000 vingapi ni vikubwa, vingapi ni vya kati na vingapi ni vidogo, lakini pia twende mbali zaidi, tutafute utaratibu wa *incentive*, namna gani mtu unamvutia. Unajua kuwekeza kiwanda Dar es Salaam kwa sababu ya baadhi ya miundombinu na kuwekeza kiwanda Biharamulo kuna

tofauti! Tukiwawekea hawa *private sector incentive* kwamba akiwekeza Biharamulo kuna zawadi fulani ambayo anaipata kikodi ili apunguze maumivu kwa sababu ya habari nyingine za miundombinu ya aina mbalimbali itamfanya aende kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ikitokea na mimi Mbunge au Mkuu wa Wilaya, mtu ye yeyote kutoka Biharamulo akawezesha kupata wadau ambao wataweka kiwanda pale Halmashauri nayo ipate *incentive* namna gani Halmashauri itapata *incentive* kikodi badala ya ushuru kwa sababu tunajua vyanzo vingi vimehamishwa kutoka kwenye Halmashauri kwenda Serikali Kuu. Tukienda namna hiyo tutapata namna sahihi ya kuweshera hata kule ambako kimiundombinu ni vigumu watu kwenda, lakini ukiwawekea uvutiaji watakenda na mambo yataaka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo niongelee uwesheraji wa makundi maalum. Naomba tuwakumbuke Watanzania wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Ni kundi maalum ambalo linashiriki kwa kiwango kikubwa kwenye ile habari ya 90-90-90. Asilimia 90 ya watu wanaodhaniwa kuwa na virusi vya UKIMWI wapime, asilimia 90 ya waliopima watumie dawa na asilimia 90 ya wanaotumia dawa watumie vizuri ili ifubae. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakitumia dawa vizuri siyo faida ya kwao peke yao ni faida ya umma mzima. Anapokuwa ametumia dawa kwanza anaondoa utegemezi wa kiuchumi kutoka kwa umma mzima kwa sababu ana uwezo wa kufanya kazi, lakini kama unampa uwesheraji anaweza akapata Bima ya Afya yeye na familia yake wasiwe na utegemezi. Pia hiyo ni namna moja ya kufanya *prevention* kwa sababu mnajua *prevention is better than cure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo hili la walimu wa sekondari kutolewa sekondari kwenda shule ya msingi, najua ni dharura na Mheshimiwa Ndalichako naamini ananisikia na nilimwambia kidogo kule kwenye Kamati, naomba nisisitize. Nafahamu ni dharura, lakini ni kwa kiwango gani hili tunalifanya kwa muda mfupi lisiwe

endelevu? Kwa sababu likiwa endelevu hili halina tofauti na ile habari ambayo nakumbuka nimewahi kumwambia Waziri, jamaa mmoja alienda kwa fundi wa kitanda akamwambia nitengenezee kitanda cha nne kwa sita, fundi akakosea akatengeneza nne kwa tano. Jamaa alivyokwenda kupima pale akakuta miguu inazidi anamuuliza fundi, tufanyaje? Fundi anasema hapa njia rahisi kabisa ya mkato ni kukata miguu ili kitanda kitoshe. Tukienda namna hiyo kwa muda mrefu, kwamba kazi yetu itakuwa ni kurudisha walimu wa sekondari shule ya msingi kuna mzunguko ambaao tutaingia, walimu wa sayansi haitatokea siku watoshe...

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Mukasa. Sasa kidogo tusaidiane maana uelewa huu ni mzuri sana. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa Kanuni 68(7) niombe Mwongozo wako kuhusu mzungumzaji aliyekaa. Amesema kwamba anazo *sample* za dawa *Duduall* ambazo amethibitisha huko kwamba haziui wadudu. *Ordinarily* ningemjibu wakati wa hotuba ya bajeti ya Wizara ambayo ni mwezi Mei tarehe 15 na 16 sasa huko ni mbali sana na kama hiyo dawa ni kweli haiui basi, kuna watu watakuwa wanaendelea kuathirika mazao yao.

Kwa hiyo, niombe tu mwongozo wako kwa nini asinipatie hizi *sample* haraka iwezekavyo ili tuweze kuzipeleka kwenye maabara na kujiridhisha kama haziui *then* tuwatafute walioziruhusu na kuziingiza nchini tuwachukulie hatua mara moja.

MWENYEITI: Ni jambo jema tu na liko ndani ya Kanuni zetu, kwa sababu unaposema kitu humu Bungeni lazima uwe na uhakika nacho na siyo suala la kubahatisha au kubuni buni tu, Kanuni ya 63 ndivyo inavyotutaka hivyo. Kwa vile lina maslahi mapana ya zao la pamba na tuhuma inayoelekezwa kwenye Bodii ya Pamba kama ni kweli ni vema Mheshimiwa Mukasa kwa faida ya wananchi wanaolima zao la pamba katika Wilaya yako, lakini pia na maeneo mengine ya Tanzania *including* ninapotoka mimi ambapo ndiyo

tunaongoza katika zao la pamba nchini Bariadi, tuyaone haya kama ni kweli, *sample* hiyo inaweza ikazaa na mambo mengine.

Mheshimiwa Mbunge, ninakuagiza tu kama unayo hapa Dodoma uikabidhi kwa Waziri na timu yake ya wataalam, wanajua utaratibu wa kufuata katika masuala haya. Kama haunayo hapa sasa kuna changamoto nyingine kwa sababu kile unachotuambia unacho hapa hakipo, lakini kinapokuja kutoka kule inawezekana isiwe kile ambacho ulikuwa unatuambia, ningependa tuwe na uhakika na kile ulichokuwa unakisema humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuachia hilo utuambie unayo au utafanya utaratibu ulio wa uhakika kwamba isiwe *contaminated* ifike Serikalini.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Moja; *sample* chupa mbili za nusu lita ziko Bihamamulo; moja anayo *Extension Officer* wa Kata ya Kabindi, moja anayo Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika.

Mbili; naamini na ninadhani, utaniongoza ni kazi ya mnyororo wa Serikali kuhakikisha zinatoka huko zinakuja huku kwa sababu ziko mikononi (hasa hiyo moja iko kwa Afisa wa Kilimo), lakini jambo la tatu narudia na utatazama *Hansard*. Nimesema *hypothesis* ni tatu, moja; kukosa *consistencyya* kupeleka dawa ndiyo kunasababisha wadudu wasiwe, mbili, dawa inayoletwa na Bodi ya Pamba haiui kwa sababu wananchi wanasema ukienda kwenye maduka binafsi wanayopata inaua. Tatu, kuna *hypothesis* kwamba wakulima hawatumii vizuri ndiyo maana walimleta Afisa Ugani wakamthibitishia na yeze yupo aletwe pamoja na *sample*. Maana ya *hypothesis* ni kwamba hujajibu mnatakiwa kufanya kazi mjibu kipi ndiyo kinasababisha. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Sawa. Hizi *hypothesis* ndiyo zinaenda hivyo lakini humu ndani tuwe na uhakika ulichokisema tu wewe. Sasa kama unaona huyo Mtendaji ambaye ulimkabidhi wewe ni mnyororo wako wewe mwenywewe.

Tusaidie tu! Wewe tuletee, wewe ndiye Mbunge uliyesema humu siyo Mtendaji. Haya tuletee. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa jinsi ulivyoliweka jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wetu kama Serikali kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri tunachotaka kukifanya, kwanza tunamshukuru Mheshimiwa kwa taarifa kwa sababu hatukuwa na hiyo taarifa ametupa taarifa ya msingi, tunamshukuru na tunampongeza sana. hilo la kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tunashukuru pia ametuambia *source* ya hiyo dawa na mtu aliyehifadhi ni nani na hasa huyo wa Serikali ambaye ametuambia. Haitupi shida, tutaomba tu wewe utatuongoza kwa Kanuni zako huko mbele lakini sisi kwa sababu Serikali yote iko hapa, tutawasiliana na Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI ili atusaidie huyo mwenye hiyo dawa ambaye yuko ndani ya Serikali atuletee na lengo la Waziri wa Kilimo ni kutaka kujithibitishia. Kama kuna mtu amefanya vurugu, kwa kweli kama Bodi ya Pamba ama kuna mtu yejote au *dealer* amefanya hiyo vurugu ndani ya Serikali ni lazima ndani ya Serikali tuna wajibu wa kusimamia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuko pamoja na Kiti chako lakini tunamshukuru Mbunge aliyetoa taarifa. Tunamshukuru Waziri kwa kuamua kulibeba jambo hili kwa haraka. Kwa hiyo wote tupo pamoja na tunaongea lugha moja na tatalishughulikia ipasavyo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

Uamuzi wangu kwa uharaka huo, lichukue mkondo wa Kiserikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu kama *coordinator* wa shughuli za Serikali waweze kuipata hiyo *sample* kwa

taratibu za Kiserikali. Nadhani tutakuwa tumekaa vizuri. Lini, nadhani mapema iwezekanavyo kwa sababu ni kitu ambacho tungelipenda tujue na kisiendelee zaidi kama kweli kipo. Tumeelewana?

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote nianze kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo amekuwa akifanya shughuli zake ndani ya Bunge na nje ya Bunge na niwapongeze Mawaziri wanaomsaidia katika ofisi yake, Mheshimiwa Jenista Mhagama na niseme tu Mheshimiwa Jenista lile tatizo la maji Nzega kule mpaka leo mambo muswano. Kwa hiyo, nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Antony Mavunde kwa kazi anazofanya na *commitment* anayoonesha na namna ambavyo amekuwa akijituma katika kufanya shuguli zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mweiti, nianze kwa maneno yafuatayo. Ukitazama ngao yetu iliyoko mbele yetu pale ina maneno mawili, uhuru na umoja. Mwaka 1957 wazee wetu wakiwa pamoja na kijana wao wakati huo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere walipoanza harakati za kutafuta uhuru kuititia Chama cha *TANU* waliwaunganisha Watanzania wote kwa makabila yao, dini zao ili kupata umoja ambao utafikia dhamira ya wao kupata uhuru wa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo yanaendelea katika nchi yetu ambayo yanaashiria kuanza kuwepo kwa migawanyiko katika Taifa letu. Mambo haya tukiendelea kuyatazama kwa macho hayaleti taswira njema huko mbele na wala hayataweza kulifanya Taifa hili kuendelea kuwa Taifa moja na kupambana na adui mkubwa ambaye ni umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanatokea matukio ya

kusikitisha katika nchi yetu ambayo ukitazama huoni *any concern* ya *deliberate effort* ambayo itawajengea Watanzania imani kwamba, hata mimi mdogo nikikumbwa na zahma basi yupo anayenilinda. Yamekuwa yakinoteka matukio mengi yakikosa majibu katika nchi yetu, lipo tukio la kijana anaitwa Allan ambaye ni muuza machungwa pale Mbeya. Mimi ningeliomba Serikali kwa heshima kabisa, matukio ya namna hii yakiendelea kujengeka katika nchi yetu na ku-*develop culture* ya *impunityyana-destort peace* iliopo katika Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana huyu amekufa. Ripoti ya Daktari Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya Mbeya imesema kwamba kijana huyu kafariki kwa majeraha ya ndani ya mwili wake. Familia yake imesema waliomuua, waliompiga ni Jeshi la Polisi. *RPC* wa Mbeya akasema hawahusiki! Matokeo yake nini, Serikali imeenda kutoa rambirambi ya shillingi 200,000. *Is that the reason?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya namna hii yameendelea kuwepo, mimi ningeliomba Wizara ya Mambo ya Ndani na Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali wakati ina-*wind up budget* ya Waziri Mkuu waagize kuundwa kwa *official independent organ* ifanye *investigation* ya haya mambo. Hatuwezi kuacha *this culture of impunity* inaendelea katika nchi yetu, *it is very sad* na ina-*destort image*. Hii ndiyo inatumika na watu wasiopenda nchi yetu kuendelea kuharibu heshima ya Taifa letu. Hili ni jambo ambalo ninaiomba Serikali ichukue hatua katika jambo hili. Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu katika hotuba yake ameellezea kukua kwa uchumi. Rais anafanya *effort* nyingi ku-*encourage* watu kujenga viwanda katika nchi yetu, kama hatutaamua *deliberate* kuwa na *specialisation* hatuwezi ku-*specialise* katika kila jambo, 70% ya nchi yetu iko katika sekta ya kilimo. Nitoe mfano, mwaka 2015/2016 uzalishaji wa zao la korosho na Serikali imesema kilimo kimekua kwa asilimia 3.6. Uzalishaji wa korosho ulikuwa tani 265,000 msimu huu tunazungumzia

tani 313,000 *inputs* ambazo Serikali iliingiza, *investiment* ya Serikali ni shilingi bilioni 28 kwenye zao la korosho. Msimu uliopita mapato tuliyoyapata ni bilioni 872. Serikali ilivyoamua ku-*invest 28 billion* mapato ya korosho sasa hivi yatakwenda *1.18 trillion shillings*. Waziri wa Fedha haoni hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it is not a rocket science*, narudia. Kilimo tulizungumzia *NFRA*, Wizara imeomba *86 billion shillings*, inapewa *15 billion shillings*. Mwaka huu tunazalisha *metric tones 900,000* mahitaji yetu ni *metric tones 5.9* hii excess inaenda wapi? Tutafunga mipaka ili tu-*create artificial control* ya *inflation* tuseme mfumuko wa bei asilimia nne, tunawatia umaskini wakulima. *We have to be serious. Inputs* kwa ajili ya pamba Wizara imeomba *10 billion* Serikali imempa *three billion*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wale wadudu wanaokula mahindi wanaitwa viwavijeshi wameshaanza kushambulia baadhi ya maeneo. Kwa nini, kwa sababu, fedha zilizombwa na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya *inputs* hawajapata *as per the requirements. What do we want?* Tunataka nini? Siyo muujiza, tukijenga viwanda kama asilimia 70 ya Watanzania ni maskini, hawana uwezo wa kununua bidhaa za viwanda hivyo, viwanda hivi vitakufa tu na wala siyo muujiza. Nataka niiombe Serikali, nimesoma mpango wa Dkt. Mpango, nitakuja kuongea wakati wa bajeti, *it is typical cosmetic measures*. Hakuna *serious fiscal measure* zinazotengenezwa na Wizara ya Fedha kuweza ku-stimulate sekta ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaagiza *crude oil* karibu tani 600,000. Nini mpango wetu wa kuwekea kwenye mazao ya alizeti, ili tuweze kujitosheleza mafuta? Kama hatutaamua, nitoe mfano wa mifugo. Kwenye hotuba ya Waziri Mkuu amezungumzia suala la chapa na mimi nimpongeze Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega kwa mara ya kwanza kajua, zamani ng'ombe alikuwa anaita mnyama siku hizi anaita mifugo, kawajua na ng'ombe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze ku-*improve mazao*

yanayotokana na mifugo ni lazima tuwekeze kwenye *proper breeding programs*. Ng'ombe wetu hawajafanyiwa *breeding* toka mwaka 1982, hakuna *investments*, leo mzalishaji wa maziwa anayezalisha maziwa, mfano mtu kama *ASAS, cost of production* ya ASAS ni asilimia 18 juu kuliko mzalishaji anayezalisha maziwa Kenya. Kwa nini? Ni kwa sababu ya mfumo wetu wa kodi. Nataka nijiulize Serikalini kwa nini mnahitaji VAT kwenye vifungashio nya maziwa? *Why?*

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe, muda ndio huo.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, zimeisha dakika? Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Balozi Adadi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana ya hotuba ya Waziri Mkuu. Hotuba ambayo ni hotuba mama, hotuba ambayo ina-*covershughuli* zote zile za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napongeza sana juhudhi ambazo anafanya Mheshimiwa Rais, tumeona maendeleo mbalimbali. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, siyo siri tumemuona jinsi ambavyo anazunguka nchi nzima kwa ajili ya kuletea maendeleo nchi yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana na Mawaziri wote kwa shughuli ambazo wanazifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona miradi mikubwa, tumeona *SGR* ya reli ya kati ikianza, tumeona ufufuaji wa *ATCL*, tumeona *flyovers*, tumeona ujenzi wa vyanzo vipya nya umeme, tumeona miradi ya Mkulazi ambayo ni maendeleo makubwa sana kwa kilimo na pia tumeona bomba la mafuta la kutoka kule Hoima mpaka Mkoani Tanga. Juhudi

ambazo nazipongeza kwa hii miradi mikubwa, hii inaongeza uchumi kupanda ndiyo maana kwenye hotuba ya Waziri Mkuu anaonesha kuna viashiria vikubwa vyta kupanda uchumi wetu kwa asilimia 6.8. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bomba la mafuta la Tanga tunaamini kabisa kwamba, shughuli hiyo imeshaanza na kwa kweli, itatusaidia sana Mkoa wa Tanga. Aidha, suala la ujenzi wa reli ya Tanga, mpaka sasa hivi ninafahamu kwamba upembuzi yakinifu umemalizika na juhudzi zinafanyika za kuweza kuingia kwenye *PPP*, lakini tunaiomba Serikali Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala hili ulipe kipaumbele. Najua upembuzi yakinifu wa Tanga – Arusha umemalizika, lakini upembuzi yakinifu wa Arusha – Musoma ndio unaendelea. Sasa ni vizuri tukaanza kutangaza hii *tender* ili ianze kushughulikiwa. Naamini kabisa wapo wawekezaji ambaao watajitokeza kama alivyojitokeza juzi kwenye ujenzi wa viwanda vyta madawa. Kwa hiyo, naomba suala hili lipewe umuhimu kwa sababu, wenzetu majirani pale Kenya *SGR* ambayo inakuja mpaka bandarini kwao Mombasa, wanatupa changamoto kubwa sana kwa hiyo, ningeshukuru na hii iende sambamba na *SGR* ya reli ya katii. (*Makofii*)

Miradi mikubwa imeshughulikiwa kwa kiwango kikubwa sana, lakini sasa naona kwamba msisitizo mkubwa twende vijijini. Naamini kabisa tutakapokwenda vijijini tutapunguza umaskini ambaao uko mwingi kwenye vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo; tumeona kabisa juhudzi ambazo zimefanyika kwenye suala la korosho, lakini hatujaona juhudzi ambazo zinafanyika kuinua zao la katani. Sasa hivi zao la katani liko bei kubwa sana kwenye soko la dunia. Ni hivi majuzi tu Waziri wa Kilimo amekuja Tanga kuanza kufufua, lakini ningeshukuru kama Waziri Mkuu utaingilia katii na kujaribu kuona totalifanya vipi soko la katani liweze kukua. Katani ndiyo imetukuza Tanga, miradi mingi sana imetokana na katani, sasa katani inadharaulika, hajapewa ule umuhimu ambaao unatakiwa. Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo naamini kabisa suala hili mtalipa umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji; maji ni muhimu sana, sasa hivi tunashindwa kupata Wawekezaji Muheza pale kwa sababu ya maji, tuna tatizo kubwa sana la maji. Ninamshukuru sana Waziri wa Maji, tumepata mradi wa kutoa maji Pongwe, mradi wa kutoa maji Pongwe unakwenda vizuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini mradi huo ambao tuliutegemea umalizike mwezi ujao mwishoni umechelewa kwa mwezi mmoja na umechelewa kwa sababu ya ujenzi wa tenki ambao utaanza baada ya wiki mbili zijazo, lakini inanipa wasiwasi kwenye mifumo ya kufumua Mji wa Muheza ambao tulitengewa bilioni tano, sasa bado hatujaruhusiwa kutangaza hili suala. Ningemuomba Waziri wa Maji aliangalie ili utakapofika wakati basi mradi huu usiweze kuchelewa kwa sabau, maji yatakapotoka kule ni lazima tufumue hii mifumo ya Mjini Muheza. Hata hivyo namshukuru sana kwa juhudzi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la miradi mikubwa 17 ambalo tumeambiwa kila siku linakwama shauri ya *financial agreement* hajasainiwa. Miradi hii 17 itakapoanza itasaidia sana tatizo la maji kwenye nchi hii, lakini kila siku tunaambiwa *financial agreement*. Najua kuna *technical ground* iliyoko pale, naamini kabisa kwamba, Waziri wa Fedha yuko hapa na Waziri wa Maji yuko hapa, suala hilo mtaweba kulitatua kabla ya bajeti ya Wizara ya Maji hajisasomwa. Nitashukuru sana na pia kwenye bajeti ya maji itakaposomwa basi ile shilingi 50 ambayo tulipigia kelele sana wakati uliopita nategemea itakuwepo kwenye bajeti ya Waziri wa Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya, tunajenga Hospitali ya Wilaya ya Muheza na hapa nimeona kwamba, kuna hospitali zitajengwa 67 nchi nzima. Namtegemea Waziri wa Afya na au TAMISEMI, Waziri wa TAMISEMI naamini kama tumeonesha juhudzi basi naamini hizo bilioni 1.5 na Muheza tutapewa ili tuweze kukamilisha hii hospitali yetu ya Wilaya. Lakini pamoja na hayo tunawashukuru sana TAMISEMI na Waziri wa Afya kwa kutupa milioni 400 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya ambacho tumekianza kule Mkuzi. Tunategemea pia kujenga vituo vingine vitano vya afya

ambavyo ambapo juhudzi za wananchi wameanza kule Muhamba, wameanza kule Ngomeni, wameanza kule Tongwe, wamenza Potwe na wamenza Ubwari ambachoz tunaendelea kukiboresha na wameanza kule maeneo ya Amani - Msarai, zote hizo wameshaanza kuweka misingi, naamini kwamba, tutakapofika juu basi Serikali itakuja iweke mkono wake pale.

Suala *REA* Muheza ina Kata nyingi sana, kata 37 kwa hiyo, nina vijiji karibu 135 ambavyo vingi bado havijapata umeme. *REA* imeanza kuingia, survey imefanyika kwa vijiji vingi, lakini kazi ilikuwa haijaanza ni wiki iliyopita tu Waziri alipopita pale, ambapo ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani kwamba baada ya kufika basi kazi zimeanza, nguzo zimeanza kuletwa, lakini ninachoomba ni suala hili lifanyike kwa haraka kwa sababu vijiji vyangu vingi havijapata umeme. Survey ilipofanyika tu kwenye vile vijiji wananchi wenyewe wameanza kufurahi, wameanza kushukuru. Mimi nimekula mbuzi na kuku wengi tu wanani, lakini bado hawajapata umeme, lakini mbuzi hao wenu nimewala pamoja na kuku wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la barabara, barabara yangu ya Amani na Muheza kilometra 36 ipo kwenye bajeti shilingi bilioni tatu, lakini mpaka sasa hivi bado siaona dalili zozote za *TANROADS* kuja kuanza kuishughulikia. Ningemba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Ujenzi basi suala hili muliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la Watendaji wa Vijiji na madereva ambao walimaliza darasa la saba, kwa kweli inasikitisha. Sisi tumeendeshwa na madereva wa darasa la saba kwa miaka yote, miaka mingi na wamefanya kazi kwa bidii. Juzi wakati hilo zoezi linafanyika tulikuwa tuna ziara ya kwenda wapi, naambiwa magari yako pale Halmashauri madereva hawapo wamesimamishwa, nini? darasa la saba. Mheshimiwa Waziri Mkuu tuwe na imani, wamefanya wameendesha gari bila ajali zozote zile miaka yote, wanakuja mwisho wanakaribia kustaafu tunawafukuza. Tuwe na ubinadamu tuangalie na hawa watu ningeshauri

kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu basi warudishwe waendelee kufanya kazi kwa miaka yao ambayo imebaki. Wakati wanaajiriwa watu hawa wakati huo darasa la saba lilikuwa lina umuhimu wake, lakini sasa hivi wasomi wengi! Lakini hatuwezi kuwa tumewapata wasomi basi tuwaache wale. Naomba kabisa Serikali iangalie na ione namna ya kurekebisha. (*Makofii*)

Baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono na ninakushukuru sana kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru kwa michango yenu, kwa asubuhi ya leo tukomee hapo. Niwataje tu Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa wa mwanzo kuchangia jioni tutakaporejea. Kwanza atakuwa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, atafuatwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani kwa jina maarufu Profesa Maji Marefu, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka na Mheshimiwa Mary Chatanda. Tutaanza na hao, halafu *tuta-balance* kutenda haki kwa Kambi zote humu ndani, tunaenda vizuri tu wala msiwe na wasiwasi.

Waheshimiwa Wabunge, narudia ni dakika 10, lakini nilisema mapema, ili muwe wengi mnaweza mkagawana dakika tano - tano ni hiyari ya moyo, siwezi kuwalazimisha, lakini uwiano ni ule ule *it doesn't change anything*. Ndiyo maana nasema tutambue hilo, siwezi kuminya orodha ya wachangiaji natenda haki ndani ya muda. Kidogo tunapopoteza tunafidia kwa wale ambao wanatunza muda na kwa hoja *straight to the point*.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Wakati wa kusitisha shughuli za Bunge nilitaja majina ya Waheshimiwa Wabunge tutakaoanza nao. Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua akifuatiwa na Mheshimiwa Profesa Maji Marefu. Mheshimiwa Chuachua, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Marry Chatanda, Mheshimiwa Ally Salehe Ally.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Nimejipanga kuchangia katika eneo moja tu, lakini kumetokezea kitu ambacho itabidi nikiseme ambacho kimetokezea jana usiku na ambacho kinahusiana na hali ya usalama na utata utata na matatizo haya ya kukamatana kamatana bila ya kujitambulisha wanaokamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana usiku huko Pemba Wete wamekamatwa vijana sita Sued Nassoro, Khamis Abdallah, Abdallah Chumu, Juma Kombo, Said Shomari na Uledi Khamisi, wamechukuliwa na watu ambao wamekataa kujitambulisha lakini wananchi kwa bahati waliziona nambari zao za gari wakachukua na leo asubuhi tulipoanza kuulizia *RPC* wa Kaskazini na Kusini wote wanassema hawako mikononi mwao. Kwa hivyo, wamekamatwa na watu wasioeleweka, tunaongezea ule msamiati wa watu wasiojulika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu hasa mimi nitabakia katika sukari. Nataka kutazama sukari *bigger picture*. Sukari kwa maana ya kwamba ni kilio cha Wazanzibari, ni mkusanyiko wa vilio vingi kinaji-*manifest* katika sukari; kwa maana kwamba kutokana na matatizo, mivutano ya kisiasa au sekesekere la kisiasa ambalo tumekuwa tukiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu pia kumekuwa na tatizo la kiuchumi ndani ya Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar au wafanyabiashara wa Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wa Zanzibar wanafikiri kwamba hii ina ukandamizaji, ina unyanyasaji, ina kuipendelea Bara zaidi kuliko Zanzibar lakini pia inaleta sintofahamu ambayo watu wengi wanafikiri inafanywa makusudi ili kuitia Zanzibar kitanzi cha uchumi. Kwa sababu yapo mambo mengine hayana *logic* lakini yamekuwa yakitokezea, na watu wanauliza au kwa sababu sisi ni Visiwa. Kwa sababu yako mambo mpaka tunafika tunajiuliza au sisi ni visiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi imekuja hii zana ambayo inaelezwa hapa ya kutojitosheleza; kwamba ikiwa wewe hujitoshelezi katika bidhaa usiuze kwingine, bila kujali uhuru wa soko, bila kujali upana wa soko. Sasa nafikiri hii ni *principlembaya* haifai kuendelezwa na inapaswa ikomeshwe mara moja. Maana yake nini, maana yake ni kwamba kama leo unawaambia Wazanzibari hawawezi kuuza sukari kwa sababu mahitaji yao ni tani 17,000 wanazalisha tani 8,000 maana yake kesho utawazuia wasiuze viazi, kesho kutwa utawazuia wasiuze nguo, kesho kutwa utawazuia wasiuze kingine kwa sababu tu mahitaji yao ya ndani hayajajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hii ni *principlembaya* sana, tunakwenda katika hatua isiyokuwa na msingi kabisa. Tunafanya *protectionism* ya viwanda au kiwanda cha sukari dhidi ya ndugu yako au kwa sababu sisi ni Kisiwa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana inayoenezwa ni kwamba pengine Wazanzibari watapenyeza sukari kutoka nje. Kwani hivi sasa sukari haiingii kutoka Malawi, kwani hivi sasa sukari haiingii kutoka kwingine inayointingia kwenye soko la Tanzania ambalo lina *starve?* Soko la Tanzania hivi sasa linahitaji tani laki tatu na hamsini kwa mwaka. Kila mtu anajua uzalishaji una upungufu wa tani laki moja nzima, sukari inatoka nje.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sukari ikipitia Zanzibar, hata ikiwa inatoka nje inapita Zanzibar inakuja katika soko la Muungano, kwa nini iwe vibaya kwamba inatoka Zanzibar wakati pia soko la Muungano linaagiza sukari kutoka nje ili kujaza lile pengo? Au kwa sababu sisi ni Kisiwa kwa maana nyingine tunahukumiwa kwa vitu ambavyo kwa kusema kweli vinatumiza sana moyoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatukuungana kwa ajili ya kugawana umaskini tu, tumeungana katika kugawana pia na neema. Sasa kama tunazuiana tusigawane neema, mtu anajulizwa Muungano huu una faida gani kwa Wazanzibari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ulikuwa unatarajia nini kuungana na Zanzibar ambayo ina eneo la kilomita elfu mbili za mraba *vis-a-vis* nchi ambayo ina kilomita elfu tisa za mraba? Ulitarajia nini unaungana na Zanzibar ambayo watu wake sasa hivi ni milioni moja na laki tano *vis-a-vis* milioni hamsini na tano? Ulitarajia nini kuungana na Zanzibar ambapo upande mmoja una soko kubwa na upande mmoja una soko ndogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulitarajia Zanzibar a-survive viyi kibiashara? Ulimfikiria Zanzibar afanye nini aingie katika soko? Kama unazuia Zanzibar asiingie kwenye soko la Tanzania Bara ina maana unamzuia Zanzibar asiingie kwenye soko la Afrika Mashariki. *Otherwise* tunaingia katika matatizo ambayo kusema kweli kama hatukuyapatia suluhu basi utakuwa mgogoro mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Zanzibar tulizuiliwa Zantel isiingie Tanzania Bara kwa muda wa miaka mitano. *That was the first mobile company, the biggest, ikafa.* Kwa maana sasa hivi ipo taabani imeshanunuliwa na *Tigo*. Hata hivyo, hivi sasa bidhaa nyingine zinazuiliwa, kwa mfano ukitoka Zanzibar kuna maji ya *drop* yanazuiliwa kuja huku. Kwa muda mrefu maziwa ya Bakhresa yalizuiwa kuja Tanzania Bara. Kuna njia inaonekana kuna watu wanafanya makusudi ili kui-starve Zanzibar kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nauliza hivi hatujui kwamba Zanzibar kwa udogo wake inahitaji ipate mahali ipate soko? Itafika lini Zanzibar kwa udogo wake itengeneze magari ya kujitosheleza halafu iuze nje, itengeneze TV za kutosheleza halafu iuze nje? *Let use our brain.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wawili watatu hapa, mmojawapo Mheshimiwa Kitwanga jana na leo amekuja na fikra mpya, tufikiri upya, tusifikiri kizamani, tufikiri kisasa, kwa sababu kama hatujatengeneza mazingira ya Zanzibar kusonga kiuchumi unatengeneza bomu lingine. Bomu ambalo likilipuka linaweza kuwa kubwa zaidi kuliko bomu hili la kisisasa ambapo pengine watu wakipewa vyeo wananyamaza, watu wakibebelezwa wananyamaza lakini watu wakiwa na njaa watashindwa kunyamaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa biashara nyngi Zanzibar zimefungwa kwa sababu ya hii *double taxation* ambayo mara nyngi inatokezea ikija huku. Imesemwa, imesemwa, imesemwa, lakini mpaka hivi leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri ikiwa kwamba tumeungana sisi kwa mambo matatu ambayo yote nafikiri yana shaka katika Muungano huu; la kwanza tumeungana kama vile tunatafutana. Kuna habari nyngi mara nyngi zinazungumzwa kuwa Zanzibar ni kichochcho. Hivi kichochoro Zanzibar tu, hakuna mipaka ya Sirari, hakuna mipaka ya Horohoro, hakuna mipaka mingine yote ya Tanzania? Hivi bidhaa zinazopitishwa Zanzibar kuja huku ndiyo ukikusanya zote pamoja itakuwa ndiyo zinapita zile ambazo zinapita katika mipaka yote ya Tanzania? Hilo moja, lakini la pili kwani... (*Makofii*)

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa kaa.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mbunge anayezungumza, kwa kanuni ya 68(8), hayo masuala anayoyazungumza ni ya kihistoria. Mimi mwenye dhamana ya biashara na Waziri Mwenzangu upande wa Zanzibar, tulishayakalia, pamoja na mambo anayoyazungumza lilikuwepo suala la viwango, tumeoanisha viwango kati ya viwango vya ZBS na TBS yote tuweze kufanya kazi. Hata hivyo yule nayevunja sheria, wa Sirari atashughulikiwa, wa Namanga wa Namanga; lakini kama lilijitokeza mtu kupitia Zanzibar na wa Zanzibar atashughulikiwa na mamlaka za Zanzibar zinalalamikia magendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo taarifa ninayotaka kumpa ni kwamba tusilikuze hili jambo, Mawaziri wa pande mbili wanaongea na tunapoongea tunakwenda *public* watu wanatuona. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Nafirikiri *It is very dismissible amechukua very minor issue*, mimi ninazungumzia sukari katika picha kubwa, lakini Waziri anajikita katika swali moja ambalo kwa miaka hamsini ya Muungano halijapatiwa suluhu. Ikiwa mpaka leo Mawaziri wanazungumza miaka hamsini na tano baada ya Muungano kwa maana gani? Bora Waziri angekaa tu akasubiri wakati wako ajibu kwa sababu hapo hajajibu kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nafikiri lazima tuwe na mfano wa kuonesha kama uchumi wa Zanzibar haukuwa *supported* kama vile kwa mfano EU walipoungana na nchi maskini Portugal na Spain walitengeneza mpango maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize leo hii hapa Serikali ya Muungano imetengeneza mazingira gani ya kiuchumi ya Zanzibar? Mtu ataniambia Zanzibar kuna Serikali yake. Serikali gani ambayo haina taratibu za kupata mikopo, lazima ipite kwenye Serikali ya Muungano, Serikali gani ambayo sera zake kuu zinafuata sera za nchi, kama ni sera za kifedha, kama ni sera nyinginezo? Kwa hivyo nyingine si

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kweli kwamba Serikali ya Muungano imeleta tatizo hili, tatizo hili lipo mpaka leo kila siku linaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tukubali tu kwamba Zanzibar ina *potential...* (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza.

MWENYEKITI: Hapana. Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwangalia kidogo mwenzangu mmoja Mheshimiwa mmoja hapo nije alikuwa ananiita anasema ninyi CCM mmekuwa timu pongezi kazi yenu kupongeza tu. Sasa nikamwambia mimi kwa upande wangu Tabora au Tabora Mjini nina mambo mengi tu ya kuipongeza Serikali. Kwa hiyo hata kama anaita timu pongezi tutaendelea kuwa tunatoa pongezi kwa yale mambo mazuri ambayo yanafanywa chini ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Tabora tumebahatika tuna mradi mkubwa wa maji wa zaidi ya bilioni 600 ambao sasa unaendelea; Kiwanja chetu cha ndege kinaboreshwu; alisimama Mheshimiwa Ntimizi hapa aliongelea kile kipande Chaya ambacho kimebaki katika barabara ya kuunganisha kuanzia Itigi mpaka Tabora kwa lami, Mkandarasi yuko anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo sisi Tabora zao la tumbaku kama ambavyo wamekuwa wakiongea wenzangu ni zao la kimkakati. Tulikuwa na matatizo sana ya tumbaku kununuliwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshakuja Tabora mara nyingi na matunda yake yanaonekana, tumbaku nyingi imekwishanunuliwa, kwa hiyo naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo inatimiza ahadi zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo changamoto kwenye suala la afya. Kwenye suala la afya sisi pale Tabora Hospitali yetu ya Rufaa ya Kitete, Madaktari Bingwa yupo mmoja tu mpaka sasa hivi na tunahitaji Madaktari Bingwa tisa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kutupatia Madaktari Bingwa ili hospitali ile iweze kuwa inajitosheleza kwa ajili wagonjwa ambao wanakwenda rufaa Bugando, Muhimbili na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tangazo pia lilitolewa Bungeni hapa kuhusu madawa au maduka ya madawa ambayo yanazunguka hospitali zetu na kwamba yangefuatiliwa na pengine kuondolewa kabisa. Kwa mfano pale Tabora Hospitali ya Kitete, imezungukwa na maduka ya dawa ambayo yenewe dawa karibu zote unapata na imekuwa ni kawaida hata dawa ambazo ni za kawaida wagonjwa wamekuwa hawazipati kwenye hospitali, lakini wanapokwenda pale nje wanapata dawa zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajiuliza zile dawa je zinatoka mle ndani au namna gani kwa sababu wale wanao miliki zile dawa au yale maduka ya dawa wengine ni wauguzi na wengine ni madaktari. Sasa naiomba Serikali lile tamko la kufuutilia ule mlundikano wa haya maduka ya dawa yanayozunguka hospitali zetu wafuutililie isije ikawa ndicho chanzo cha dawa kupotea kutoka mahospitali yetu na kupelekwa kwenye *pharmacyambazo* zipo jirani na hospitali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la pembejeo. Tabora wengi ni wakulima kama ilivyo sehemu nyingine, lakini

mara nyngi pembejeohaziendi kwa wakati. Kwa mfano, mwaka jana wakulima walipata mbolea katika kipindi ambacho ilikuwa sasa na mazao yameshakuwa kiasi ambacho mengine yalishakuwa yameharibika na hata ilipokuwa imekuja mbolea haikuwa na faida kwa wakulima wengi. Kwa hiyo, naiomba Serikali yetu sikivu kuangalia suala hili la pembejeo za kilimo, ziwe zinawafikia wakulima kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi imekuwa ni changamoto nadhani kwa nchi nzima katika sehemu mbalimbali. Hata hivyo, kwa Tabora kwa sababu ilisemekana au ile Tume ambayo ilipita kwa ajili ya kuchunguza migogoro ile bado hatujapata jibu la migogoro ya ardhi hasa kwa Tabora Mjini. Tabora Mjini imezungukwa na Kambi za Jeshi na migogoro mingi ni katii ya wananchi na jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuptitia Wizara ya Ardhi iliahidi kwamba itaongea na Wizara ya Ulinzi ili kuangalia ni nani hasa alivamia eneo la mwenzake; kwa sababu wananchi wanadai kwa muda mrefu kwamba maeneo hayo ni ya kwao miaka na miaka na Jeshi la Wananchi wanasema kwamba maeneo yale ni yao. Sasa kwa sababu Serikali ilishaamua muda kwamba itangalia upya ramani, hajibibiwa mpaka sasa hivi na mgogoro ule bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naihimiza Serikali kwamba ili kuondoa matatizo ambayo sasa yamekuwa sugu kwenye kata mbalimbali za Jimbo la Tabora Mjini na maeneo mengine, basi wawahishe ule mchakato wa kuangalia upya ramani ili waweze kuweka alama ambazo zitaepusha migogoro ambayo si ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria. Tulifanya ziara juzi juzi katika Mkoa wa Shinyanga, tulikwenda Mikoa ya Simiyu, Geita na tulikutana na changamoto nyngi. Ukiangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 62 kuna suala la kesi karibu asilimia

96.3 ambazo zimekwisha, kwa maana kwamba mashauri yake yalishamalizika, lakini uwiano huu ni kwa nchi nzima. Sasa kama ni uwiano kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni uwiano kwa nchi nzima kuna sehemu zingine ambazo bado kuna mlundikano wa kesi kutokana na uhaba wa Majaji pia na Mahakimu wa kawaida. Kwa mfano sehemu hizi nilizozitaja; ukichukulia Shinyanga Mjini wanatakiwa Majaji sita lakini kuna Majaji wawili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Simiyu yuko Hakimu mmoja ambaye anashindwa kuzimudu kesi zote kwa sababu kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu. Sasa kesi nyingi zinarundikana kwa sababu ya upungufu wa Mahakimu na Majaji pia. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kufuatilia hiyo ili hii *figure* iliyotolewa hapa ya asilimia 96.3 iendane na wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna suala la wenzetu hawa ambao wana matatizo ya uathirika wa UKIMWI kama alivyozungumza mwenzangu mmoja hapa. Nadhani tuwape upendeleo katika pato letu lile la ndani angalau asilimia moja kwenye zile *percentage* ambazo ni *own source* katika hal mashauri waweze kuchangiwa hawa wenzetu ili kuwawezesha kumudu maisha; kwa sababu wako waathirika ambao kwa kweli bila kusaidiwa hawawezi kujisaidia wenyewe. Nina imani Serikali yangu ni sikivu inaweza ikaliangalia hilo na ikalifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Stephen Ngonyani, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Chuachua ajiandae.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja

iliyoletwa hapa mezani na aliyoyaongea yote Mheshimiwa Waziri Mkuu nimpongeze sana kwa kazi nzuri wanayoifanya Serikali hii ya Awamu ya Tano. Vile vile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba kumbe inawezekana. Amefanya mambo makubwa na yameanza kuonekana ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania. Mungu ambariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa suala la reli. Reli ni kichochea kikubwa sana cha uchumi Tanzania, lakini niombe, sitashika shilingi tena kama mwaka jana; mwaka jana nilishika shilingi kwa ajili ya reli ya kutoka Tanga-Arusha – Musoma ila nataka Waziri husika katika suala la reli ahakikishe safari hii hakuna haja ya kushikiana shilingi atuambie; tunahitaji *standard gauge* lakini huwezi kujenga zote kwa wakati mmoja, lakini ni namna gani reli ya kutoka Tanga kupitia Kilimanjaro, Arusha na kwenda Musoma itaanza kazi ili na sisi mizigo yote ambayo ilikuwa inatoka katika bandari ya Tanga ifanye kazi nzuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Bomba la Mafuta, tumshukuru sana Rais. Bomba la Mafuta lingeweza kwenda mkoa wowote lakini limeletwa Tanga kutoka Uganda. Naomba sana Serikali hii sikivu wajaribu sana Watanzania wapate kazi pale, ule mtaji wa kwamba Watanzania wanalishangilia bomba la mafuta wanaokuja kufanya kazi ni Wakenya uwe sasa mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kawaida ya watu wanatengeneza biashara kama hizi vijana wa Kitanzania hasa wa Mkoa wa Tanga na jirani na wanakopita Bomba la Mafuta hata kuchekecha zege watolewe watu Kenya, hata kushika lile toroli mtu atoke Kenya! Safari hii haiwezekani, wakija kwetu watu wa namna hiyo tutawafukuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu msikivu sana, kuna Watanzania waliamua kujenga shule za kata; shule za kata zimejengwa maabara nyingi na Watanzania wenywewe kwa nguvu zao wenywewe. Naomba sana Serikali, kwa sababu tunataka watoto wetu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wasome tuangalie ni mazingira gani watatengewa fedha, zile sehemu zote ambazo wananchi walitumia nguvu kubwa sana kujenga maabara za kata katika shule za sekondari watenge fedha ambazo watamalizia nguvu za wananchi wenyewe walioamua kujitolea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nimeona niliseme kwa sababu wananchi walihamua wenyewe kujenga shule za kata lakini mpaka leo hii kuna magofu ya ajabu sana katika shule za kata, hakuna mahali ambapo utaenda utakuta maabara, na vijana wengi lazima waingie kwenye maabara kujifunza sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *REA* ni suala la msingi sana katika Tanzania. Tunategemea sana kwamba umeme utakwenda vijiji, lakini cha kusikitisha utashangaa kuona *REA* tulipewa taarifa kwamba katika kila wilaya kutakuwa na vijiji ambavyo vitapata *REA* na tukashukuru sana. Hata hivyo, hatua ya mwisho unakuja kuambiwa vijiji vile vimekatwa, wananchi wanaanza kulalamika kwamba Waheshimiwa Wabunge hatuwatendei haki, kwa nini vijiji fulani vimekatwa na ni kwa nini mlituambia kwamba vijiji hivi vitapata *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye simu yangu hapa, ukinunua bando unaambiwa umekatwa shilingi fulani za kwenda kwenye *REA*. Ukiwaliza watu wanaosimama kujenga au waliopata *contract* za kusambaza umeme wanakwambia hatujalipwa. Sasa najiuliza hii hela inayokatwa kwenye simu hii ambayo inaonesha kabisa inaenda kwenye *REA*, sasa inakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri husika, Mheshimiwa Waziri Mkuu vijana wake wamekuja Jimboni kwangu Mawaziri zaidi ya kumi (10) na nawashukuru sana wamenifanya kazi nzuri sana. Wamekuja wametoa fedha nyingi sana; na kwa sababu katika Tanzania Korogwe ni wilaya ya kuigwa kwa sababu tukipewa hela chache tunafanya kazi kubwa na chenchi inabaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mziangalie zile wilaya ambazo zina uchungu na fedha ya Serikali kwa macho yote ili mtusaidie kutengeneza zile sehemu ambazo zimeanza. Leo tunajenga kule vituo vya afya, kuna vituo vya afya vizuri na kuna shule za sekondari nzuri ambazo hata Waziri wa Elimu, Waziri wa Nishati, Waziri wa Ardhi, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Maji, Mawaziri karibu wote wamekuja pale na wameona. Naomba sasa ...

MHE. CECIL D. MWAMBE: Taarifa.

T A A R I F A

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa keti kwanza,

MHE. CECIL D. MWAMBE: Naomba nimwongezee taarifa Msemaji anayeendelea kwamba hata hao Mawaziri wanapokuja kwenye Kamati, wanalamika kwamba *REA* wanakata pesa kwa wananchi lakini hazifiki kwao kwa ajili ya kuzitumia, ndiyo maana miradi hii imesimama, namwongezea taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngonyani taarifa unaipokea?

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Tena nimeipokea kwa mikono miwili ahsante sana ndugu yangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala...

MWENYEKITI: Ngoja kidogo, naomba ukae tena. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba nimpe taarifa msemaji aliyemalizia kusema kwamba tulihudhuria Kamati yetu ya Nishati na Madini na tulitoa taarifa mpaka mwezi Februari, 2018 tumepokea kiasi cha Bilioni Mia mbili ishirini na moja kutoka Hazina kwa ajili ya Miradi ya *REA* vijijini, kwa hiyo hatujapeleka malalamiko. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngonyani unaipokea hiyo taarifa?

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Naipokea, tena kati ya watu ambao wamenisaidia sana Wizara ya Nishati ni huyo Naibu Waziri.

MWENYEKITI: Sasa ulipokeaje ile taarifa nyingine?

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Alifika akafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye upande wa Maji. Taarifa zote nimezipokea, ya huyu niliipokea kwa vizuri na Mheshimiwa Waziri kwa sababu amefika mpaka jimboni kwangu na amelizungukia jimbo lote na ameona haya matatizo, zote nazipokea na ninaomba Serikali izifanyile kazi. (*Makofii*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

T A A R I F A

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla Mheshimiwa Profesa hajatoka kwenye hoja yake ni kwamba Bunge lilipitisha sheria hapa kwamba tutenge fedha tuweke wigo yaani zuio *tu-ring fence* hizo fedha zinazotoka kwenye mafuta kwa ajili ya miradi ya umeme vijijini.

Sasa kilichotokea ambacho amekijibu Mheshimiwa Waziri ni kwamba wamepokea fedha sasa hivi wakati zile hela kila mwezi zinaingia zinakatwa, zinaingia kule Hazina. Sasa na miradi ile kule imekuwa ikisimama kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ambacho alikuwa anazungumza Profesa ni kwamba miradi ipo kule, fedha zinakatwa na miradi haitekelezeki. Sasa Mheshimiwa Waziri hapa amekuja tu

tumepokea hizi fedha wakati miradi kwa mfano awamu ya tatu ya *REA* imesimama karibu kwa mwaka mzima na Wakandarasi kule mitaani hawafanyi kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwongeza Mheshimiwa taarifa hayo malalamiko aliyokuwa anayatoa Mheshimiwa Mbunge ndiyo malalamiko yetu sote, kwamba tunataka hizo fedha siyo mmezipokea tu mmekaa nazo tunataka ziende kutekeleza miradi ya maendeleo ili wananchi wetu waweze kupata umeme. Kwa hiyo nilikuwa tu naongeza hiyo taarifa kuliweka sawa sawa.

MWENYEKITI: Unachangia bwana! Mheshimiwa Ngonyani.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana unillindie muda wangu, umeona wengine hapa, haya. (*kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la *REA* nafikiri wenzangu wamenisaidia na Waziri amenisaidia, tuje kwenye upande wa TARURA. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili *TARURA* ni kama jipu, tulilipendekeza sisi hapa kwamba *TARURA* itufanyie kazi sasa ipewe kazi ya kutengeneza barabara lakini mpaka leo hii kwangu hawajatengeneza barabara hata moja. Kuna daraja limekatika kutoka Kwa Sunga kwenda Mswaha darajani, miezi tisa daraja halijajengwa hata kujengwa tunaambiwa kuna *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Korogwe unategemea sana Mji wa Mombo kupata fedha ya kuendesha Wilaya ya Korogwe, lakini leo hii mtu aende mpaka Mombo akaangalie barabara zilivyo leo tunaambiwa kuna *TARURA*, hawa *TARURA* ni mtu binafsi? Kama ni chombo ambacho kimeundwa kwa ajili ya kusaidia Serikali ina tatizo gani kwenda kutengeneza barabara ambazo zimekufa? Ni nini kinazuia wakati kuna fedha tayari wameshatengewa na Serikali? (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *TARURA* naomba ielevweke kabisa kwamba *TARURA* pamoja na kwamba wanadai kwamba wametengewa fedha hiso fedha ziko wapi? Kama zipo kwa nini hawatengenezi barabara za vijijini? Tumeziondoa kwenye Halmashauri kwa sababu walikuwa wanataka sana *ten percent*, tukawapa *TARURA* ambao hawaingiliwi na mtu yejote. Sasa kama hawaingiliwi na mtu yejote, fedha zikae mifukoni mwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maji, suala hili ni kigezo kikubwa sana kwa sisi Watanzania, Mbunge yejote atakayefika jimboni kwanza unaulizwa maji. Kuna maji toka mwaka 2010 ambayo yanatoka Mkoa wa Kilimanjaro, Bwawa la Nyumba ya Mungu, hili mpaka leo hatujui yameishia wapi. Tunasikia tu mradi unaendelea, mradi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya Benki ya Dunia, tangu mwaka 2010 mimi naingia Bungeni mpaka leo imesimama. Leo tunasema maji vijijini haya maji vijijini wanapata kina nani? Naomba sana Serikali ile miradi yote ambayo imeanzhishwa na baadhi ya viongozi wamepita na kui-*support* naomba ikamaliziwe kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata shida sisi Wabunge, unafika mahali unawaambia maji yanakuja, unakwenda siku ya pili wanakwambia maji yako wapi? Unafika mahali unawaambia barabara ya lami kutoka Korogwe kwenda Lushoto kuititia Bumbuli itatengenezwa, mwaka wa 10 huu mtu anakuangalia anakwambia barabara ichongwe. Unafika barabara za vijijini zimekufa; unafika suala la vituo vya afya; tunawashukuru sana Serikali hii imetenga fedha taslimu kwenda kwenye madawa kwenda kwenye vituo vya afya, lakini kuna vituo vya afya vingine vimeshaanza kuleta nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Hospitali ya Magunga ya Korogwe, ndiyo hospitali kubwa katika barabara kuu hii, haina gari. Magari yalikuwepo yamekufa na ndiko kwenye ajali kubwa zinazopatikana barabara ya

kutoka Chalinze kwenda Kilimanjaro, wanapitia pale, hakuna gari. Naomba Serikali iiangalie Korogwe kwa macho ya ukunjufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la katani. Katika mazao makuu ya biashara katika Tanzania yamewekwa manne, naomba liwekwe na katani. Katani ni zao kubwa ambalo limeingiza fedha, sisi wengine Tanga tumekwenda mwaka 1961 tukiwa manamba tumefuata Katani. Katani ilikuwa inaingiza fedha kuliko zao lingine lolote, lakini cha kushangaza mpaka sasa hivi katani hii wanaoendeleza ni watu wachache wakulima binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa ambao wanajiita Bodi ya Mkonge wameyajaza mashamba. Katika Tanzania eneo lenye mashamba makubwa ya Mkonge ni Korogwe Vijijini, nina mashamba zaidi ya 18; watu hawaendelezi, wanaoendeleza ni watu walioshika mashamba binafsi akina Mohamed Mo, Mura, Luhinda pamoja na Gai; lakini ukiangalia mashamba ambayo yameshikwa na hawa wenzetu wa Bodi ya Mkonge hakuna shamba hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi si kwamba tunakataa katani, tunaipenda sana katani hata juzi Waziri wa Kilimo amefika pale na kuwakemea sana, lakini yale mashamba ambayo hayaendelezwi wapewe wananchi walime Mkonge. Tunakuwa tukisema mkonge, mkonge, mkonge wenyewe kwa mkulima mdogo kwenye katani ananunua kwa shilingi elfu nne wakati watu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Nahamia sasa kwa jirani yako Korogwe Mjini, Mheshimiwa Maria Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

aliyoiwasilisha Waziri Mkuu. Aliiwasilisha kwa umahiri mkubwa, hatuna budi kuiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudini kubwa anazozifanya akishirikiana na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri na Watendaji Wakuu wa Serikali. Kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu sisi wote tunaiona. Tunaiona kwa macho, tunaiona kwa vitendo na ushahidi wake upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kauli mbiu imezaa matunda kwa kuleta Bomba la Mafuta kutoka Hoima kwenda Tanga ambako ni kwetu, lazima nitaje Korogwe kwa sababu ni kwetu. Tumeona hizo juhudini za reli ya *standard gauge*, tunaona hizo juhudini za ununuzi wa ndege tatu ambazo wengine wanabeza, wanabeza halafu baadaye wanapanda. Tumeona juhudini za upelekaji wa umeme wa REA vijijini, tumeona juhudini za ujenzi wa viwanda, tunaona juhudini vile vile za ujenzi wa ukuta wa Mererani ambaao Mheshimiwa Rais leo ameenda kuufungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudini zote hizi zinafanywa na viongozi wetu ambaao tumewachagua kutoka 2015 hadi 2020, tunawapongea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa ule wa 10 ameeleza ni namna gani Serikali inavyosimamia uhuru wa wananchi kuijunga katika vyama wanavyovitaka. Sasa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kusimamia hayo hadi Chama cha Mapinduzi kimeweza kushinda Kata 58, kimeshinda Majimbo matano, haki ya Mungu hiki chama dume, hapana chezea CCM, kabisa hao wengine wajikaze. Pamoja na hayo naomba niendelee kuipongeza Serikali yangu na nitaipongea sana, mtalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali pale kwangu Korogwe kwenye Halmashauri yangu ya Mji wa Korogwe imeniwezesha kunijengea Stendi ya kisasa kwa

gharama ya bilioni nne. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuja kuifungua ile stendi anasema haipo stendi kama ile ya Korogwe, naishukuru sana Serikali. Hata hivyo, tunajengewa Soko la Kimataifa kwa gharama ya bilioni moja *point mbili*, hivi kwa nini nisipongeze Serikali? Hilo nalo ni dogo? Lazima niipongeze Serikali kwa kazi ambayo inafanya. Piga makofi kabisa ndugu yangu wa CHADEMA huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Maji. Tuna mradi wa maji ambao umeanza, unafanya kazi, kwa maana ya Msambiazi; tulitengewa milioni mia sita na saba, mkandarasi yuko kazini, mradi ule umekamilika asilimia 96. Tuna mradi wa Lwengela Relini na Darajani tulitengewa milioni mia tano na nane, mradi ule mkandarasi yuko kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tatizo kubwa la maji pale Korogwe Mjini Waziri wa Maji alitembelea Wilaya ya Korogwe akaamua kwamba tuachane na kuchimba visima tutumie ule Mto Ruvu, walituletea milioni mia tano ambapo sasa hizo milioni mia tano zimeweza kujenga chanzo cha maji ambacho kitatupatia maji katika Mji wetu wa Korogwe. Ninachokiomba kwa Wizara ya Maji sasa, naomba sasa nipatiwe fedha kwa ajili ya miundombinu ambayo itafikisha maji kwenye maeneo hayo yote ambayo tumetengewa fedha kwenye mradi ule wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilipoonana naye aliniambia watatutengea bilioni mbili ili ziweze kutusaidia kuweza kupata miundombinu ili kusudi ile miundombinu iweze kusambaza maji katika ule Mji wa Korogwe. Kwa hiyo, hayo ni maendeleo mazuri yanayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda. Niendelee kuipongeza Serikali yangu kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kuifanya ya kuhimiza suala la viwanda. Pale Korogwe tulikuwa na kiwanda cha matunda, katika suala

la ubinafsishaji kiwanda kile kilibinafsishwa. Yule bwana aliyepewa kiwanda kile aliamua kuondoa mashine zote akahamia nazo Dar es Salaam, jengo lile limebaki gofu. Kitendo cha kuondoa zile mashine kimesababisha akinamama na vijana hasa ikizingatiwa Korogwe, ikizingatiwa Muheza tunalima sana matunda, yanaiza hakuna kwa kupeleka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Serikali yangu, kwa sababu jengo lile sasa limebaki ni gofu tuombe tupewe sisi Halmashauri ya Korogwe ili tuweze kulitumia kwa kuwawezesha akinamama na vijana waweze kutengeneza matunda kwa kutumia kile kiwanda, watengeneze *juice* kuititia kile kiwanda, viwanda vidogo vidogo ili kusudi waweze kujiwezesha kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umeme wa *REA*. Naishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo. Nami kama mmoja wa watu ambao nina uhitaji na umeme wa *REA* niliomba nipatiwe umeme wa *REA* kwa kata zangu kama tano, sita hivi; Kata ya Kwamgumi, Kwamndolwa, *Old Korogwe*, Mtonga, Mgombezi na Bagamoyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu Waziri niliongea nao wamenipokea vizuri sana na waliahidi kwamba watanisaidia ili niweze kufanikisha hili. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana yule Mkandarasi anasema vile vijiji havipo kwenye orodha yao. Kwa hiyo walikuwa wanaomba ikiwezekana wapelekewe hiyo orodha ili kusudi waweze kuanza kuifanya kazi ya kuweka umeme katika wilaya yetu au katika kata zile ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara; naipongeza *TARURA*, natofautiana kidogo na ndugu yangu maana yake mwenzangu yuko vijijini mimi niko mjini. *TARURA* kwangu kwa maana ya barabara inafanya kazi vizuri. Inafanya vizuri isipokuwa kwa sababu ni wilaya ya mjini, naomba barabara za mjini; nilimsikia Mheshimiwa Waziri juzi nilipokuwa nimeuliza

swali la nyongeza alisema halmashauri za miji zimewekwa kama halmashauri 25 ambazo zitaanza kujengewa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati tunaendelea kusubiri mpango huo wanatengeneza kwa kiwango cha changarawe. Sasa niombe hawa wanaotengeneza kwa kiwango hiki cha changarawe, TARURA, watengewe mafungu kwa ajili ya kujenga hii mitaro, mifereji kwa mawe ili kusudi barabara hizi ziweze kudumu kwa muda mrefu wakati tunaendelea kusubiria habari ya lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu. Naishukuru Wizara ya Elimu ilinisaidia kunipatia fedha kwa ajili ya kujenga Maktaba ya Chuo cha Ualimu pale Korogwe, walnipatia milioni mia mbili na arobaini na tano. Naomba niwataarifu tu kwamba kazi inaendelea vizuri imefikia asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu ile maktaba ikikamilika itatusaidia kwa watoto wetu, wanachuo pamoja na shule zetu za sekondari; ni maktaba kubwa ambayo nadhani hata nchini hapa atakayekuja kuifungua ataiona kwamba ni kubwa kuliko za maeneo mengine yote ambayo wamejenga zile maktaba... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chuachua, Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waziri Mkuu. Kwanza nataka niseme tu mwanzo kwamba nahitaji kumpa pole Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama Taifa, lakini pia pamoja na Wabunge wote wa Upinzani ambaao kwa muda mfupi wiki mbili zilizopita wamepata matatizo na kashkash kutokana na Jeshi la Polisi kutumia nguvu, lakini pia viongozi wetu kuendelea kupata shida kwa sababu wanapigania haki katika Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji kujikita kwenye mambo machache tu na ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikilize kwa makini kwa sababu katika Mkoa wa Katavi tuna changamoto nyngi ambazo tangu mwaka 2008 mpaka sasa tumekuwa tukipigania mambo haya lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inashindwa kutoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 halmashauri ilitenga fedha kwa ajili ya mchakato wa ujenzi wa Chuo Kikuu, lakini pia kuna fedha ilitengwa kwa ajili ya mchakato wa ujenzi wa hospitali ya mkoa katika Mkao wetu wa Katavi. Hata hivyo, lakini *projects* hizi zimefeli, pesa zimepigwa, halmashauri iko kimya na sisi kama Wabunge tumekuwa tukipata hoja kutoka kwa wananchi kwamba ni kwa nini mambo haya, Mkurugenzi pamoja na Baraza la Madiwani 2010 mpaka 2015 walipitisha maazimio haya na fedha hizi zikawa zimetumika ndivyo sivyo, lakini tukihoji kwamba ni kwa nini michakato hii imeishia hewani, wananchi wanapiga kelele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo haya, kwa sababu ujenzi wa hospitali ya mkoa, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo katika Mkao wa Katavi yalikuwa yametengwa katika eneo moja kwa maana ya Kata ya Kawajense. Kuna zaidi ya ekari mia tano lakini mpaka sasa wananchi wako pale, wamechukuliwa maeneo yao hawajalipwa fidia, wakienda kufuatilia kwa Mkurugenzi pamoja na Meya Serikali iko kimya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini tamko la Serikali ili tujue kwamba wananchi hawa ni kweli wameporwa maeneo haya na ni kwa nini Serikali iko kimya kufuatilia

michakato hii? Kwa sababu maswali ya msingi nimekuwa nikiyauliza sana kuhusiana na wizi huu uliofanyika katika Manispaa ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri Mkuu atakapokuja kuhitimisha, naomba kabisa kupitia jambo hili, kwa sababu ndiyo imekuwa kero ya wakazi wa Mkoa wa Katavi. Sasa kama Serikali ni sikuvi na imekuwa ikitumbua majipu. naomba katika Manispaa hii ikasimamie jambo hili. Wizi uliofanyika katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo katika Mkoa wa Katavi, lakini pia wizi uliofanyika katika suala zima la ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; nataka niongelee tu kidogo kuhusiana na ununuzi wa gari la taka. Baraza la Madiwani 2010 - 2015 lilipitisha fedha zaidi ya milioni mia moja kwa ajili ya ununuzi wa gari la kisasa la taka, lakini mpaka hivi tunavyoongea gari halijanunuliwa, matokeo yake Baraza la Madiwani linakuja kuitisha fedha nyingine kununua gari lingine jipya. Maana yake yule *Mr. Kisira ambaye alipewa tenda kwa ajili ya ununuzi wa hilo gari la taka* mpaka sasa hajarudisha hizo fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimepigwa, matokeo yake Baraza la Madiwani kazi yake ni kuitisha tu kwamba tunanunua gari lingine wakati tukiendelea kufanya mchakato huyu *Mr. Kisira ambaye ndiye alikuwa mzabuni wa ununuzi wa hilo gari la taka* alishindwa na hakuwa na vigezo vyta kununua hilo gari la taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nifahamu tu, kwamba kama Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ni sikuvi inashindwaje kwenda kutatua mgogoro huu ambaou umekuwa ni kero kwa wakazi wa Mkoa wa Katavi, lakini mpaka hivi tunavyoongea wananchi wa Mkoa wa Katavi Manispaa ya Mpanda wanachangishwa shilingi elfu mbili kila kaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, takataka zinazagaa kwenye maeneo yao, Manispaa iko kimya, ukimuuliza Mkurugenzi

hana majibu, Meya hana majibu. Sasa tutaendelea kupongeza mambo kama haya ikiwa manispaa ni chafu? Mnatumbua maeneo mengine Manispaa ya Mpanda mnaiacha na wananchi wanachangishwa fedha. Sasa mtueleze tu kwamba gari hili la taka, mimi kama Mbunge nimeshindwa kupata majibu ya msingi niende nikawaeleze nini wananchi wa Manispaa ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niongelee kidogo kuhusiana na masuala ya viwanda. Bado tuna changamoto za viwanda katika Mkao wa Katavi na hazikidhi na ukizingatia Mkao wa Katavi tunalima sana, kwa maana ya mazao ya biashara pamoja na mazao ya chakula. Sasa tunavyoongea ni kwamba hatuna viwanda ambavyo vinaweza kukidhi kuzalisha ajira kwa wananchi wa Mkao wa Katavi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda cha alizeti ambacho kiko katika Kata ya Makanyagio, Kiwanda cha Mpadeku. Kiwanda hiki kiko *dormant*, tunalima alizeti lakini hawazalishi hata zaidi ya tani moja, matokeo yake tumekuwa tunatumia gharama kubwa za uzalishaji, kitu ambacho kinasababisha sasa tunatumia gharama kubwa ya uzalishaji lakini hatupati masoko, lakini pia hatupati faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeomba tu, kwa sababu mnajinasibu ya kwamba ni Serikali ya Viwanda, basi ningeomba tu sasa mtuongezee viwanda kwenye Mkao wa Katavi kwa sababu viwanda vingi ambavyo viko kule tukitegemea vingeweza kuzalisha mazao mbalimbali tungeweza kusindika mazao hayo kwenye viwanda vidogo vidogo lakini imekuwa ni tofauti, kwamba wananchi hawaoni matokeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika changamoto hizo za viwanda, Manispaa ya Mpanda imetenga eneo la Kata ya Misunkumilo, eneo hili wamechukua wajasiriamali wadogo wadogo ambao wamewatoa katika maeneo mbalimbali kwenye Manispaa ya Mpanda. Wamewafukuza kwenye maeneo ambayo wanafanya kazi wakiwepo wanaokata

mbao maana ya viwanda vya mbao kwenye Manispaa, lakini wakiwepo wakata vyuma, wale mafundi *welding*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe tu wajasiriamali hawa wadogo wadogo wamepelekwa katika eneo la Misunkumilo, Manispaa wametenga eneo hili, lakini wamepelekwa kule, hakuna umeme, hakuna maji lakini pia miundombinu yake ni mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali hii ni sikuu ningeomba ingeweza kuwasaidia wananchi hawa kwa sababu wanapigwa, wanafukuzwa kwenye manispaa wanapelekwa kwenye eneo ambalo hakuna miundombinu, sasa niombe tu kama mko tayari kweli kuwasaidia wananchi kwa ujumla na wakazi wa Mkoa wa Katavi mpeleke kwanza miundombinu ya maji pamoja na umeme na si kukurupuka tu kuwafukuza wananchi kuwapeleka kwenye maeneo ambayo hakuna miundombinu ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tu suala la mikopo kwa vikundi vya vijana, wanawake, wazee pamoja na wale mavu katika Mkoa wetu wa Katavi. Mikopo inayotolewa katika manispaa ninayotoka mimi, Manispaa ya Mpanda Mjini, leo hii tunavyoongea vijana wamekopesha fedha, baadhi yao kwa maana ya kwamba sasa hawa Maafisa Maendeleo na watendaji ambao wanahusika na masuala mazima ya kutoa mikopo hii, kuna baadhi ya vikundi vinatoa malalamiko kwamba pesa hizi zinatolewa kwa ubaguzi kwa maana ya kuangalia itikadi zao za vyama na mambo mengine. Kwa hiyo... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana muda wako ndio huo. Tunaendelea, naanza na Mheshimiwa Shabani Shekilindi na hawa wafuatao ninaowataja wajiandae; Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma na Mheshimiwa Alfredina Kahigi wajiandae. Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema kwa kunijalia na mimi niweze kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya, kwani naamini kabisa mwenye macho haambiwi tazama. Pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kazi kubwa anayoifanya sambamba na kumpongeza Waziri Jenista pamoja na Timu yake Naibu Waziri Mheshimiwa Ikupa na Mheshimiwa Mavunde, kwani Watanzania wanaona kazi mnayoifanya hongereni sana. Sisi tunaamini hatuna cha kuwalipa ila Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye atajua cha kuwalipa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika kuchangia sasa. Wenzangu wameshachangia mambo ya bomba kutoka Hoima Uganda kuja Tanga. Niendelee kupongeza juhudhi hizo za Mheshimiwa Rais kwani Mheshimiwa Rais anatupenda sana, naamini kabisa Watanzania sasa itakuwa ni fursa ya kupata ajira katika bomba lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze kupanuliwa kwa Bandari au kuongezwa kina cha bandari pale Tanga, nimpongeze Rais wangu kwa kutupa pesa na kazi ile inaendelea kupanua bandari ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo niiombe Serikali yangu sasa Tukufu kwamba vitu vyote hivi viende sambamba na *standard gauge* hiyo ambayo itaanzia Tanga kwenda Arusha mpaka Musoma. Naomba Serikali yangu tukufu iende sambamba na reli hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tuna uwanja wa ndege wa Tanga. Kwa kuwa tayari tuna *Bombardier*, kwa hiyo niiombe Serikali sasa *Bombardier* ile

iweze kufika Tanga. Ianze Dar es Salaam iende Pemba ije Tanga hadi Mombasa, naamini hiyo sasa ni fursa yetu pamoja na upanuzi wa uwanja ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupongeza hayo niende moja kwa moja sasa kwenye suala la afya. Nimshukuru Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kunitengea milioni mia saba kwa ajili ya Kituo cha Afya Mlola, milioni mia nne kwa ajili ya majengo na majengo yale tayari mpaka sasa hivi yako kwenye hatua nzuri, mengine yanapauliwa, mengine yanafanyiwa usafi na mengine yako kwenye mtambaa wa panya. Mheshimiwa Rais, ahsante sana Mungu akubariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hayo kuna juhudzi za wananchi zinaendelea kufanyika kule, kuna vituo vya afya zaidi ya viwilli vinajengwa pale; Kituo cha Afya Gare na Kituo cha Afya Ngwelo. Kwa hiyo, niombe Serikali kwa kuwa vituo vile vinajengwa kwa nguvu za wananchi...

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa hebu keti kidogo, taarifa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kumpa taarifa mchangiaji, ameeleza hapa kwamba anamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumtengea milioni mia saba, naomba tu kumpa taarifa fedha zote za maendeleo zinatengwa na Bunge hili na siyo Rais.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shekilindi, Taarifa hiyo unaikubali au unasemaje.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo siikubali hata yeye anajua kwamba Rais ndiye Mkuu wa Nchi, ndiye mwenye maamuzi yote. Kwa hiyo wafu ngoja wakazike wafu wao, sisi tuendelee kutangaza injili. (*Kicheko*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo vya afya viwili ambavyo vinajengwa kwa nguvu za wananchi. Sasa niiombe Serikali iweze kupeleka pesa kwa ajili ya kumaliza vituo vya afya vile, ambavyo ni Kituo cha Afya Gare na Kituo cha Afya Ngwelo. Sambamba na hayo kuna Zahanati zaidi ya 19, zahanati zile ziko kwenye nanii tofauti tofauti. Kuna ambazo zinahitaji watumishi na kuna ambazo zinahitaji kumaliziwa, kwa hiyo niiombe Serikali yangu tukufu kwamba ipeleke mafungu sasa...

MHE. CECIL D. MWAMBE: Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msemaji anayeendelea sasa hivi kwamba kwa maneno yake anayoyaongea Bunge hilli halina umuhimu tena kwa sababu silo linalotenga bajeti ya nchi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, saa nyingine hawa watu wakitoa taarifa usiwaruhusu kwa sababu Bunge ndilo linalotenga Bajeti Serikali inatekeleza. Kwa hiyo, mtu wa kwanza kabisa kutekeleza na kutoa maelekezo ni Rais.

T A A R I F A

MWENYEKITI: Taarifa

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nimuunge mkono Mheshimiwa Shekilindi kwamba kama...

MWENYEKITI: Mpe taarifa

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Mheshimiwa Shekilindi na taarifa

yangu kwanza naanza kwa kumuunga mkono; kwa sababu Rais kama haweki mikakati na miongozo imara ya kuzipata hizo pesa, hilo Bunge analolisema Mbunge pale litatenga kitu gani. Kwa hiyo, ndio maana Mheshimiwa Shekilindi anamshukuru Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na ni haki yake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shekilindi taarifa hiyo unaikubali?

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Ulega naipokea kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema awali kwamba naomba sasa Serikali katika bajeti hil itenge pesa kwa ajili ya kwenda kumalizia vituo vile vyaa afya ambavyo ni Kituo cha Gare na Ngwelo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, niende kwenye suala la umeme. Kwanza nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Dokta Kalemani na Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira Mgalo kwani wanafanya kazi kubwa sana. Watu wa REA, sisi tumepangiwa mkandarasi anaitwa *DEM Contractors*, huyu bwana alikuja mara moja tu mpaka leo hajaonekana na vijiji na vitongoji vyote ambavyo vimepangiwa bado hajavifanya kazi, amekuja kupima kama vitongoji viwili, vitatu ameondoka moja kwa moja. Niiombe sasa Serikali Tukufu kwamba mkandarasi yule atafutwe popote alipo aende akatekeleze ile miadi ambayo wameahidiana na Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu. Kuna maboma mengi sana ya maabara yamejengwa lakini maboma yale mpaka sasa hivi yamekuwa ni magofu. Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa ichukue hatua madhubuti kuhakikisha kwamba inakwenda kumaliza maboma yale kwani maboma yale yalikuwa yanajengwa na nguvu za wananchi, kwa hiyo tunapoyaacha vile yalivyo wananchi sasa hivi hata uwezo

hawana. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu Tukufu sasa imalizie maboma yale ili watoto wetu waweze kusoma elimu kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Wilaya ya Lushoto tangu iumbwe ina wananchi wengi sana lakini hajjawahi kupata Chuo cha *VETA*. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu, hususan Wizara; Waziri wa Elimu naomba atakaposimama pale aniambie lini atanitengea pesa za kujenga Chuo cha *VETA* Lushoto. Kuna sekondari zaidi ya 105, kwa hiyo nimwombe Waziri wangu atakapo-*wind up* hapo basi aniambie kwamba ni lini atatenga mafungu hayo kwa ajili ya kujenga Chuo cha *VETA* Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, niende kwenye barabara; wenzangu wameongea mambo ya *TARURA*, ni kweli lakini mimi nilichoona *TARURA* ni watu wazuri sana ila naamini bado hawajatengewa mafungu kwenda kule. Mfano mimi ninachoongea, barabara zangu pale Lushoto Mjini bado ni tatizo, kuna mashimo makubwa sana, hata nikipita pale wananchi wananiuliza hivi Mheshimiwa Mbunge upo, hivi hii hali unaiona? Kwa hiyo niiombe sasa Serikali ipeleke mafungu kwenye Taasisi ya *TARURA* iweze kujenga barabara zile sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna barabara ambayo kila siku naiongelea hapa, Barabara kutoka Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya – Mlingano hadi Mashewa ambayo ni kilometra 57.7, barabara hii imeshasemwa mara nydingi, kabla ya mimi kuingia Bungeni waliopita wameshaizungumzia barabara hii tangu 1995, lakini barabara hiyo mpaka sasa hivi bado haijapandishwa hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Waziri sasa, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, atakapo-*wind up* hapo anipe majibu barabara ile itapandishwa hadhi lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna barabara ya mchepuko ambayo ni kilometra 16, inaanzia

Dochi – Nguli hadi Mombo. Nimwombe sasa Waziri barabara ile iweze kutengenezwa kwani barabara ile ni barabara mbadala ambayo barabara hii kubwa ya kutoka Soni – Mombo ikiziba basi barabara ile inatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye wale mavu, ukurasa wa 24; nimeona wale mavu wametengewa vitu vingi kidogo, lakini upande wa vijiji ni wale mavu hawa wamesahaulika. Niiombe Serikali yangu sasa itakapotenga pesa hizi basi ipeleke vijiji ni kwani vijiji ni kuna wale mavu wengi sana ambao wamesahaulika, kwa hiyo niiombe Serikali yangu tukufu iweze kutenga pesa ili iweze kuzipeleka vijiji ni. Uizingatia mazingira ya vijiji ni miundombinu si rafiki, mnaifahamu wenyewe hata Mwenyekiti naamini unaifahamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji; kama unavyo jua maji ni uhai na katika mwili wa binadamu maji ni asilimia 75. Kwanza niipongeze na niishukuru Serikali yangu kwa kunitengea milioni mia saba sabini kwa ajili ya Mamlaka ya Maji Mjini. Pia niendelee kuipongeza kunitengea milioni mia tano kwa ajili ya mradi wa Ngulu – Kwemashai na pia niipongeze Serikali kwa kunipa milioni mia nne hamsini kwa ajili ya maji Mlola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mradi ambao una miaka mingi sana, mradi wa kutoka Mtumbi kuja Kwekanga, kuja Malibwi kuja Kilole kwenda mpaka Mbwei, mradi huu ni wa miaka mingi sana, kwa hiyo niiombe Serikali yangu sasa iweze kutenga pesa awamu hii ili tuweze kutekeleza mradi ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, kuna mradi ambao unatoka Lushoto kwenda Mkuzi kupitia mpaka Kwemakande, mradi ule walishafanya *feasibility study* (upembuzi yakinifu), lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea ambapo mradi ule unaghanimu shilingi bilioni moja na milioni mia sita, ambapo ukitekelezwa utatoa kabisa changamoto au utatatua matatizo ya maji katika maeneo hayo niliyoyataja.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, mimi niko kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii; tulienda Mkoa wa Geita tukaenda mpaka Mkoa wa Kagera, nilikuwa na rafiki zangu Mheshimiwa Kalanga, Mheshimiwa Nassari na wengineo, tuliona pale Chato Uwanja wa Ndege Chato. Kwa hiyo niendelee kumpongeza Rais wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine walikuwa wanasema uwanja ule hauna maana, uwanja ule una mapori matatu wanaita BBK (Biharamulo, Burigi na Kimisi), kwa hiyo uwanja ule naamini kabisa utatoa fursa kubwa sana. Ningetegemea wenzangu hawa wamuunge mkono Rais kwamba juhudzi alizozifanya ni juhudzi ambazo zinatakiwa tumwombee dua, lakini... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Gekul.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Hapana, kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu anasema kuhusu utaratibu kwa sababu inahusu ukiukwaji wa Kanuni, ndio tunaanza na hilo. Sasa huyu anayeniambia kuhusu

utaratibu nampa *preference* na aniambie ni Kanuni ipi imekiukwa ili niweze kutoa uamuzi.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kuhusu utaratibu wa Kanuni ya 64...

MWENYEKITI: Umeniomba kuhusu utaratibu, usiniombe mwongozo.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, naendelea. Ni Kanuni ya 64(1)(a), naomba niisome, inasema:-

"64.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli;"

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliyejita wakati anachangia alieleza kwamba Mheshimiwa Rais ndiye anayetoea fedha, lakini kwa mujibu wa taratibu na sheria zetu Bunge ndilo linalopitisha mpaka bajeti ya Mheshimiwa Rais na ofisi yake, ndiyo maana siku ya leo tunajadili bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu zaidi ya bilioni 124.

Sasa naomba ufanuzi kwenye Meza yako, je, hili linaruhusiwa? Wewe umekaa hapo kama Spika ambaye unaongoza Bunge hili, Mbunge anapotosha kwamba Rais ndiye anayetoea fedha; anisaidie tu kama Rais huyu anatoa fedha mfukoni au hizo milioni 700 ni mshahara wake au ni sisi Bunge tunapitisha na ni fedha za wananchi walipakodi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, Kanuni ya 64 umeomba kuhusu utaratibu; uniambie ni Kanuni ipi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

iliyokiukwa na Mheshimiwa Shekilindi, niambie tu Kanuni iliyokiukwa, nitajie tu.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema ni Kanuni ya 64(1)(a); Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Taarifa alizotoa kwamba amepewa milioni 700 na Mheshimiwa Rais hazina ukweli kwa sababu Rais hatengi bajeti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul na Waheshimiwa wengine, ili tujifunze taratibu za Kibunge mzielewe; ni kweli Serikali inakuja humu kuomba, Waingereza wanaita *demand for grant*; inaomba, inajenga hoja, Bunge linaridhia au kukataa. Linaporidhia, utekelezaji ni wa Serikali kupitia mafungu yake yote mliyoidhinisha kama Bunge. Ndiyo maana tunapoanza zile wiki tatu za mwanzo kufuatilia utekelezaji wa fedha ambazo Bunge liliombwa na likaridhia muweze kuona zimetumikaje ili mpime kwa maombi yanayokuja kwa mwaka unaofuata. (*Makofii*)

Kwa hiyo zikisharuhusiwa na Bunge kutoka ni za Serikali; mmeidhinisha ninyi na ndiyo maana mnakuja kuwasimamia mmetumiaje. Kwa hiyo Rais ndio anayesimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Bado Bunge linabaki na *role* yake ya kuidhinisha. Ni Bunge linalidhinisha baada ya kuombwa, lakini ye ye anaposhukuru pia anashukuru kwamba Rais ameona *priorities* zile amepeleka milioni mia saba. Waheshimiwa Wabunge, mimi nadhani tusilet semantics na mnafahamu. (*Makofii*)

Mnaona tunakula muda wetu, lakini mimi nawashukuru sana; Mheshimiwa Naibu Waziri Mazingira.

MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ulikaribia kunifilisi mwongozo wangu; naomba mwongozo wako, kwa sababu wakati Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Paresso wanatoa taarifa kwa Mheshimiwa Shekilindi walitumia neno la kutenga bajeti, kwamba si kazi ya Mheshimiwa Rais, si kazi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa sababu katika Bunge hili la Bajeti Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli, imetenga, narudia, imetenga triliuni 32.7 ambazo ndiyo Bajeti Kuu na baada ya kutenga fedha hizo kila Wizara wametenga fedha kwenye Wizara zao ambapo ndipo tunajadili makadirio ya Wizara hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa wao Bunge halina *role* ya kutenga na lina *role* ya kuidhinisha au ku-*pass the budget*, naomba mwongozo wako; katika mazingira ambayo Waheshimiwa Wabunge hawa hawajui kutofautisha maneno kati ya kutenga na neno la kuidhinisha au ku-*approve budget...*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: ,Bunge hili lina utaratibu gani wa kutoa elimu kwa Wabunge wa aina hiyo ili wajue kutofautisha maneno na wajue kwamba...

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: ...Jemedari Mkuu wa nchi hii wa bajeti ambaye ndiye ownerwa bajeti katika kutekeleza...

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: ...ni Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Magufuli. Kwa hiyo Dkt. Pombe Magufuli kutenga fedha za kwenda kwa Mheshimiwa Shekilindi sio kazi ya Bunge?

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, narudia; tutaendelea kujifunza, mimi huwa narudia kusema hakuna mwenye *monopoly* ya *knowledge*, unaweza kuwa na uzoefu zaidi kidogo kuliko mwenzako lakini ndiyo sehemu ya *knowledge*.

Nimejaribu kulielezea suala hili; nendeni kwenye Sura ya Saba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isomeni kwa utulivu tu halafu sasa shuka chini uje kwenye Sheria ya Bajeti, isome vizuri, soma na Sheria ya *Public Finance* na Kanuni zake, soma sasa vizuri na Kanuni za Bunge kwenye maeneo haya ambayo tuko sasa hivi ya bajeti; ndipo utaelewa *process* nzima hii.

Sasa nitaendelea kumwomba Katibu wa Bunge aendelea kutunoa tuwezeshwe kupitia semina tuelewe masuala haya. Mheshimiwa Shekilindi alipokuwa anashukuru wala hakwenda nje hata kidogo; Bunge liliidhinisha, liliombwa likaidhinisha, utekelezaji ni wa Serikali na ndiyo maana Bunge sasa linaangalia kama tumetekeleza vizuri. Mkikataa mmekataa, kuna taratibu. (*Makofî*)

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. La Mheshimiwa Kangi nimeshajibu, mwongozo wangu ndiyo huo.

Waheshimiwa Wabunge, tumechukua muda mrefu sana kwa mambo haya, inakula muda wetu mjue wengine hamtapata nafasi ya kuchangia, nami kwa sababu ni *driver* hapa nitajua namna ya kucheza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Dokta Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kumpa pongezi Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya; kwa muda wa miaka miwili na nusu hii amefanya mambo mazuri sana. Mwenyezi Mungu ambariki katika kazi zake zote anazozifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri naye anayoifanya pamoja na watendaji wake wote wa Serikali, kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana; Mheshimiwa Jenista, Naibu Mawaziri pamoja na Makatibu wote na wafanyakazi wote nawapa pongezi sana kwa hotuba hili ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ameitoka hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mazuri sana ambayo yamefanyika katika Mkoa wangu wa Morogoro, nianze na viwanda. Katika Mkoa wangu wa Morogoro, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi naye juzi juzi alikuja kwenye kiwanda cha sigara, Mheshimiwa Rais ameweza kufungua kiwanda cha sigara. Kwa kweli Morogoro tunakwenda vizuri kwa upande wa viwanda, si mbaya sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda tuna *21st Century*, tuna Mazava na viwanda vingine vyote vinaendelea vizuri. Ila hapa naomba vile viwanda ambavyo havifanyi kazi ambavyo vimekuwa, naomba itafutwe namna ya kuvifufua na wale ambao hawawezi kuviedesha naomba sana waweze kunyang'anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda cha magunia, wananchi wengi sasa hivi wanalima wanahitaji magunia ya kuhifadhi mazao yao, lakini hiki kiwanda hakifanyi kazi. Naomba sana Serikali ione jinsi ya kufufua hiki kiwanda cha magunia badala ya kuagiza magunia kutoka nchi za nje. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Morogoro tayari *standard gauge* inajengwa kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro na naaminini kuwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro wataitumia vizuri sana; nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Kilombero; kwa kweli wananchi wa Morogoro tunashukuru sana kuona kuwa Daraja la Kilombero sasa hivi linafanya kazi na unaweza ukapita wakati wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shamba la miwa la Mkulazi ambalo linafaidisha sana hata wakulima wa nje (*out growers*), ambao tunaweza tukapata sukari, pamoja na shamba la Mkulazi // ambalo litaongeza sukari. Kwa hiyo kwenye matatizo ya sukari kuna kipindi ambacho huwa tunapata tatizo la sukari, naaminini kuwa Watanzania tutaweza kupata sukari pamoja na ajira na mambo mengine; pia na umeme, tutaweza kuzalisha hata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimaliza hayo nakuja kwa upande wa *TARURA*; pale mjini Morogoro barabara kwa kweli zimeharibika, naomba watu wa *TARURA* waweze kutengeneza barabara za Morogoro Mjini kwa sababu Morogoro Mjini kuna barabara ambazo unapita zimekuwa mashimo, kwa hiyo naomba sana Serikali iweze kuwapatia hela ili waweze kututengenezea Mji wetu mzuri wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya; naomba niongelee hospitali yetu ya mkoa. Wabunge wengi wa Morogoro hapa Bungeni huwa tunaongelea hospitali ya mkoa, tunaomba kila siku *X Ray*. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Morogoro wakati pale anaangalia kiwanda pamoja na Mkulazi //nilomba *X Ray*na humu ndani Wabunge wenzangu wamekuwa wakiomba kuhusu *X Ray*. *X Ray* ya Hospitali ya Rufaa ya Morogoro haifanyi kazi vizuri. Pia tumeomba vifaa vingine kama *CT Scan*. Naomba muiangalie vizuri Hospitali yetu ya Morogoro, inahitaji kuboreshwa zaidi na zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Morogoro kuna Wilaya ambazo hazina hospitali kwa mfano Wilaya ya Mvomero na Morogoro Vijijini. Unakuta Wilaya hizi wagonjwa wengi wanakuja kutibiwa kwenye Hospitali ya Mkoa ya Rufaa na wanarundika sana. Kwa hiyo, naomba kwenye bajeti nijue hii Hospitali ya Morogoro Vijijini ni lini itajengwa? Naamini hela kiasi ilipelekwa lakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hajengwi pale Mvuha iliposemekana basi naomba kiboreshwe Kituo cha Afya cha Dutumi au cha Tawa na kupata hadhi ya Hospitali ya Wilaya pamoja na Mvomero hatuna Hospitali ya Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye upande wa maji, Mkoa wetu wa Morogoro Wilaya nyingi hazina maji safi na salama hasa Morogoro Mjini kwa kweli mitaa ipo, lakini unakuta kata nyingi hatuna maji safi na salama. Tuliambiwa kuwa Bwawa la Mindu litaweza kukarabatiwa na tukaambiwa kuwa usanifu tayari umefanyika, lakini mpaka sasa hivi haieleweke ni lini hili Bwawa la Mindu litaweza kukarabatiwa na tutaweza kupata maji, kwa sababu ukiongea na Mheshimiwa Waziri wa Maji inaonekana muda wake bado kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maji pia niongelee kuhusu Wakala wa Maji Vijijini. Naomba Wakala wa Maji Vijijini iweze kuanzishwa kusudi tuweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niongelee kuhusu Sh.50 kwa kila lita ya dizeli pamoja na petroli iweze kuwa Sh.100 ili tuweze kupata maji ya kutosha. Wananchi wote wanahitaji maji, hakuna hata Mbunge mmoja hapa ambaye hahitaji maji. Maji ni muhimu sana naomba Wabunge wote waunge mkono kuhusu jambo hili la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu asilimia nne ya akinamama, asilimia nne ya vijana na asilimia mbili kwa wale mavu. Ni kweli Halmashauri zingine zinatoa lakini Halmashauri zingine hazitoi. Kwa hiyo, naomba kuwa

tamko litoke hapa Bungeni tena Wakurugenzi waweze kutoa hizi hela bila kujali wanapata mapato ya ndani kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa nishati ni kweli Waheshimiwa Mawaziri wanafanya vizuri mdogo wangu Mheshimiwa Subira pamoja na Mheshimiwa Kalemani mnafanya vizuri kwa upande wa *REA*. Hata hivyo, kuna vijiji mbalimbali kwenye Mkoa wa Morogoro hasa Kimamba, Kitongoji cha Diwani Frola ambacho mmekipitia, lakini wananchi wote wanaokaa hapo hawana umeme. Kwa hiyo, naomba mkiangalie pamoja na vijiji vingine ambavyo bado havijapata umeme wa *REA* kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, namshukuru Mheshimiwa Rais na vlongozi wote wa Serikali kwa kweli elimu bure (bila malipo) ni nzuri sana. Hata hivyo, naomba mhamasishe kuchangia chakula cha mchana kusudi watoto wetu waweze kupata chakula cha mchana, naona wazazi wengi hawajaelewa. Kwa hiyo, naomba litoke tamko hapa Bungeni kuhamasisha kuchangia angalau chakula cha mchana kwa watoto wetu hawa wanaosoma kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Morogoro upande wa Walimu wa sayansi sekondari tuna upungufu wa Walimu 614 na kwa upande wa maabara tuna upungufu wa maabara 281. Kwa upande wa shule za msingi ambapo mara kwa mara huwa tuna Walimu wengi, lakini sisi tuna upungufu wa Walimu 4,643. Kwa hiyo, naomba wazifanyie kazi hizi takwimu ambazo nimezitoa ili tuweze kupata Walimu wa sayansi kusudi tuweze kwenda na sayansi na teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo hasa cha umwagiliaji, naomba tukiangalie. Tuiseme tu *green house, green house, no, lazima tuangalie tutahamasishaje* kilimo kwa sababu bila ya kilimo...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ingawa muda ulikuwa kidogo, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma na Mheshimiwa Kaboyoka ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Ijumaa Tukufu na nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza uko kwenye ukurasa wa 14 juu ya suala zima la uvezeshaji wananchi kiuchumi. Napenda kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha za Mfuko wa Maendeleo kwa ajili ya uvezeshaji wananchi kiuchumi, lakini niseme bado kuna changamoto kubwa kwa sababu hela inayotengwa haijaweza kuwanufaisha wananchi waliokuwa wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iwe na jicho pana zaidijuu ya huu Mfuko wa Maendeleo kuhusiana na hii asilimia 10 kwa maana asilimia nne vijana, asilimia nne wanawake na asilimia mbili walemavu. Changamoto kubwa hapa asilimia 10 hii upatikanaji wake tunategemea vyanzo vya ndani vya Halmashauri zetu na Halmashauri nyingi zina changamoto kubwa mara baada ya kupokonywa baadhi ya vyanzo vyao kwenda Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na changamoto ya matamko ama maagizo ya Waheshimiwa Mawaziri pengine asubuhi ama wakisimama hapa Bungeni kwa kuagiza mambo kadha wa kadha, Halmashauri zifanye pasipo kuwatengea bajeti. Kwa hiyo, hilo ni tatizo kwani ile dhana nzima iyotafutwa ya uvezeshaji wananchi kiuchumi kama hili jambo halijaangaliwa vizuri, haitakaa ifikiwe. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea hapohapo, tunawaambia Wakurugenzi kwamba wahahikishe wanatenga hizi hela ama baada ya kupokonywa hivi vyanzo tunawaambia wawe wabunifu, lakini wanapokuwa wabunifu wakianzisha vyanzo vipyta Serikali Kuu mnawanyang'anya. Kwa hiyo, hili ni tatizo lazima Serikali tuliangalie kwa jicho pana kabisa. Pia, *so long* hii asilimia 10 hatujaiwekea utaratibu wa kisheria itakuwa kila siku ni hivihivi tunapiga *dilly-dally* hizi hela hazitakaa zitoke kwa ukamilifu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye ukurasa huohuo wa 14, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaendelea kwa kusema kwamba, uwezeshaji wa wananchi wakiwemo vijana, wanawake na wazee. Hapa nitaomba kusaidiwa, nashindwa kufahamu Mfuko wa moja kwa moja ambaao uko kwa ajili ya uwezeshaji wa wazee, nitaomba nije nisaidiwe ni Mfuko gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niseme sioni namna wazee wanavyoweza kushiriki kwenye mchakato huu wa *VICOBA, SACCOS*ama huu Mfuko wa Maendeleo ambaao tayari umeshajipambanua ni kwa ajili ya vijana, wanawake pamoja na watu wenye ulemavu. Kwa wazee napenda kuishauri Serikali, pengine muda umefika sasa ule mchakato wa *universal pension* (pensheni kwa wazee) mje nao ili tuweze kuwasaidia wazee wa Taifa hili. Sitaki kuzungumza sana, ni wazi tunafahamu mchango wa wazee kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, nipende kuiambia Serikali...

TAARIFA

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji anayeongea anaongea mambo ya

muhimu sana lakini Waheshimiwa Mawaziri ukiwatazama wanapiga stori na Mheshimiwa Waziri Ulega pale anamsemesha Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu anamsikiliza yeye badala ya kusikiliza Waheshimiwa Wabunge wanasema nini.

MWENYEKITI: Unampa taarifa nani?

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji asikilizwe. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia, ye ye ndiye anaweza kuwaambia hawa Mawaziri wasiendelee kuzungumza? Mimi ndiyo ungeniambia kanuni, kama ni kanuni ningekupatia lakini hii, haya, Mheshimiwa Chakoma endelea.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda tu kuishauri Serikali iangalie namna bora ya kuanzisha mchakato wa *universal pension* (pensheni kwa wazee wote) ili tuweze kuwasidia wazee wa Taifa letu kwa mchango wao mkubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili uko kwenye ukurasa wa 18 kuhusiana na suala zima la ajira. Nipende kuipongeza Serikali kwa kuanzisha miradi mikubwa ukiwemo wa *Standard Gauge*, *Stiegler's Gorge*, bomba la mafuta, ujenzi wa viwanja vy a ndege pamoja na ujenzi wa meli pamoja na vivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba uanzishwaji wa miradi hii inaenda sambamba na upatikanaji wa ajira. Ninachopenda kuishauri Wizara isikae ikaishia *ku-count* kwamba *Standard Gauge* imetoa ajira ngapi, *Stiegler's Gorge* itatoa ajira ngapi, napenda twende mbele zaidi ihakikishe inafuatilia huku kwenye hii miradi watu ama wananchi wanapata ajira zenye staha na *job security*. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu mikataba inayoingiwa kwa wananchi ambao wanapata ajira kwenye miradi hii imekuwa ina ukakasi ama imekuwa ikiwaminya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano kwenye ujenzi wa feri ile ya Kigongo - Busisi, tulienda pale tumekuta ujenzi wa feri unaendelea, Watanzania wengi wako pale wameajiriwa, lakini changamoto inayojitokeza pale mikataba inakiukwa, ile mikataba ambayo imeingiwa haifuatwi. Kwa hiyo, nawaomba msiishie tu kuhesabu ajira zillizopatikana mwende mbele zaidi mkaangalie ajira hizi kama zina staha, mikataba inafuatwa na kama *job security* iko ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine uko ukurasa wa 44 kuhusiana na barabara. Asubuhi hapa wakati Mbunge wa Singida anauliza swali Wabunge wengi walismama hapa kuhusiana na suala zima la barabara. Sote tutakubaliana Mikoa, Wilaya ama Majimbo ambayo yamepata ujenzi wa kuunganishwa kwa barabara ya lami uchumi wao unaenda haraka ukillinganisha na yale maeneno mengine. Tunakubaliana kabisa upatikanaji wa barabara ya lami kuunganisha mkoa mmoja na mkoa mwingine unapeleka maendeleo ya kiuchumi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa nataka niiombe Serikali ikae chini na iangalie jambo moja. Kiukweli ujenzi wa barabara una ghamama kubwa mno, kilometa mbili tu unakuta ni *billions of money*. Sitaki kuamini kama kwenye Wizara kuna kushindanishwa kwamba Wizara gani imekusanya kwa kiasi gani kwa sababu *nature* ya Wizara zingine ziko kwa ajili ya kutoa huduma tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu kwenye ujenzi wa barabara kumekuwa kuna tozo nyingi sana. Ukiacha hii ya fidia (*compensation*) ambayo hiyo kwa namna moja ama nyingine itakuwepo tu kuna hii fidia ya mrabaha au *royalty* ambayo barabara zetu zinajengwa kwa kutumia changarawe, kokoto, mawe, mchanga, maji, chokaa na kadhalika. Mradi wowote wa barabara huwa unai-*include* hivi vitu pamoja na hizi tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, vumbi la kokoto kwenye ujenzi wa barabara kwa mita moja ya ujazo Wizara

ya Nishati na Madini inatoza Sh.25,000, mawe inatoza Sh.16,000 lakini kokoto kwa mita moja ya ujazo inatoza Sh.80,000, kuna tozo nyingi ambazo zinaingia inapelekeea miradi ya barabara kuwa ya gharama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali ama kuiomba hebu wakae chini waangalie kwamba endapo wakiondoa hizi tozo watakuwa wamepunguza gharama ya barabara kwa asilimia ngapi ama wamepunguza kwa kiasi gani, pengine inaweza ikasaidia. Niwaombe wakafanye hiyo *analysis* waone kama itaweza kuwa na mchango tukijaribu kuziondoa hizi tozo. Kwa sababu kuna ile Sheria ya Ardhi wanasema kwamba Serikali inapotwaa ardhi yake haiwezi kulipa, sasa inakuwaje hapa Wizara ya Ujenzi inaenda inalipa hela nyingi kwenye Wizara ya Madini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa sababu kila Wilaya, kila Jimbo na kila Mkao unashuburi kuunganishwa kwa barabara ya lami, ni vema sasa wakapitia sheria hii kama kuna uwezekano wa kupunguza hizi tozo zikapunguzwe ili suala zima la ujenzi wa barabara liende haraka haraka ili ziweze ku-*boost* uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumzia barabara kuna Kisiwa Mafia. Kisiwa kile ili uweze kufika kwenye Makao Makuu ya Mkao wa Pwani hakuna usafiri zaidi ya maji na kwa wale waliojaliwa ndege, lakini wananchi wengi wanasaferi kwa njia ya maji. Hatuna kivuko cha kuwavusha wananchi kutoka Mafia kuja Makao Makuu ya Mkao wa Pwani ambayo ni Kibaha Maili Moja. Sisi kule hatuhitaji barabara, tunahitaji kivuko. Kwa hiyo, niombe Serikali iwasaidie wananchi wa Mafia ili kuweza kupata kivuko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho utakuwa kwenye ukurasa wa 44 kuhusiana na TARURA. TARURA ina changamoto kwamba kile kiasi cha 30% ambacho wanapewa hapohapo kinatumika kwa *administration cost* lakini nyingine kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo, kile kiasi cha 30% kiongezwe ifike angalau 50%.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu tuna barabara ya Vigwaza – Kwala – Dutumi - Kimalamasale ambayo inaunganisha Wilaya tatu za Mkoa wa Pwani, Bagamoyo, Kisarawe na Kibaha Vijijini. Tuna barabara pale ambapo unapita mradi wa bandari kavu, barabara ile *TARURA* wanasema hawana uwezo nayo, *TANROADS* wanasema iko kwa *TARURA*, wamekuwa wanatupiana mpira kati ya *TARURA* na *TANROADS*. Naamini kama *TARURA* wataongezewa hela ya kutosha pengine wanaweza wakaijenga barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu Serikali tuisubiri mpaka ule mradi wa bandari kavu ukamilike ndipo tuweze kuipitisha ile barabara ya Iami. Nadhani ni vema tungeitengeneza sasa hata kuvutia wawekezaji waende wakajenge kule hoteli. Pia wakati mradi unaendelea vifaa vinavyotumika kujengea mradi ule wa bandari kavu viweze kupita kwenye barabara ambayo inapitika vizuri. Kwa sasa hivi ile barabara haipitiki vizuri. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iangalie namna bora aidha, kuichukua hiyo barabara kwa upande wa *TANROADS*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Alfredina Kahigi na Mheshimiwa Kaboyoka, Mheshimiwa Mashimba Ndaki na Maulid Mtulia, wajiandae.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami ili kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyotuletea mbele yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo imeja mambo mazuri mengi, inasomeka na inaeleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nichangie hoja chache ambazo nimezipangilia. Nianze na upande wa kilimo. Mimi natokea Mkoa wa Kagera. Hatujamaliza mwaka mzima Mheshimiwa Rais amepunguza tozo ambazo zilikuwa zinabambikizwa wakulima wa kahawa lakini nami lazima niungane na Wabunge ambao jana walizungumzia zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa, sijui hao ambao wameleta kilio tena kwa mara nyingine wamepewa mamlaka na nani kushusha bei ya kahawa na kuirudisha kilo moja Sh.1,000. Wakulima wa kahawa sisi tunakaa pembezoni mwa nchi ya Uganda na kahawa nyingi huwa zinaenda sehemu ya Uganda, nina wasiwasi hata kama wakiweka ulinzi wa namna gani kahawa zitavushwa zitaenda Uganda na pato la Taifa litapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo, Waziri wa Kilimo yupo, naomba hili suala walishughulikie haraka sana iwezekanavyo kabla kahawa hazijavushwa kwenda Uganda. Binadamu ana akili kali sana huwezi kumzuia, hata ukiwa na bunduki atafanya njia zozote zile atavusha hizo kahawa. Toka juzi wamenipigia simu wanaomba hili suala tuliongelee kwenye Bunge. Sasa maadam tuko kwenye Bunge, kilio cha wananchi nimekifikisha, hivyo naomba hatua za haraka zichukuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi upande wa barabara, kuna Wilaya tatu ambazo zina barabara ambayo haina lami lakini barabara ni nzuri. Nashukuru Serikali ya Mheshimiwa John Joseph Magufuli imeshughulikia barabara na nchi yetu ni kubwa. Nishauri kutoka Muleba Kusini kwenda Bukoba Vijiji kwenda Wilaya ya Karagwe tuna barabara ya udongo. Niishauri Serikali kwa kipindi hiki ambacho tunaingia kwenye bajeti, barabara hiyo waitengeneze kwa kiwango cha lami maana ni kilometra 74. Naomba hilo walizingatia kwani barabara hiyo inasaidia Wilaya tatu, kuingiliana ni kitu cha maana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Omurushaka - Murongo katika Wilaya ya Kyerwa, ina kilomita 120 inaungaisha nchi mbili, Tanzania na Uganda. Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba na barabara hiyo waishughulikie. Ukienda upande wa Uganda unakuta wana barabara ya lami, ukija huku ni barabara ya udongo. Mvua zikinyesha magari yanapita kwa shida sana, hivyo, kama wakitengenezewa wakawekewa lami itakuwa ni nzuri zaidi na itadumu kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke kwenye suala hilo nije kwenye afya. Kikao kile tulichomaliza niliomba Wilaya ya Bukoba Vijijiini na sisi tujengewe Hospitali ya Wilaya kwani hatuna Hospitali ya Wilaya. Wilaya zote zina Hospitali za Wilaya, lakini ni Bukoba Vijijiini peke yake ndiyo haina Hospitali ya Wilaya. Nina matumaini makubwa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Naibu wake wallinahidi kwamba watatujengea na sisi hospitali. Nimesikia wanasema Wilaya 27 watajengewa hospitali, sina uhakika kama na Wilaya yetu wameiweka, kama wameiweka nitashukuru sana na sisi kupatiwa nafasi hiyo. (*Makofi*)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa. Mheshimiwa Kahigi kaa kidogo.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba hoja iliyoko mbele yetu sasa ni hotuba ya Waziri Mkuu. Haya anayoongea yako kisekta zaidi sijui yako ukurasa wa ngapi wa kile kitabu mbele yake?

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina akili timamu, naongea kitu ambacho nakijua na wamekuwa na mazoea nikisimama kuongea wanaanza kubeza, lakini siyo wote ni wale ambao akili zao sijui zikoje. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea.

MBUNGE FULANI: Endelea.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika bajeti hii kweli waikumbuke Wilaya yangu, watujengee Hospitali ya Wilaya tuachane na kwenda kwenye hospitali za *private* na sisi tuwe na hospitali yetu ya kujitegemea moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka upande wa afya nakuja kwenye siasa. Sina vyta sijui ni ukurasa gani na nini mimi natwanga tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siasa tuna Msajili wa Vyama vya Siasa, nipende kumtia moyo na kumshukuru sana. Ni Jaji mwenye akili nzuri sana, ni mtiifu na nimshukuru Mheshimiwa Rais aliyemteua kumpa nafasi hiyo. Ujumbe nataka ufile kwa Mheshimiwa Rais; huyu baba hapaswi kumtoa katika nafasi hiyo, ni mvumilivu, ni mstahimilivu ametukanwa sana, lakini mimi nimemsikiliza sana ni baba mwenye moyo safi sana, baba anayependa kulea vyama vyetu, Mheshimiwa Rais aendelee kumweka katika nafasi hiyo mpaka tujue ustaarabu ni nini, anatukanwa bure baba wa watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili na Mheshimiwa Mutungi alipo ajue kwamba Mama Kahigi nipo pamoja naye, Mheshimiwa Rais namshukuru sana kwa kutupa Msajili mwenye busara kama huyu, anatukanwa bure, Mungu atawaona. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niende kwenye miundombinu. Kwenye miundombinu naishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mkao wangu wa Kagera tuna uwanja wa lami ni mzuri mno, lakini hatuna taa za kwenye uwanja ndege haiwezi kuteremka usiku. Ni kitu kimoja tu hicho ambacho wanaweza wakatusaidia, wakatuwekea taa za ndege kuweza kushuka usiku vinginevyo uwanja ni mzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kahigi kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka kama nilivyosema atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaki.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Nasikitika sauti yangu kidogo siyo nzuri nilikuwa na *flu* lakini nisameheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika mambo mawili, matatu hivi. La kwanza nitaangalia hii kaulimbiu ya awamu ya tano kuhusu viwanda, lakini pia nitaangalia jinsi ambavyo Serikali inajipanga kuwekeza katika kuboresha miundombinu ambayo itasaldia viwanda hivi viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Waziri Mkuu amesema kwamba hadi kufikia Februari, 2018 viwanda vipyta 3,306 vilikuwa vimeanzishwa. Nasema wazo la kuanzisha viwanda ni zuri maana nia ni kuboresha nchi yetu kufikia katika uchumi wa kati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu kubwa ni jinsi ya utekelezaji wa hii miundombinu. Rais alivyotamka hilo kama ndiyo kipaumbele chake nilitegemea kuwe na mkakati madhubuti ambapo sekta mbalimbali zinakaa, Wizara zinakaa kuangalia kwenye kila Mkoa kuna *opportunity* gani za kuanzisha kiwanda gani. Katika hizo kuangaliwe miundombinu imeboreshwa? Je, kuna barabara za kwenda sehemu iliyyotengwa kuwekwa hicho kiwanda? Je, kuna maji? Je, kuna umeme? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu nachokiona hapa ni kwamba imefika hatua Tanzania sasa hivi tunafanya kazi kama maroboti. Inatamkwa watu wanakimbia, tunapata sifa kwamba tumeanzisha vitu hivi, je, tunaangalia *sustainability* yake au tunajua kuanzisha tu? Je, tumejifunza

vile viwanda vyote vilivyokufa viliuawa na nini? Je, kutokana na hapo tunajiwekaje vizuri ili hivi tunavyoanzisha visije navyo vikafa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa vile nina mfano mdogo tu, Kamati yangu ya *PAC* ilivyokuwa inatembelea viwanda mbalimbali nilipata *shock* kidogo nilivyofika kwenye Kiwanda cha Kibaha cha Kutengeneza Matrekta. Matrekta yale yamejazana pale ndani hayana soko na ukiuliza hakuna mtu anayejua hawa wanaotengeneza matrekta haya kutoka nchi za nje chini ya Wizara wamejitangazaje, yanajulikana au kuna mahali ambapo yamefanyiwa hata *testing* ili kuangalia ubora wake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema Mkoa wa Pwani una viwanda vingi, nafikiri hata hiki cha trekta kimewekwa lakini yamejazana ndani mle, hayafanyi kazi, hayajafanyiwa *testing* kuonesha kama yanahimili ardhi za kwetu. Kibaya zaidi ni kwamba hata watu kufundishwa bado hawajafundishwa *ku-assemble* tunategemea hao wenzetu kutoka nje, Wazungu ndiyo tunapanga mkakati wa kupeleka wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uone nchi yetu tunavyofanyakazi *upside down* kwamba Mkuu wa Nchi ametamka watu wote wanakimbia hatukai tukafaya *analysis*, kwanza tuka-evaluate huko nyuma tulikotoka tulikosea wapi na mkoa gani uko endowed kuweza kufanya kitu ambacho kweli kitakuwa *productive* kwenye nchi yetu kikawekewa miundombinu yote ili uchumi wetu ukaanza kukua kupitia pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia matrekta ya Suma JKT huko yalikopelekwa. Kwanza hayajulikani yamepelekwa wapi which means hata Wizara ya Kilimo hawajatathmini matrekta haya ya Suma yaliyokopeshwa watu mbalimbali yameweza je kuboresha kilimo badala yake tunaona kilimo ambavyo kimeanguka, mwaka hadi mwaka kilimo kinaanguka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dawa hizi za kuua viluwiluwi nya mbu na dawa hii inatengenezwa Kibaha, tumefika pale maboksi kwa maboksi yamejazana. Wakalalamika kwamba Halmashauri nydingi walishapelekewa au walishakopeshwa lakini ni kama moja au mbili ambazo zimelipa nydingine zote hazijalipa. Waheshimia Wabunge tuliokuwa nao wakasema kwenye Majimbo yao au Wilaya zao hawajui kama hata hiyo dawa ipo wala hawajui Halmashauri hizo walishachukua hizo dawa. Maana yake ni kwamba zimewekwa hapo Halmashauri, hazitumiki kuua viluwiluvi vile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa zile wanasema vile viluwiluvi vikishaota mabawa dawa ile haiwauwi, kwa hiyo inawauwa kwenye *septic tanks* yale maji machafu sasa *imagine* huko vijijini wangapi wana hayo matenki ya maji machafu, wengine vyoo vyao viko pembedi pembedi huko. Kuna wenzangu ambao vyoo vyao bado ni kwenye migomba, sasa sijui hiyo dawa au hicho kiwanda kitakuwa *sustained* kiasi gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachosema *with due respect* napenda sana tuijenge nchi yetu maana hii nchi ya watu wote, lakini kama tunafanya vitu kwa pupa, *talk of numbers* siyo *quality*, hatutafika popote. Tutakuwa na viwanda 10,000 au milioni *but at the end of the day* tunaweza kuona kwamba *return* ya zile *investments* ni zero. Sasa viwanda kama hivyo tunavi-sustain namna gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mfano kidogo tu kule kwenye Jimbo langu la Same Mashariki kuna Kiwanda cha Tangawizi. Kiwanda hiki sitatoa historia yake lakini nipende tu kusema *LAPF* wameungana na wakulima, wamechukua asilimia 60 ya *ownership* na wakulima asilimia 40, *well and good*. *LAPF* wamefikia hatua sasa hivi wanataka ku-*install* mashine kubwa, wameshapitia michakato yote ili kiwanda kianze kazi, sheshe linakuja barabara kwanza ya kutoka Mkomazi kwenda Same imekuwa historia miaka nenda rudi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inatumiwa na wananchi wa Majimbo kama manne au matano ya Korogwe Vijijiini, Mlalo, sehemu ya Lushoto, Same Mashariki na Same Magharibi. Barabara hii tumepeiga kelele miaka nenda rudi. Kilichonishangaza mwaka 2015/2016, Wizara ya Miundombinu ilisema imetenga pesa ambayo ilikuwa shilingi milioni 145 kwanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Mkomazi – Kisiwani - Same, hizo zilikuwa pesa za bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara ilitenga shilingi milioni 450 kwa ajili pia hiyo hiyo ya usanifu wa kina wa barabara hiyo, *total* ni shilingi 595 milioni kwa ajili ya usanifu huo, lakini mpaka leo hakuna hata kilometa moja ambayo imetengezwa. Sasa unajiuliza hivi hiki Kiwanda cha Tangawizi ambacho Mfuko huu wa Jamii wa LAPF wanataka waanze na ilikuwa waanze *soon mwezi* huu watapita wapi? Ukiangalia hata wakulima wenyewe miundombinu ya maji hawajatengenezewa, hiyo *production* ya kiwanda kikubwa watapata malighafi kutoka wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako mzuri.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Ndaki atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia na Mheshimiwa Aeshi, ajiandae.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kurejea kidogo kwenye Kitabu cha Wakristo kinachoitwa Biblia, Kitabu Kitakatifu kwenye Kitabu cha Nehemia, Sura ya 1-4. Nehemia alianza kazi ya kujenga ukuta wa Yerusalem. Wakati ameanza kujenga ukafika ngazi fulani walitokea watu waliokuwa wakiitwa akina Sanbalati na Tobia wakaanza kusema ukuta wenyewe anaojenga hata mbweha akipanda hapo unaanguka mara moja. Kwa hiyo, wakaanza kumdhihaki, kumdharaa na mambo mengine mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Rais mwenyewe wajenge ukuta wa Yerusalem, ni wakati wao sasa wa kujenga ukuta wa Yerusalem bila kujali makelele yanayopigwa na akina Tobia na Sanbalati, kwa sababu wakiwasikiliza hawataweza kufanya cha maana kwenye nchi hii, lakini huu ni wakati waou Mungu amewapa wafanye kazi ambayo iko mbele yenu kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa maana wakiendelea kuwasikiliza hawatafanya kitu; wakinunua ndege watasema ndege yenewe wanunuwa kwa *cash* wangekopa, wakikopa watasema wanaongeza deni la Taifa, wanaongeza mzigo kwa wananchi, wakijenga viwanda watasema viwanda vyenyewe vinavyojengwa ni mashine za kusaga unga na kadhalika, kwa hiyo, wakiwasikiliza watawatoa kwenye reli. Nawaambia viongozi wangu kwamba ni wakati wao mzuri, wajenge Taifa hili na wako kwenye mwelekeo mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, niende kwenye huduma za jamii hasa upande wa maji. Mkoa wa Simiyu tuna mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria; leo ni kama miaka mwili mradi huu ulishapitishwa lakini mgogoro upo kwenye eneo litakalowekwa tanki kubwa ambalo litasambaza maji kwenye Mkoa wa Simiyu kuanzia Wilaya ya Bariadi, Itilima, Meatu na Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali ambapo kutajengwa tenki hilo ni mahali ambapo kuna madini ya *nickel*, kizungumkuti kiko hapo. Mheshimiwa Rais aliwahi kuja Mkao wa Simiyu, akasema tenki lijengwe kwenye Mlima Ngasamo mahali ambapo mwekezaji anataka kuchimba *nickel*, lakini bado uamuzi wa kujenga tenki hilo haujafanyika. Sasa sielewi tumsikilize nani Mheshimiwa Rais, mwekezaji au nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia kibali kinatafutwa kutoka kwa Kamishna wa Madini, sasa huyu Kamishna wa Madini anakaa nchi gani kwamba ameshindwa kuandika kibali ili mkandarasi aweze kuanza? Maana najua mkandarasi alishatafutwa, amepatikana na pesa zipo lakini kazi haifanyiki leo ni kama mwaka mmoja na zaidi mradi huu haujaanza. Naomba sana mradi huu wa maji sasa uanze na kama ni kibali kinachotakiwa kutolewa kutoka kwa huyo Kamishna wa Madini, basi kifuatiliwe haraka kipatikane ili mradi uweze kuanza na sisi watu wa Mkao wa Simiyu tuweze kupata maji yaliyo safi na salama na ya uhakika zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la huduma za kiuchumi lakini niende moja kwa moja kwenye awamu ya tatu ya Mradi ya *REA*. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Kalemani pamoja na Naibu wake kwa sababu wanajitahidi sana kuhakikisha kwamba *REA* awamu ya tatu inafanya kazi yake kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nina tatizo kidogo kwenye Wilaya yangu ya Maswa mkandarasi aliyepangwa Mkao wa Simiyu ambaye pia yupo Wilaya ya Maswa amepewa kilomita kidogo kulinganisha na vijiji alivyonavyo. Utakuta kwenye vijiji anapokwenda kuweka umeme anaweka kitongoji kimoja kwa sababu anasema kijiji hiki nimepewa kilomita moja na nusu au kilomita mbili, kwa hiyo, inatosha kupeleka umeme kwenye kitongoji kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imezua ugomvi kwenye vijiji vyetu, kitongoji kimoja kinapata umeme vitongoji vinne

kwenye kijiji hicho havipati umeme. Wananchi kwenye vijiji vinavyobaki wanauliza wao ni wananchi wa nchi gani? Wanauliza wao ni wananchi wa wapi mbona kitongoji kimoja tu kinapata umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana mikataba hii ambayo Wizara ya Nishati wameingia na wakandarasi hawa hebu iangaliwe upya, vinginevyo itaacha ugomvi mkubwa kwenye vijiji vyetu kwa sababu maeneo machache tu yatapata umeme na maeneo mengine yatakuwa hayajapata umeme sasa inatuletea ugomvi sisi viongozi tunakuwa kama tumewabagua watu wetu. Kwa hiyo, naomba sana suala hili liweze kuangaliwa hasa kwenye REA awamu ya tatu hii inayoendelea lirekebishwe kwa haraka ili kwamba kama umeme unaenda kwenye kijiji basi uende kwenye vitongoji vyote. Hii habari ya kilomita mbili kwenye kijiji haitusaidii itatuletea ugomvi mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la sekta binafsi lakini upande wa wafanyabiashara. Nashukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu amekwishakutana na wafanyabiashara wa nchi hii na kuzungumza nao kujaribu kutatua changamoto ambazo wanazo. Najua hakika ya kwamba kuanzia Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Rais mwenyewe wana nia nzuri kabisa na wafanyabiashara, lakini tatizo liko kwa watendaji wa Serikali katika kutekeleza maelekezo na kazi wanazotakiwa kuzifanya ili biashara ziweze kwenda kwenye nchi hii. Watendaji wa Serikali sijui hawaelewi kitu gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wafanyabiashara kutoka kwenye Wilaya yangu wanafanya biashara ya ng'ombe wanavusha ng'ombe kutoka kwetu kwenda Dar es Salaam wamefika hapa Dodoma wanasmamishwa halafu wanaulizwa leseni yenu iko wapi, leseni wanaionesha, kisha wanaulizwa mwenye leseni yuko wapi, mwenye leseni hayupo tunawapiga faini Sh.500,000. Sasa najiuliza mwenye leseni ya kupeleka ng'ombe Dar es Salaam naye apande kwenye gari ambalo limepakia ng'ombe? (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu ambavyo kwa kweli havieleweki kwa hawa watendaji wetu. Huyo mwenye kufanya hiyo biashara na mwenye leseni ana watu wake wanaowasafirisha wale ng'ombe na yeye mnataka apande kwenye hilo roli?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Said Maulid Mtulia na Mheshimiwa Aeshi na Mheshimiwa Mary Deo Muro, ajiandae.

MHE. ABDALLAH S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa na mimi kuwa sehemu ya wazungumzaji siku ya leo. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima wa afya njema na kuwepo kwenye Bunge hili Tukufu nikapata fursa ya kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge nimeapishwa juzi tu hapa, nimeingia kupitia dirisha dogo na mara nyingi wachezaji wanaosajiliwa katika dirisha dogo ni wachezaji wazuri sana. Nikishukuru Chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa hatimaye kuwagaragaza jamaa zetu kule na kupata ushindi wa kishindo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano Dokta John Pombe Magufuli, mimi namuita *field marshal*. Niliwaambia kuwa nampenda balaa na nampenda kweli kweli kwa namna anavyochapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijafanyaawa nisipomshukuru mama yetu, Mheshimiwa Samia, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyomsaidia Rais wetu kutekeleza majukumu yake. Pia sasa nikushukuru wewe Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo imetoa mwelekeo wa namna gani Serikali yetu katika mwaka wetu huu mambo yatakavyokuwa mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana Kinondoni wana matumaini makubwa sana na bajeti hii ya mwaka huu. Wana Kinondoni tuliwaeleza kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli ni Serikali ambayo imedhamiria kuleta maendeleo kwa Watanzania wote na wao ikiwa ni sehemu ya Watanzania. Niwaahidi wana Kinondoni kwamba uchaguzi umeshakwisha, tumepata ushindi unatosha na wote wawe kitu kimoja kushirikiana na Mbunge wao kuhakikisha wanaleta maendeleo katika Jimbo lao la Kinondoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze tu ndugu zangu wa kipande cha kule kwamba uamuzi nilioufanya Katiba ya Chama nilichokuwa nipo kule unaruhusu na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaruhusu. Kwa sababu na wao siku hizi wamekuwa waumini wakubwa wa kutaka Katiba basi jambo hili wasilonee, usichokila usikitie hila, kwa maana kwamba, tumefanya kwa mujibu wa Katiba na siye ni waumini wa Katiba tusiwe na maneno maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine watazungumzia gharama hapa, uchaguzi umegharimu bilioni sita lakini siye au nyie siyo ndiyo mnataka twende kwenye Katiba Mpya, hivi Katiba Mpya tukiingia kwenye hiyo kura ya maoni hatutotumia gharama? Hivi gharama yake itakuwa ndogo kuliko hiyo bilioni sita? Kama tunataka kweli kuwa waumini wa Katiba tuanze kuishi kwa mujibu wa Katiba tusianze kusemana kwa mtu ambaye amefanya maamuzi ambayo yanatekelezwa kwa mujibu wa Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri tu, ushauri wa kwanza kwa chama changu kile kilichonilea kwamba kibaya chako chema kina wenyewe. Ushauri wa pili kwa Chama Kikuu cha Upinzani, CHADEMA waache kulialia wagangamale, kulonda kazi ya Jeshi kugangamala. Kama umeingia kwenye uchaguzi umepigwa unafanya tathmini unajipanga kwa ajili ya uchaguzi ujao. Mwisho wa uchaguzi ndiyo mwanzo wa uchaguzi mwagine, tuonane 2020 na *Inshallah* Maulid Mtulia mtamkuta pale pale Kinondoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu chapa kazi. Chama cha Mapinduzi ndiyo chama chenye Serikali na ndiyo chenye jukumu la kuhakikisha maendeleo yanafika kwa wananchi wa Tanzania na wengine jukumu lao ni kukosoa, kushauri, lakini bahati mbaya sana hili la kukosoa ndiyo wanalipenda, kwa hiyo usishangae wakija na maneno ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jamaa yangu mmoja mtani wangu anatoka hapa Ifakara, anakebehi kununuliwa ndege, basi *okaywewe* watu wako hutarajji kupanda ndege basi hata Daraja la Kilombelo hujalionia? Hata ile barabara inayojengwa kutoka Ifakara - Kidatu nayo hujaiona? Kwa hiyo, watu kama hawa wasimtoe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye lengo la kuwatumikia Watanzania na kuwaleta maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kinondoni katika kuhakikisha tunatunza mazingira, tunainua uchumi wa wana Kinondoni na kuhakikisha tunashirikiana na Serikali kuleta ustawi tumekuja na mradi mkakati wa kuhakikisha *Coco Beach* tunaiendeleza. Tunahitaji Serikali itupatie pesa shilingi bilioni 7.2 ambayo tuna uwezo wa kuirejesha ndani ya mwaka mmoja. Tafsiri yake nini? Tafsiri yake ni kwamba kila baada ya mwaka mmoja tuna uwezo wa kutumia hicho kama chanzo cha ndani cha kuingiza shilingi bilioni 7.2. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuliahidi kwamba tunataka kujenga barabara na sisi Dar es Salaam na hasa

Kinondoni tunatarajia sana kwamba barabara zetu zitajengwa. Tuna magari mengi na tunapojenga barabara na kuondoa foleni kiuchumi magari haya yanaweka mafuta na tozo ya mafuta sasa hivi ndiyo inaingia moja kwa moja kama kodi, maana yake magari yatakapotembea sana mafuta yatatumika sana na tutapata kodi sana. Kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha tunaondoa foleni katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna suala la masoko. Niishukuru Serikali imetutengea shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya soko letu la kisasa la Magomeni, lakini vilevile itenye pesa kwa ajili ya soko la Tandale ambalo ndiyo soko kubwa la chakula Dar es Salaam, pia na soko la Makumbusho na Mapinduzi ambayo ni masoko makubwa Dar es Salaam. Tukiyafanya haya yote, tutaongeza ajira kwa watu wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Rais amehimiza kwamba wawekezaji wetu wa ndani na hasa katika masuala ya dawa na vifaa tiba wapewe kipaumbele. Mimi nina mwekezaji pale Jimboni kwangu, mpiga kura wangu ana kiwanda cha vifaa tiba pale Mwananyamala kinatengeneza gozi, hakijapata kupewa kipaumbele na badala yake *MSD* bado wanaendelea kununua kutoka nje. Sasa hii ndoto ya Mheshimiwa Rais tutaifika lini? Naomba sana ...

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. ABDALLAH S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Aeshi atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Deo Muro na Mheshimiwa Desderius Mipata ajiandae.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjalilia Mheshimiwa Spika

wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kurudi salama na kuja kuwatumikia wananchi wa Jamhuri wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya kuwatumikia wananchi hawa. Nisiwe mchoyo wa fadhila kutoa shukrani kwa Wabunge wote walio humu ndani kwa heshima kubwa waliyonayo mbele ya Waziri Mkuu ndiyo maana unaona Bunge letu hili sasa hivi liko salama salmini. Laiti isingekuwa mahusiano mazuri na Waziri Mkuu leo hii Mawaziri wengine tungeshikana mashati humu ndani ngumi zingeruka, lakini haijawahi tokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee mambo machache sana lakini yanayohusiana na Mkoa wangu wa Rukwa. Kama inavyojulikana sisi tunatoka Nyanda za Juu Kusini lakini zao letu kubwa ni mahindi. Nimeiona bajeti *NFRA* waliomba shilingi bilioni 86 lakini Wizara ya Fedha imetenga shilingi bilioni 15. Ni nini dhamira ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusiana na hawa wakulima wanaolima zao la mahindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa wakiongelea mambo mengi, nimeona wakiongelea kilimo cha pamba, korosho, katani, tumbaku lakini bila kulima mahindi hawa wanaolima tumbaku watakula nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli *NFRA* wametengewa shilingi bilioni 15 na naamini shilingi bilioni 15 zinatosha tu kwenye Wilaya moja tena Wilaya ya Sumbawanga Mjini kwa mahindi ambayo tunalima kwa wingi. Sasa ombi langu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ananisikiliza, endapo Serikali haitakuwa na uwezo wa kununua mahindi haya ambayo wakulima wameyalima basi Serikali isifunge mipaka, iache mahindi yawe huru kila mtu akauze anapotaka kwa sababu mwaka jana mlifunga mipaka mlikuja kufungua mipaka dakika za mwisho kwa masharti makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilimfuata Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na kumweleza kuna wakulima au wafanyabiashara wadogo wadogo wenye gunia 10 au 15 wanataka kuvuka kwenda Congo, Kigoma leo hii mwambao wa Lake Tanganyika imekuwa ni rushwa kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ananisikiliza; kama hawana uwezo wa kununua mahindi wawaacie wakulima wakauze mahindi wanapotaka. Watakuja hapa kama alivyosema Mheshimiwa Bashe mwaka huu, watazuia tena mahindi tusipeleke nje ili waweze kusingizia kwamba, hakuna mfumuko wa bei, wanawaumiza wakulima, hawana soko la kuuza mahindi yao, matokeo yake wamemweka mkulima ndiyo ngao ya kuhakikisha wananchi wa Tanzania hawafi na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si kazi ya mkulima, ni kazi ya Serikali kuhakikisha mkulima au mwananchi wa Tanzania hawesi kufa na njaa, mkulima mnambania kila eneo, kila sehemu na vikwazo juu ya vikwazo. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri kwa kweli mwaka huu kama itatokea wanafunga mipaka mimi nitakuwa wa kwanza kushikana mashati humu ndani ya Bunge hili Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sambamba na kilimo kuna mateso mengine yanawapata wavuvi wa Ziwa Tanganyika. Hawa Mawaziri mimi sijui Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ulega tulimtegemea sana kama Mbunge kijana na Naibu Waziri kwamba atakuwa kimbilio la wavuvi; matokeo yake amekwenda kule amekutana na Waziri mwingine kazi yao imekuwa kuwaadhibu tu wavuvi, choma nyavyu na mitumbwi, nyanga'anya huyu, piga faini huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu niambie huyu mkulima anateseka, mvuvi anateseka nani kimbilio letu sisi wakati wa uchaguzi? Semeni tu maana imekuwa ni matamko tu, nafikiri kuna kasoro au tatizo ndani ya Wizara zetu na nafikiri labda kuna baadhi ya Mawaziri wanataka kumhujumu Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ana dhamira njema sana lakini kila kukicha nyavu zimechomwa, maboti yamechomwa, faini kubwa, mkulima hana pa kuuza mahindi, Mheshimiwa Tizeba ameinuka mbolea hakuna, yaani tabu juu ya tabu, vitu vinapandana siku hadi siku hakuna unafuu wowote kwenye hizi Wizara mbili, ni mateso juu ya mateso mpaka hata ngo'mbe wenyewe wanateswa sasa hivi wanapigwa mihuri siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Tizeba na Waziri wa Mifugo, hebu watupe afueni kidogo, tupumue sisi huko tunakotoka, matokeo yake sisi ndiyo tunaotakiwa kuwatetea, sasa tunakuwa tukiongea siku hadi siku na hawatusikilizi, matokeo yake tunakuwa kama tunaimba nyimbo bila sababu yoyote ya msingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nlongelee barabara ya kutoka Sumbawanga – Tunduma, hajjawahi tokea, ina kilometra 234 lakini ina matuta 240, matuta ni mengi kuliko kilomita tulizokuwa nazo kutoka Tunduma - Sumbawanga. Nataka nitoe mfano tu, Mheshimiwa Mipata alitoka India kufanyiwa operesheni ya mgongo ametua na ndege pale *Airport Songwe* kapanda gari kufika Sumbawanga mgongo umemrudia tena kutohana na matuta yalivyokuwa mengi kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ananisikiliza, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu sijui ananisikia au wanaongea, sijajua; matuta yamekuwa mengi, tumwombe sana Mheshimiwa Waziri wajaribu kupunguza matuta haya, ni kero kubwa kuliko ambavyo tulitegemea kupata barabara ya lami yenye manufaa na wananchi. Sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hilo alichukue na alifanyie kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kuhusiana na meli, *Lake Tanganyika*. Kila nikisikia hapa nasikia Mwanza meli mpya, tishali jipywa, hivi *Lake Tanganyika* tumerogwa? Tuna meli toka uhuru mpaka leo hatuna meli nyingine yoyote ile. Wananchi hawa wanateseka mno na ukiangalia ile meli kwa

kweli hata ng'ombe hatakiwi kupanda kwenye ile meli lakini leo kila kitu kinaachwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu afanye ziara siku moja aende akaitembelee ile meli aone athari zake na uchakavu wake ulivyokuwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kiwanja cha ndege. Tumekuwa na mvutano wa muda mrefu sana lakini uwanja wetu wa ndege naamini ukikamilika utaleta tija kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa hususan Jimbo la Sumbawanga Mjini. Tunapokuwa na kiwanja cha ndege na ndege zetu ambazo sasa hivi zimepatikana zikifika Sumbawanga tutarahisisha hata wawekezaji kufika ndani ya mikoa yetu na hata watalii kuja kwenye mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka juzi tumepitisha bajeti ya kujenga uwanja, bajeti ya mwaka jana tumepitisha tutajenga uwanja, bajeti ya mwaka huu nimeona tunajenga uwanja, sasa sijajua labda ni uwanja mkubwa sana kuliko wa Dar es Salaam au ni uwanja mkubwa kuliko Dodoma kwa sababu kila mwaka tunapitisha bajeti, ifike wakati iwe mwisho. Kama bajeti ya mwaka huu itapita watuambie sasa wananchi wetu wasubirie uwanja wa ndege kama utajengwa au hautajengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa kubwa tunalolililia sisi, wale wananchi wanaozunguka uwanja wa ndege toka wamefanyiwa tathmini ya malipo huu ni mwaka wa kumi wakati huo bei ilikuwa iko chini leo hii vifaa vya ujenzi vimepanda, viwanja vimepanda, sasa sijui fidia hii tutawalipa kiasi gani. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ifike mahali wananchi hawa ni wa kwetu sisi na sisi ndiyo tunaowatetea. Tuwe na moyo wa imani jamani, Mungu ametufundisha tuwe na upendo, tusali, tuombe Mungu, tuwasaidie na wale wasiokuwa na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya wanapokuwa Mawaziri wanajisahau na bahati mbaya sana wakiwa huko sijui huwa kuna kitu gani kinapita, huwa wanajisahau kabisa kama na nyie ni Wabunge kama sisi. Wakirudi nyuma huku ndiyo wanaanza kuomba miongozo

na kadhalika, lakini wakiwa huko wanajisahau kabisa, Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aangalie suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nitawazungumzia watumishi hawa wa darasa la saba kama walivyosema Waheshimiwa Waunge wenzangu. Sumbawanga tuna dereva anaitwa Mapugilo ambaye alishawahidi kumwendesha Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya, kamwendesha vizuri, kaendesha Mawaziri wengine vizuri, kamwendesha Mkuu wa Mkoa, Waziri Mkuu Mstaafu, akija Sumbawanga gari la Mkuu wa Mkoa analotumia anayemwendesha ni Mapugilo, darasa la saba, lakini leo wameenda kuwatumbua, leo hii wamefukuza madereva wengi wa darasa la saba ambapo naamini kabisa udereva sio elimu, udereva ni ujuzi. Dereva anaweza kukuendesha hata kama hajui kuandika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, naamini kwa hili wanalisikiliza, warudisheni watu hawa. Warudisheni Watendaji wa Vijiji ambao wenyewe tuliwaajiri kwa cheo cha darasa la saba. Jamani tuwe na imani, hawa tunaowaonea ni binadamu kama sisi, inawezekana kwa njia moja au nytingine hatujui au hatuna ndugu ambao wanateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukimwangalia Mapugilo hana nyuma hana mbele, kafanya kazi leo mwaka wa 50 bado miaka mitano astaafu leo hii tunamfukuza, hivi kweli utu uko wapi? Wakulima shida, wafanyabiashara shida, madereva wa darasa la saba shida...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Mary Deo Muro na kwa kutegemeana na muda Mheshimiwa Mipata.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami nina machache, najua mengi sana wameongea wenzangu lakini kuna machache ambayo ningependa kuongezea. Nafahamu kwamba kazi ya Bunge ni kuwatumikia wananchi na ni kwa ajili ya ustawi wa wananchi. Kama hivyo ndivyo basi, ina maana kwamba wananchi wangefurahi sana kuona kwamba tunawatetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu moja tu. Huko mitaani sasa hivi wastaaafu wana shida kubwa sana. Wastaaafu waliostaafu tangu mwaka jana mwezi wa Julai hawajalipwa mafao yao mpaka sasa hivi. Nyumba hiyo unakuta baba na mama wamestaafu, nyumba hiyo hiyo ina vijana ambao wamesoma mpaka chuo kikuu lakini hawajaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba Serikali inashughulikia ustawi wa wananchi lakini tuangalie jinsi ambavyo wastaaafu hawa hawatendewi haki. Mstaafu anaenda kwenye Ofisi za Serikali kufuatilia mafao yake anaambiwa tunalipa waliostaafu mwezi wa Aprili, ni lini Serikali imeanza kuweka foleni ya wastaaafu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu nina watu ambao ni jamaa zangu, majirani, wanajamii na wapiga kura wangu ambao wamestaafu mwezi wa saba mpaka sasa hivi ninavyoongea hawajalipwa mafao yao, wataishije? Januari wameshindwa kupeleka watoto shule sababu ni kwamba hajapewa mafao. Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa mafao kwa wakati na sheria za ajira zinasema nini juu ya mfanyakazi anapomaliza kipindi chake cha kutumikia Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tuna nia ya dhati ya kuinua uchumi huyu mtu ambaye tangu Julai mwaka jana hajapewa mafao yake, angekuwa amepewa angekuwa amejiendezea kiasi gani? Tuna nia kweli ya kupunguza umaskini, hivi kweli Serikai itapunguza umaskini kwa njia hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kabisa sisi ni Wabunge, hivi leo hii kama tungefika 2020 halafu tuambibiwe kwamba mafao yetu tutalipwa 2021 tungekubali? Nauliza Wabunge ambao tupo kwenye Bunge hili, tungekubali 2021 ndio tulipwe mafao yetu? Kwa nini tunawafanya hivi wananchi ambao wametutuma mahali hapa kuwatumikia? Kwa nini hatuwasemei na kwa nini Mawaziri wanaohusika wanajua kabisa kwamba wafanyakazi hawa ambao wamelitumikia Taifa hili wameweza kutoa nguvu zao na muda wao, wamemaliza vyema lakini wanashindwa kuwapa stahili zao. Mtu anastaafu mwezi wa Julai, huu ni mwezi wa Aprili, hajapewa hata mafao yake, anaishije? Wanapata *depression*, wanakufa vifo ambavyo havitegemewi. Kwa nini lakini Serikali inafanya hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie sheria zinasema nini na kinachofanyika ni nini? Je, hizi foleni ni mpango wa Serikali, ni Serikali haina fedha za kuwalipa au vinginevyo vyovoyote vile atuambie ili tuweze kuelewa na tukawaambie kwamba Serikali sasa hivi inapangisha foleni wastaafu kwa sababu haina hela na kama hela zipo za kufanya mambo mengine kwa nini hazipo za kuwalipa wastaafu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niongee kuhusu elimu. Watu wote wameongelea kuhusu elimu lakini nilisikia siku moja Mheshimiwa Mkapa anasema kwamba tukae tuzungumze elimu inaenda wapi, tunaelekeea wapi na elimu. Nami nataka niulize swali kwa sababu najua kabisa Waziri wa Elimu yupo hapa, atuambie, kuna kitu nilikisikia mijadala ikiendelea juu ya wanafunzi kukariri, tunaambiwa kwamba wasirudie madarasa. Naomba nipate ufanuzi, hivi kama mwanafunzi amefika darasa la nne amefeli halafu anaendelea la tano huyo tunazalisha wasomi wa aina gani miaka ijayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kujadili mijadala ambao uwazi kabisa na nini hasara ya kumfanya mwanafunzi akariri? Kama akirudia darasa Serikali inapata hasara gani badala ya kupata faida kupata mtu ambaye ni

bora? Ni kwa sababu ya elimu bure tunataka wasiendelee kuwa wengi kwenye madarasa hayohayo wakati wengine wanaingia? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itoe jibu ambalo litakuwa makini tuelewe kabisa kwamba Serikali inasema wanafunzi wasikariri kwa sababu inaogopa gharama itakayoingia kwa sababu itakuwa na wanafunzi wengi au sababu yoyote ya msingi ambayo itaonesha kwamba ni kweli Serikali imesema hivi kwa sababu hizi na hizi, vinginevyo tunaomba wakati ana-*wind up* atuambie ni nini kinataka kufanyika kwa Serikali na hii elimu kweli tuna nia ya dhati na elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulisoma, tulikuwa tunarudia mpaka mara sita, tuko hapa leo hii tunasema watoto wasirudie, darasa la nne aende mpaka la saba. Halafu akishafika la saba hajui kusoma na kuandika, akishakuwa hajui kusoma na kuandika anafanya nini au anakuwa wa kitu gani? Ningependa kusisitiza Serikali ipambanue huo mjadala unaoendelea. Kama kweli ni kutokukariri watupe sababu, kama kuna kukariri tutashukuru kwa sababu ndivyo tunavyohitaji iwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuongelea ni kwamba, bajeti ya mwaka jana tuliongelea kwamba tunahitaji tozo ile ya mafuta lende kwenye maji. Ni jambo jema na tuliona nijema kweli, lakini kama imeshaenda tangu wakati huo, hatujui kwamba ilienda ngapi kwa sababu hatujaona imeenda ngapi lakini cha muhimu ni kwamba ikienda kule inafanya yale matarajio na kama haifanyi yale matarajio sababu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa kwangu mimi kule Kibaha, niliandika swalii kuuliza kwamba miradi ya Kibaha inajengwa chini ya kiwango, wananchi wa Kibaha wanakosa maji siyo kwa sababu hela hazijatolewa. Ilitolewa shilingi milioni 531 mradi wa maji, vikao, imepotelea yote porini kwa sababu mabomba yamewekwa mabovu na hayako kwenye viwango, badala ya kuweka *connector*

kachomelea moto, sehemu nyingine kafunga mipira ikawa maji yanamwagika, mradi ukakataliwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukataliwa na wananchi ukarudishwa Halmashauri, wana miezi nane mpaka sasa hivi watu wa Vikawe hawapati maji, lakini Serikali ilishatoa shilingi milioni 530 lakini zimepotea kwa sababu watendaji wamekula zile hela. Tangu siku ile niliyosema Serikali haikufanya kitu chochote mpaka sasa hivi ninaposema ni miezi nane, ukienda Vikawe hakuna maji na shilingi milioni 531 zilishaliwa, tunaelekea wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la wajasiriamali wadogo wadogo wanaoinua maisha yao. Kwa kweli Waziri wa Viwanda alisema kwamba tuanzishe viwanda vidogo vidogo, wanawake wajasiriamali wameanzisha, wengine wanasindika *spices* lakini tatizo ambalo limetokea ni kwamba tozo ndogo ndogo kwenye viwanda vidogo vya wajasiriamali ni nyingi mno. Mtu anatengeneza *spice* anaambiwa anatakiwa apate usajili *TFDA*, anatakiwa aende *OSHA*, anatakiwa aende *TBS*, wote hao wanachukua hela za huyu huyu mjasiriamali mdogo ambaye ndiyo kwanza anahangaikia maisha yake tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hivi vitu vyote visiwekwe pamoja gharama zipunguzwe ili hawa wajasiriamali waweze kupata faida. Inafikia mahali wajasiriamali wanakata tamaa, wanaona kwamba hawapati kitu chochote. Tutaendelea kuzalisha maskini kwa sababu tu Serikali imeweka mlolongo wa tozo ambazo zingeweza zikawekwa pamoja na zikaleta faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ningependa kuzungumzia jinsi ambavyo viwanda tumevipokea sawa, kuna mwenzangu mmoja ameongelea, lakini kuna tatizo ukaguzi wa viwanda na shughuli zinazofanywa katika viwanda hivyo. Hawa vijana wetu tumesema watapata ajira, sawa, lakini mwisho wa siku tunazalisha magonjwa ambayo Serikali itaingia tena hasara ya kutibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kiwanda pale Kibaha kinazalisha sabuni, vijana wameajiriwa lakini hamna vitendea kazi, hamna *mask*, wanafanya kazi vumbi za sabuni zote zinaishia kwa vijana hawa. Vijana hawa wanaishia kuwa na *TB...* (*Makofii*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Desderius Mipata.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima anaotujalia. Nichukue nafasi hii pia kuishukuru Serikali, Mheshimiwa Rais na uongozi wa Bunge kuniwezesha kwenda kutibiwa India na leo nimepona. Najisikia niko vizuri, namshukuru sana Mungu. Naishukuru sana Serikali yangu kwa huruma hiyo na sasa niko kazini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema kabisa naunga mkono hotuba iliyotolewa na Waziri Mkuu hapa mbele yetu kwa sababu imejaribu kuangalia maeneo muhimu mengi. Kusema kweli Waziri Mkuu na viongozi wanaomsaidia akiwemo Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mawaziri wengine, wanafanya kazi vizuri na wanatusikiliza vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja chache ambazo naziwasilisha hapa Bungeni. La kwanza, ni suala la shamba la Milundikwa ambalo nimekuwa nikilizungumza sana katika Bunge hilo. Shamba hili lilikuwa la Serikali na lina ukubwa wa ekari 26,500 baada ya kuacha shughuli zake wakaja Jeshi kwa muda. Wanajeshi walikuja mwaka 1994 baadaye walismamisha shughuli zao na kuwaachia wananchi. Shamba lile liligawanywa katika vijiji mbalimbali, Kijiji cha Milundikwa kilipewa ekari 12,000, Kasu walipewa ekari 6,000, Kisulu walipewa ekari 2,000, Malongo walipewa ekari 1,000 na zikawa zimebaki ekari 5,500, tukashauriwa eneo hilo libaki kuwa eneo la Halmashauri tuendeleze utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kwa busara na namna walivyofanya wakaamua eneo hili kuanzisha Sekondari ya Milundikwa ambayo nayo nilipigia kelele sana hapa kwamba Serikali ilitwaa, lakini lazima nishukuru kwamba Serikali ilikwishatoa pesa nyingi zaidi ya shilingi milioni 360 na sasa tunaendeleza sekondari nyingine japo miundombinu bado haijatosha, tutaendelea kuomba Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu ni nini? Wanajeshi walivyoingia kwenye eneo hili sisi tulidhani watachukua eneo hili la ekari 5,500 ambalo lilibaki kwa Halmashauri badala yake wamedai eneo lote lililokuwa shamba la Milundikwa ambalo wananchi wa vijiji nilivyovitaja vyote walipewa kwa barua na kwa maelekezo ya mkoa na mimi wakati huo nilikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilienda kutembelea kwenye vijiji hivi ni kilio, wananchi hawana mahali pa kulima na wamefukuzwa katika maeneo yao, wamebakwa na ekari 4,000 tu. Kwa hiyo, takriban wananchi 5,000 hawana mahali pa kulima na ni wakulima. Habari hii nimewahi kuipeleka kwenye Ofisi yake Mheshimiwa Waziri, nimeshapeleka pia Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo hili nimekuwa nalizungumza peke yangu siaona kama naungwa mkono na mtu yejote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nimejaribu kuliongea kwenye vikao vya mkoa, nikaambiya nisiendelee kuongea hilo ni uamuzi wa Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais kwanza ni mtu mwenye huruma. Inawezekana sisi wote hatusemi lugha moja, tukilifafanua jambo hili na athari zinazoonekana kwa wananchi, naamini kabisa Mheshimiwa Rais ataona umuhimu wa kuligawa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanajeshi hatuwakatai wapate eneo lao na wananchi ambao ni wapiga kura wetu lakini ndiyo wakulima na hawana namna nyingine ya kujikimu ni kutegemea kilimo waweze kupata eneo la kulima. Naomba hili lichukuliwe kwa umuhimu wa pekee kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la elimu. Wilaya yetu ya Nkasi chini ya Mkuu wetu wa Wilaya Said Mtanda, wengi wanamfahamu, tumekuja na sera ya kuitikia kwa vitendo elimu bure. Tumejenga madarasa matatu matatu kwa kile eneo ambapo kuna shule ya msingi na sasa tuna madarasa zaidi ya 348, lakini wananchi hawana uwezo wa kuezeka, wananchi wameshaitikia vizuri, wametimiza wajibu wao. Naiomba Serikali, kwa namna yoyote mtakavyoweza kutusaidia ili wananchi wasivunjike moyo tuweze kumaliza kuezeka madarasa haya ili yaweze kuleta maana ya kuhamasisha wananchi wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la lingine ni afya. Nchini kwetu kuna sera mbalimbali na nashukuru sana jana katika swalilangu, kusikia kwamba Serikali imekubali sasa ombi letu la muda mrefu mimi na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Ally Keissy la kujenga Hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Nkasi. Jambo hili ni faraja kwetu, tumelipokea vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado vituo vya afya tumekuwa tukivijenga kila mahali. Kwenye Jimbo langu wananchi wanajenga vituo vya afya vinne, tumewahamasisha. Licha ya ahadi tulioipata jana lakini bado kuna vituo vya afya vitatu na zahanati zaidi ya 15, zote hizi tumewahamasisha wananchi na sasa wanatimiza wajibu wao, lakini tunaomba Serikali iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la umeme. Katika vijiji vyetu imeonekana tutapelekewa umeme katika vijiji karibu vyote lakini wakandarasi wamechelewa. Kuna eneo muhimu sana ambalo nafikiri kama inawezekana wakandarasi waanzie ambapo ni Vijihi vya Sintali, Nkana na Mkunachindo. Vijihi hivi vilisahaulika mara ya kwanza, vikisaulika mara ya pili tena inaweza kuwa sio vizuri sana. Naomba sana hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya watumishi ambao leo hii tunaambiwa utumishi wao usitishwe kwa sababu wana elimu ya darasa la saba. Jambo hili ni maumivu makubwa sana. Nikiwa Mwenyekiti wa

Halmashauri karibu miaka 17, nimeshirikiana na hawa kujenga Wilaya ya Nkasi, kujenga zaidi ya sekondari 23 na sasa niko Mbunge, naendelea kushirikiana nao. Unapowaambia wanaondoka bila kufahamu au kutambua juhudini ambazo wamechangia kwenye maendeleo ya Wilaya, Serikali na wananchi kwa ujumla hii ni dhambi. Hivyo, naiomba Serikali hii siku na yenye huruma iweze kuliangalia suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo kwetu ndiyo *alfa* na *omega* na kwenye hotuba hii nimeona maendeleo ya kilimo na juhudi zinazofanywa na Serikali ikiwemo kuunganisha matrekta. Ni juhudi nzuri zinazotupeleka kwenye kilimo ambacho kitaleta tija zaidi kwa sababu tunatumia mashine. Hata hivyo, uunganishaji huu ungefanyika hata Mkoa wa Rukwa ambako tunalima, pengine ingependeza zaldi kulikoni tunafanya sehemu ambayo hata killimo hakifanikiwi vizuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile changamoto za kilimo amezieleza mwenzangu hapa ni kwamba sisi Mkao wa Rukwa msimu wetu wa kulima unaanza Oktoba, mbolea tunapata mwezi Februari, suala hili ni kilio kwa wakulima. Nilifanya ziara hivi karibuni, kwa kweli ni kilio. Naomba Waziri na Serikali itambue, nchi hii ni kubwa, inawezekana hatujui misimu mbalimbali, sisi kwetu tunahitaji pembejeo zitufikie Septemba ndiyo tutaweza kufanya vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mtuhakikishie pembejeo hizi zinapatikana kwa wingi. Mwaka huu pamoja na Mheshimiwa Rais kuingilia kati jambo hili lakini bado pembejeo ziliisha ikabaki wakulima wanalima bila pembejeo na sasa hivi sisi Mkao wa Rukwa chakula hakitakuwa kingi sana kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile masoko ni muhimu sana. Tulitembelea Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko huko Iringa, pamoja na majukumu mengine kumbe kuna jambo muhimu ambapo ingeweza kuwasaidia wakulima. Wajibu wake ni pamoja na kutafuta...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa leo ndiyo tunafikia tamati ya shughuli zetu za leo. Niliwapa tahadhari mapema kwa sababu ya maombi ya mwongozo na taarifa, yote hayo ni kheri lakini yana kula muda. Upande wa kulia kwangu kuna orodha ya Waheshimiwa Wabunge, nina majina kama manne na upande huu wapo watatu/wanne lakini ndiyo hali hiyo. Muda wakati wote si rafiki lakini nashukuru kwa michango yenu na kwa kazi nzuri tuliyofanya.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili. La kwanza linahusu wageni tulionao hapa.

Kundi la kwanza, tuna wageni 137 wa Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambaao ni Waheshimiwa Mameya, Wenyeviti wa Halmashauri pamoja na Makatibu wa Kamati wa Mamlaka wa Serikali za Mitaa kutoka mikoa mbalimbali nchini, karibuni sana. Mmeona shughuli zinazofanywa na Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa hapa, lakini pia hao hao mnakuwa nao kwenye vikao vyetu vya Halmashauri. (*Makofi*)

Kundi la pili, ni wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambaao ni wageni wawili wauguzi kutoka Wilaya ya Mkuranga, Mkoani Pwani. Nao ni Sister Pili Ndauka Muuguzi Mkuu Wilayani Mkuranga na Sister Grace Zephaniah Muuguzi Mkuu Kitengo cha Mama na Mtoto Wilayani Mkuranga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulikuwa nao leo. Matangazo mengine; Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa William Ngeleja anapenda niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa siku ya tarehe

8 ambayo ni Jumapili kutakuwa na Tamasha la Pasaka 2018, Mkoani Dodoma na limeandaliwa na Kampuni ya *Msama Promotions* yenye lengo la kusherehekea Sikukuu ya Pasaka pamoja na kumsifu Mungu hiyo tarehe 8 Aprili, 2018, Mkoani Dodoma. Litafanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 7.00 mchana mpaka saa 1.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge kama sehemu muhimu kwa tamasha hili mnaombwa mijumuike na wageni wetu hawa. Kutakuwa na kiingilio kidogo tu cha Sh.3,000 kwa kila mtu lakini wanatuomba sana, mtaviona vipaji kwa upande wa nyimbo za dini, wapo waimbaji wa ndani wa nyimbo za injili lakini pia na wa kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana. Tumshukuru Mheshimiwa Ngeleja Mwenyekiti wetu kwa kutuletea hayo. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine, niwatakie mapumziko mema ya *weekend* hii, lakini tukikumbuka kesho historia ya Tanzania ni siku muhimu. Ni maombolezo lakini ni ya kihistoria kwa maana ni siku ambayo Hayati Mzee Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar alifariki dunia. Kwa hiyo, tarehe 7 Aprili pamoja na tarehe 14 Oktoba ya kila mwaka huwa zina maana sana kwa Tanzania. Kwa sura hii ya Muungano naomba tumkumbuke Mzee wetu huyu katika maombi yetu aendelee kulala mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 9 Aprili, 2018, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.45 Usiku Bunge lillahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 9 Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)